# Nipashe

Jumatano Machi 22, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581257

www.ippmedia.com

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS.1,093,395,265

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




## Wafa kwa kuungua na joto la gesi

UKURASA 3



Anayoyafanya Rais yanaonekana mchana, hata gizani kwa ukamilifu — Ukurasa 12

Japo ametangulia ameacha zawadi nono — Ukurasa 14

siasa

JUMATANO MACHI 22, 2023 Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

Utata uliojivika katika siasa ya uchumi kati ya Russia na Ulaya — Ukurasa 13

Kambaya anapochomoka akitimkia rasmi CHADEMA

• Awatabiria kifo 'watesi' wake CUF, Msajili, CUF wamjibu aambiwa 'shiii'

Na Sabato Kasika

"NI maamuzi magumu, ila imebidi iwe hivyo, kwani muda muafaka ndiyo umewadia, sijali wangapi watalia, lakini ni lazima maisha ya siasa yaendelee hata kupitia vyama vingine, si lazima kufanyia ndani ya CUF tu".

Hivyo ndivyo mwanasiasa machachari Abdul Kambaya, ambaye amewahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi, katika Chama cha Wananchi (CUF), kabla ya yeye na wenzake kutimuliwa mwanzoni mwa mwaka 2021.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kambaya ambaye sasa amejiunga na CHADEMA, anasema ameachana na kesi aliyofikisha katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, akipinga kuvuliwa uanachama wa CUF na sasa anasonga mbele.

"Kesi inakaa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa zaidi ya mwaka mmoja bila kutolewa uamuzi, nimeona isiwe shida, niachane nayo na nijiunge na chama kingine niendelee na harakati zangu za kisiasa," anasema Kambaya.

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema kauli ya Kambaya haiwezi kuyumbisaha wanachama wa CUF kwa mambo yasiyokuwa na msingi na kwamba badala yake wataendelea kuungana katika kukiimarisha chama hicho.

"Chama hiki kiko imara na kitaendelea kuimarika kutokana na uwezo wa viongozi wake ambao wamepata sifa kutokana na umahiri wao wa masuala ya uchumi na siasa," anaeleza.

Anasema chama hicho siku zote kimekuwa mstari wa mbele, katika kusimamia misingi ya haki na usawa kwa wote na kwamba kitaendelea kufanya hivyo kwa wanachama wake na wapenzi wa CUF.

KIGUGUMIZI MSAJILI

Hata hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Francis Mutungi, anapoulizwa kuhusu tuhuma zinazoelekezwa kwake, kuhusu kumkumbatia. Profesa Lipumba, anasema kwa kifupi kuwa 'no comments'.

"Huyo mtu wako si kashahamia CHADEMA? Mambo ya CUF awaachie wenyewe...

UKURASA 11

# TAHADHARI

## • Wauzaji kitoweo wadaiwa kuchakachua mizani... *Ukurasa 2*





Mwonekano wa sehemu ya Barabara ya Morogoro ya njia nane kutoka Kimara hadi Kibaha (km 19.2), jijini Dar es Salaam jana. Ujenzi wa barabara hiyo, umefikia asilimia 98 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa Aprili, 2023. **PICHA: WUU**

## ACT yadai Watanzania 11 wamefariki dunia Msumbiji

UK. 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 2

### UGONJWA ULIOUA WATU WATANO MKOANI KAGERA WAGUNDULIKA

SERIKALI imesema uchunguzi wa kimaabara kuhusu ugonjwa uliosababisha vifo vya watu watano mkoani Kagera umegundua kuwa...

UKURASA WA 4

### KINANA AKEMEA MAKUNDI UWT

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amekemea makundi ndani ya Umoja...



UKURASA WA 5

### WAANDISHI NIPASHE WASHINDA TUZO

SHIRIKA la Merck Foundation ambalo ni tawi la Merck KGaA, kwa kushirikiana na Wake wa Marais wa Afrika limewatangaza waandishi wa habari wa gazeti la Nipashe linalochapishwa na...

## Lissu ataka muswada wa sheria Katiba mpya kupelekwa rasmi bungeni

UKURASA 3

MICHEZO **SIMBA: TUNAVUNJA MWIKO CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Wauza nyama wadaiwa kuchakachua mizani

**Na Christina Mwakangale**

BAADHI ya wakazi wa jijini Dar es Salaam, wamelalamika kupunjwa nyama wanapokwenda kununua buchani kwa madai ya mizani kuchakachuliwa.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wakazi hao walidai wauzaji wa kitoweo hicho wanatumia mwanya wa kutokaguliwa kwa mizani hiyo mara kwa mara kwenye mabucha hayo kutoka mamlaka husika.

Mmoja wa wakazi hao, Philbert Msaki, alisema ana utaratibu wa kununua nyama kwenye bucha za eneo moja na hununua eneo la Mwenge, wiki iliyopita alinunua kilo tano, lakini alipofika nyumbani na kuipima akabaini kupunjwa robo kilo.

"Ni kawaida yangu kununua nyama kwenye eneo la Mwenge, nilipofika kwa ajili ya kununua nyama ya matumizi ya nyumbani kwangu nilibaini nimepatiwa kilo 4.75 niligundua kwa kuwa nina mzani wangu nyumbani," alisema Philbert.

Alisema pia alibaini bei ambayo hubandikwa nje ya bucha hizo, haiendani na anayotakiwa kulipia baada ya kuuziwa nyama.

"Mfano utakuta bucha nyingi zinabandika bei nje ya bucha, sijui ni kumvutia mteja au sheria inawataka hivyo kama vile wauzaji wa bidhaa ya mafuta kwenye vituo. Najiuliza wale madalali nje ya bucha wanafanya nini?

"Nilipofika buchani kuna madalali wanakwambia bei ya nyama Sh. 10,000 kilo moja na kwenye ubao inaonyesha Sh. 9,000. Hii maana yake nini iandikwe na kutajwa nyingine, mamlaka ifuatilie hili, kwa sababu tunapunjwa na bei hazikosawia," alilalamika Philbert.

Kadhalika, alisema bucha nyingi zinatumia mizani wa kidigitali ambao wateja wasio na uelewa ni rahisi kurubuniwa uzito halali wa bidhaa wanayonunua.

Musa Baruani, mkazi wa Mtaa wa Mazizini, Ukonga Mombasa jijini hapa, alisema hununua kitoweo hicho kila wiki ingawa amebaini uzito wa kilo moja kati ya bucha moja na nyingine hutofautiana.

"Unajua hata hizi pesa tunazitafuta kwa tabu sana, hata mambo mengine hatufuatilii lakini kumbe yanatugusa. Hii kupunjwa kilo ya nyama ipo, ila utathibitishaje na mnunuzi na muuzaji, zaidi muuzaji atajitetea, sasa mimi mwananchi wa kawaida nina utaalamu gani? Nitachukua nyama niwapelekee wanangu wale tu," alisema Musa.

Naye Zainab Ismail, mkazi wa Tegeta alisema mchezo wa kuchezea mizani upo pia kwenye mabucha ya eneo hilo hali inayowaumiza wananchi.

"Nilinunua nyama kwenye bucha moja pale Tegeta wameandika kilo ni Sh. 7,000 nilipoipima nyumbani nikakuta nimepunjwa robo nzima, kuna wizi sana na mamlaka hazifuatilii, ukiona umepunguziwa bei jua hapo unauziwa pungufu," alisema.

Akizungumzia suala hilo, Meneja wa Wakala wa Vipimo (WMA) Mkoa wa Ilala, Alban Kihulla, alisema mwishoni mwa wiki walifanya ukaguzi wa kushtukiza ambao upo kisheria, kuangalia matumizi ya vipimo kama ni sahihi.

"Tulifanya ukaguzi kwenye mabucha ya nyama, Mkoa wa Dar es Salaam, tulitembelea bucha 21 na kati ya hizo nne tukagundua kuna udanganyifu unatokea kwa kutoa nyama kidogo kwa mwananchi anayenunua. Tulibaini mtu anayenunua kilo mbili, anapunjwa nusu kilo, ukipiga hesabu mtu anayenunua kilo 10 anapunjwa karibu kilo nne.

"Tumegundua tatizo ni kubwa, bado lipo, kwa mujibu wa sheria tutafanya kazi usiku na mchana, ili mwananchi apate thamani ya kiasi cha fedha na bidhaa, hatua zitachukuliwa kwa hawa, ili tatizo hili kuhakikisha linakoma," alisema Alban.

Aliwatahadharisha wauazaji wa kitoweo hicho kuuza bidhaa yenye uzito sahihi na wamiliki wa maduka hayo watahusika moja kwa moja na mashtaka iwapo kuna ukiukwaji wa utaratibu kisheria.

"Mmiliki atakuta anasema anayehusika ni muuzaji, lakini kama kuna mashtaka moja kwa moja mmiliki unahusika na ndio tunakufahamu, wamiliki wahakikishe mizani yao iko sahihi," aliongeza Alban.

Kwa mujibu wa Mkataba wa Huduma Kwa Wateja 2020 wa Wakala wa Vipimo katika Wizara ya Viwanda na Biashara, unaelekeza kufanyika hatua kadhaa za uhakiki na ukaguzi wa vipimo wa bidhaa zote rasmi za kitaifa, ili kujenga haki ya mtumiaji, huku mzalishaji akitekeleza yale yaliyoidhinishiwa kiserikali na si vinginevyo.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa kwenye mazungumzo na Mtendaji Mkuu na Rais wa Kampuni ya Barrick Gold Corporation, Mark Bristow (wa pili kushoto), Ikulu Chamwino mkoani Dodoma juzi. Baada ya kupokea mfano wa hundi yenye thamani ya Dola za Marekani 30,000,000 kutoka kwa Mtendaji huyo kwa ajili ya shughuli mbalimbali za elimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT: Watanzania 11 wamefariki Msumbiji

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimedai kuwa kuna vifo 11 vya wavuvi waliokuwa mahabusu na Watanzania wengine 17 wanashikiliwa gerezani nchini Msumbiji kwa miaka sita sasa.

Kutokana na kuwapo kwa taarifa hizo, kimeiomba serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kutoa ufafanuzi kuhusu hali ya Watanzania walioko nchini humo kwa sasa. Pia kimedai kuna ukimya wa serikali kuhusu vifo na mahabusu hao.

Waziri wa Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, aliiambia Nipashe kwa njia ya simu kwamba kama chama hicho kina taarifa za kuaminika, iziwasilishe wizarani ili zifuatiliwe na kutolewa majibu.

"Wamewasiliana na wizara? Walete kwetu tutawapa majibu. Wao wameleta gazetini, walete hizo taarifa tuzifuatilie tutawapa majibu," alisema Waziri Tax.

Katika taarifa iliyotolewa jana, Waziri Kivuli wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa chama hicho, Dk. Nasra Nassor Omar, alitaka serikali itoe ufafanuzi kuhusu Watanzania hao na iwajibike kuwanusuru na izifute machozi familia zilizoathirika.

Alidai kuwa pamekuwapo na ukimya kutoka serikalini kuhusu kukamatwa kwa wavuvi 24 waliotoka Zanzibar na boti mbili za uvuvi na Watanzania wengine tangu Agosti, 2017. Dk. Nasra alidai kuwa wavuvi hao walipatiwa vibali mapema Septemba 2017, kwa ajili ya kufanya shughuli za uvuvi, kupitia Bahari ya Hindi.

"Mwezi mmoja baadaye, yaani Oktoba 2017, kulitokea machufuko Msumbiji ndipo wavuvi 24 na Watanzania wengine 13 waliokuwa kwenye shughuli mbalimbali, walikamatwa na kuwekwa magerezani.

"Ukimya wa serikali unaibua simanzi, sintofahamu na kushusha imani za ndugu, jamaa na marafiki kuhusu hatima ya ndugu zao waliopo vizuizini," alidai.

Pia alidai kuwa chama hicho kimefuatilia suala hilo na kubaini kuwa kati ya Watanzania hao, wavuvi tisa tu (wakitaja majina yao) ndio wamerudi nyumbani na 11 ikisemekana wamefariki dunia wakiwa gerezani.

Dk. Nasra alidai kuwa mpaka sasa, wavuvi wanne kutoka Zanzibar na Watanzania wengine 13 (wakitaja majina yao), bado wapo gerezani.

"Kwa masikitiko makubwa imepita miaka sita, hakuna taarifa ya kupelekwa mahakamani Watanzania hao, wavuvi 11 walifariki wakiwa magerezani, hakuna taarifa ya uhakika kuhusu sababu ya vifo vyao," alidai.

Dk. Nasra alidai kuwa licha ya taarifa za Watanzania wanaoshikiliwa katika magereza kufahamika na ofisi za uhamiaji na ubalozi, hakuna jitihada za makusudi za kuwatafutia haki wa miaka sita sasa.

Kutokana na kuwapo kwa madai hayo, chama hicho kimependekeza kuwa serikali ifuatilie tuhuma za Watanzania hao na wengine 11 waliofariki dunia.

"Ijulikane sababu ya vifo vyao na haki zao zipatikane na waliopo magerazani serikali ihakikishe wanarejeshwa nyumbani na pamoja na boti zao za uvuvi," ACT-Wazalendo kimependekeza.

Pendekezo lingine lililotolewa alilitaja kuwa ni serikali za nchi hizo mbili, ziunde ukanda maalumu wa kiuchumi ili kutoa fursa kwa vijana kufanya shughuli halali, kuzuia vijana kushawishiwa kujiunga na makundi ya yanayotishia amani na utulivu wa nchi.

# Ugonjwa ulioua watano Kagera wagundulika

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema uchunguzi wa kimaabara kuhusu ugonjwa uliosababisha vifo vya watu watano mkoani Kagera umegundua kuwa unatokana na kirusi cha Malberg ambacho asili yake ni mji huo ulioko nchini Ujerumani.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akitoa taarifa za uchunguzi wa ugonjwa huo kwa waandishi wa habari, ambao watu wanane waliripotiwa kuugua Machi 16, mwaka huu.

Alisema mpaka sasa serikali imefanikiwa kuudhibiti ili usienee maeneo mengine na inaendelea kuwafuatilia watu wengine 161 wanaohisiwa kuchangamana na wagonjwa hao.

"Uchunguzi tuliofanya katika maabara yetu, umethibitisha kuwapo kwa virusi Malberg, ambavyo viligundulika mwaka 1967 huko Ujerumani katika mji wa Malberg ndio asili ya jina hili," alisema.

Waziri Ummy alisema ugonjwa huo huambukiza kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine hususani kwa njia ya kugusa majimaji pale mtu anapokuwa na michubuko au kidonda.

"Majimaji haya yanaweza kuwa mate, mkojo, damu, machozi au kinyesi yatokayo kwenye maiti au mgonjwa mwenye dalili. Maambukizi yanaweza kutokea kwa wanyama kwenda kwa binadamu iwapo mtu atagusa mizoga au mnyama anayeumwa," alisema.

Alitaja dalili kuwa ni kutapika, kuharisha, kutoka damu sehemu za mwili na kwamba hauna tiba mahususi zaidi ya zile za kuumwa kulingana na eneo la mwili.

"Hadi kufikia siku ya leo (jana) ikiwa ni siku tano tangu kuripotiwa kwa watu wenye dalili hizo, watu waliothibitika kuwa na ugonjwa huu ni watu wanane na kati yao vifo ni vitano," alisema.

Waziri Ummy alisema wagonjwa watatu wanaendelea na matibabu katika vituo vilivyoandaliwa mkoani humo Kagera.

"Ninawashukuru wananchi kwa kutoa taarifa za ugonjwa huu, tarehe 16, Machi nilipokea jumbe nyingi kutoka kwa wananchi, tunawashukuru kwa kutoa taarifa, ninawasihi wananchi kutoa ushirikiano kwa wataalam, hadi sasa serikali imefanikiwa kudhibiti usisambae nchini," alisisitiza.

HABARI KITAIFA

# Wafa kwa kuungua na joto la gesi

Na Pilly Kigome

WATU wawili wamefariki dunia baada ya kuungua wakiwa ndani ya nyumba kwa moto unaodaiwa kusababishwa na gesi iliyowashwa na kuachwa bila kubandika kitu.

Tukio hilo linadaiwa lilitendwa na mmoja wa wanafamilia hali iliyowafanya watu hao kuungua kwa joto lililoathiri miili na kushindwa kupumua kwa kukosa hewa safi.

Tukio hilo lilitokea mwishoni mwa wiki iliyopita katika Mtaa wa Mabibo Farasi, eneo lijulikanalo kama Gombe, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Shina namba 19, Geoffrey Masawika, alisema tukio lilitokea Machi 18, mwaka huu, na inadaiwa Eliza Fares (31) aliwafungia mwanawe na mdogo wake ndani ya nyumba huku jiko la gesi likiwa limewashwa.

Masawika aliwataja walioungua na baadaye kufariki dunia wakiwa wanapatiwa matibabu ni mtoto wa mtuhumiwa huyo, aliyefahamika kwa jina la Esta na mdogo wake aitwaye Tabitha Fares (23).

Alisema siku ya tukio, Eliza kabla ya kulipua nyumba hiyo, alianza kumpiga mdogo wake huyo, ambaye sasa ni marehemu, kwa kile kilichodaiwa ni kumchoka kwa kuwa alikuwa na ulemavu wa akili na baadaye kudaiwa kwenda kuwasha moto katika moja ya vyumba ambacho kilikuwa na vitu vingi yakiwamo makabati ya nguo na vitu vingine vya nyumbani.

Mjumbe huyo anayeishi jirani na nyumba hiyo, alisema kabla ya kulipuka kwa moto huo, majira ya saa 6:00 adhuhuri, kulikuwa na kutokuelewana ndani ya nyumba.

Alisema ndani ya muda mfupi alimwona mzazi wa mtuhumiwa aliyetambulika kwa jina la Gati Wangwe (60) akikimbilia ndani akatoka na jiko la gesi dogo na kulipeleka nyumba ya jirani.

Masawika alisema ndipo majira ya saa 8:20 mchana ilisikika sauti ya mmoja wa majirani karibu na nyumba hiyo aliyefahamika kwa jina moja la Mama Fei akipiga kelele na mayowe kuwashtua majirani wengine kuwa kuna moto unawaka ndani.

"Ndipo mimi na wajumbe wengine na majirani tulifika eneo hilo na kukuta milango na mageti yote yamefungwa. Tulivunja dirisha na kuwaokoa wahanga (waathirika) hao ambao walikuwa bado wako hai, lakini walikuwa na hali mbaya sana,"alisema.

Wakati wanaendelea kuvunja, alisema walikuwa wanawasiliana na polisi kuwajulisha tukio hilo na baadaye askari walifika eneo hilo wakavunja dirisha na kuwatoa binti na mtoto huyo. Alisema waliwatoa watu hao ambao miili yao ilishaungua na kuwapeleka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Pia alisema wananchi wenye hasira kali walianza kumsaka mama mwenye nyumba na walipompata walimpiga wakimhusisha na tukio hilo.

Alisema mtuhumiwa awali alipelekwa kituo kidogo cha polisi Mabibo kisha kuhamishiwa Urafiki na baadaye kupalekwa Kijitonyama (Mabatini) ambako yuko hadi sasa.

Inadaiwa kuwa wiki tatu zilizopita Eliza aliunguza godoro katika moja ya vyumba na kusababisha moto mkubwa kulipuka lakini majirani waliuzima kisha kumkamata mtuhumiwa huyo na kumpeleka Kituo cha Polisi Urafiki.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Mabibo Farasi, Andrew Kibuya, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo katika eneo lake.

Mmoja wa ndugu ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema Eliza amekuwa na mambo mengi na matukio mengi ya kutisha na tukio hilo halikuwa la kwanza kufanya.

Mjomba wa mtuhumiwa aliyejitambulisha kwa jina la Medan James (65) aliiambia Nipashe kuwa kutokana na vitendo vinavyofanywa na Eliza, wanafamilia wameshachoshwa, hivyo wanaiomba serikali kuchukua sheria na kuongeza kuwa majirani hawahitaji tena kuendelea kuishi mtaani hapo kwa kuwa woga umeshawaingia kutokana na vitendo vyake.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni, ambaye simu yake haikupatikana.

# Lissu ataka muswada wa sheria Katiba mpya kupelekwa bungeni

Na Elizabeth Zaya

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, ameshauri serikali kupeleka muswada wa sheria kurejesha mchakato wa Katiba mpya katika bunge lijalo.

Lissu alisema hayo hivi karibuni wakati akihojiwa kwa njia ya mtandao na kituo kimoja cha televisheni nchini.

Katika mahojiano hayo, Lissu alisema hataamini maneno ya Rais Samia kuwa atarejesha mchakato wa Katiba, bali kwa kufanya kwa vitendo akianza kwa kupeleka muswada bungeni lijalo.

"Tunataka Rais na serikali yake apeleke muswada mwezi ujao kwenye bunge linaloanza hivi karibuni. Anatuambia maneno matamu, tunataka vitendo na mimi nitamwamini akifanya kwa vitendo," alisema Lissu ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Singida Kaskazini.

"Kwenye hili inabidi tuwe kina Tomaso (mwanafunzi aliyesema hataamini kama Yesu Kristo amefufuka mpaka atakapomwona). Anachohitajika kufanya Rais katika hili ni kuenenda kwa vitendo hizo kauli zake tamu. Kauli ni tamu, matendo ni bora zaidi, akifanya hivyo tutasema mama ameanza kwa vitendo kutekeleza maneno yake. Asipofanya hivyo, tutamwambia maneno matupu hayavunji mfupa," alisisitiza.

Januari mwaka huu, Rais alitangaza kuondoa zuio la mikutano ya hadhara iliyokuwa imepigwa marufuku takriban miaka saba iliyopita huku akiahidi kwamba serikali yake inadhamiria kukwamua mchakato wa Katiba mpya, uliokwama kwa zaidi ya miaka minane tangu mwaka 2014.

**USALAMA WAKE**

Kuhusu usalama wake, Lissu alisema hana shaka tena na kwamba amethibitisha hilo aliporudi nchini Januari, mwaka huu.

"Hali ya usalama wangu binafsi nchini Tanzania imekuwa nzuri ukilinganisha na kipindi kingine cha nyuma, nilivyorudi nyumbani Jeshi la Polisi walinipa ulinzi wa kutosha. Nafikiri kusema haya ni sahihi kwamba hali ya usalama ni nzuri tofauti na ilivyokuwa,"alisema Lissu.

Akizungumzia sababu ya kwenda tena Ubelgiji baada ya muda mfupi tangu aliporejea nchini, alisema alilazimika kufanya hivyo kwa ajili ya kwenda kuonana na daktari wake.

"Kilichonirudisha mapema Ubelgiji ni yatokanayo na shambulio la mwili wangu ambao una vyuma vingi sana vilivyowekwa na madaktari. bado kuna risasi moja imebaki mahali fulani karibu na uti wa mgongo. Kwa sababu ya yote hayo, inahitaji uangalizi wa mara kwa mara wa madaktari.

"Wakati nakuja nyumbani Januari, tayari nilikuwa nina ahadi ya kuonana na daktari Februari 20 na jumanne (jana) nitakwenda kuonana naye tena," alisema.

Lissu alisema alilazimika kurejea mapema Tanzania kabla ya kumaliza ratiba ya kuonana na daktari wake kwa sababu ya ufunguzi wa mikutano ya hadhara ambayo walikubaliana ndani ya chama chao.

"Na kilichonifanya nirudi nyumbani badala ya kusubiri mpaka nimalizane na daktari wangu ni baada ya mikutano ya hadhara kuruhusiwa, chama kilipanga ratiba ya kuanza mikutano ndani ya wiki mbili.

"Tulishauriana kama viongozi kwamba kwa kuwa mikutano imeruhusiwa itakuwa vizuri kwa sisi wengine tuliokuwa tumekimbia turudi ndiyo maana ilibidi nirudi kwa sababu tulikubalina niwapo nyumbani wakati mikutano inaanza rasmi. Chama kilikuwa kinajua kwamba baada ya hapo nitarejea kuja kuonana na madaktari.

"Kwa hiyo hayo ndiyo mambo ambayo yanasababishwa na hali halisi ya afya yangu, ili nifanye shughuli zangu vizuri ni lazima niwe na afya njema," alisema.

**MADAI YA MPASUKO**

Alipoulizwa na Nipashe kuhusu maneno yanayozungumzwa ya madai ya kuwapo kwa mpasuko ndani ya CHADEMA, Lissu alisema hayo ni maneno ambayo yamekuwa yakizungumzwa miaka mingi.

"Tumeambiwa kuwa tuna mpasuko tangu nilipojiunga na CHADEMA mwaka 2004! Siyo swali jipya hata kidogo,"alisema Lissu.

MAGNIS ENERGY TECHNOLOGIES

URANEX NACHU GRAPHITE PROJECT

**REQUEST FOR EXPRESSION OF INTEREST (EOI) RE-ADVERTISED**

**Title of the EOI: Construction of Storm Water Dam (Pre-Qualification EOI)**

**Date of this EOI: 22nd March 2023**

**Closing Date for Receipt of EOI: 6th April 2023**

**Address EOI Response by E-mail to the Attention of: Procurement Unit**

**E-mail Address: uranex.tanzania@gmail.com**

**DESCRIPTION OF REQUIREMENTS**

1. Uranex Tanzania Limited a subsidiary of Magnis Energy Technologies Limited is issuing this Request for Expression of Interest (REOI) to seek interest from qualified Local and International Companies/Contractors with required expertise and experience, domestically situated for pre- qualification as a potential Main Contractor for the construction of Storm Water Dam at the Nachu Graphite Project located in Ruangwa, Lindi Region Southern of Tanzania.
2. Contractors expressing interest should note that this REOI serves as a pre-qualification of the Companies that will be invited to participate in the Bidding process that will follow. As explained in the detailed REOI (to be provided) Mandatory Requirements, only contractors that meet the minimum pre-qualification criteria set out in this REOI will be invited to participate in the ensuing competitive bidding exercise.
3. This call for EOI does not constitute solicitation. Uranex Tanzania Limited (UTL) reserves the right to change or cancel the requirement at any time during the EOI.
4. Applicants may ensure better understanding of the opportunity and the requirement of the Expression of Interest by contacting **uranex.tanzania@gmail.com**

**PRE-QUALIFICATION SELECTION PROCESS AND EVALUATION CRITERIA**

(a) Interested Vendors/Contractors will be pre-qualified through the pre-qualification evaluation criteria stipulated in the detailed REOI.

(b) Applicants/interested parties can obtain the project scope in the detailed REOI by emailing **uranex.tanzania@gmail.com**. A hardcopy will also be available at **Uranex Tanzania Limited, located along Yacht Club Road, House 19. Dar es Salaam Tanzania.**

(c) While preparing and sending their responses to this REOI, Contractors are requested to take note of important REOI dates as outlined below. Contractors will be notified in case of any changes in the dates indicated below:

(i) REOI Publication date – 22nd March 2023;
(ii) Deadline for posing REOI related questions and clarifications – 28th March 2023, 16:00hrs Tanzania local time;
(iii) Deadline for responding to REOI questions and clarifications –31st March 2022, 16:00 hrs. Tanzania Local Time;
(iv) REOI Closing Date – 6th April 2023, 16:00 hrs, Tanzania Local time.

217334502

**NOTE**
**Information of the Company's Projects is available free of charge at the following address: https://magnis.com.au/nachu- project**

# Lema aweka msimamo kauli yake kuhusu kazi bodaboda

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MBUNGE wa zamani wa Arusha Mjini (CHADEMA), Godbless Lema, amesema hajutii, na wala hatafuta kauli yake kuwa biashara ya bodaboda si kazi bali ni umaskini na laana inayoua nguvu kazi ya taifa.

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara jijini hapa, Lema ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Kaskazini, alisema ataendelea na msimamo wake huo kwa kuwa bodaboda zimeongeza idadi ya watu kupata ulemavu na wajane.

"Nasema sifuti kauli na leo tena (jana) napigilia msumari kwamba udereva bodaboda siyo kazi ya maana na watu wanazidi kuwa maskini na hii inajenga ufukara. Bodaboda zimeongeza vilema na wajane. Kila siku kuna watu wanapoteza ndugu zao na maisha kwa sababu ya ajali za bodaboda," alisema.

Machi Mosi, mwaka huu, wakati anazungumza na maelfu ya wananchi katika uwanja wa Relini jijini Arusha baada ya kuwasili kutoka uhamishoni nchini Canada, Lema alinukuliwa akisema: "Wakati ninyi mnanipokea kwa shangwe, mimi moyo wangu ulikuwa unahuzunika.


"Bodaboda siyo ajira ni umaskini uliopitiliza. Aah! jamani tukae na serikali vizuri sisi bodaboda, hiyo ni ajira ya laana ikemeeni. Hamwezi kufanya ajira ya kukimbiza upepo kwa Sh. 7,000 kwa siku, no men. Hapana,"

Lema alisisitiza kuna athari ambazo zinaweza kujitokeza baadaye kutokana na wazazi, walezi na jamii kwa ujumla kushindwa kuwalea watoto katika maadili mema, jambo ambalo linaweza kuchochea kushamiri kwa vitendo vya ukatili na kupoteza nguvu kazi ya taifa.

"Watoto wengi wanaozaliwa sasa hivi hawalelewi na wazazi wao ipasavyo kama nyakati za wazee wa zamani. Je, mmeangalia taifa hili baada ya miaka 30 nchi itakuwaje nyie? ndio maana sasa hivi tunashangaa kuna tabia zinazuka, umasikini umekuwa mkali kuwanyima nafasi kwa wazazi kuwaangalia watoto," aliongeza Lema.

Awali, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Grace Kiwelu, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua aliyochukua ya kufungua milango na kuridhia ushirikiano baina ya vyama vyote vya siasa pamoja na kuruhusu mikutano ya kisiasa.

"Niwashukuru sana viongozi wetu wa vyama viwili wa kitaifa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CHADEMA kwa kuleta maridhiano. Leo Watanzania tunazungumza, tumekuwa kwenye kifungo cha miaka saba bila Watanzania kuzungumza," alisema Kiwelu.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akimkabidhi Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Jenerali mstaafu, Davis Mwamunyange, tuzo ya ushindi kwa mamlaka iliyofanya vizuri katika uwasilishaji wa tozo ya udhibiti (EWURA Levy) jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mwenyekiti wa Bodi ya EWURA, Prof. Mark Mwandosya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kinana akemea makundi UWT

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, amekemea makundi ndani ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) katika kufanya uamuzi wa masuala mbalimbali badala ya kutumia vikao halali.

UWT kutumia makundi kuamua mambo badala ya vikao.

Kinana aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha Baraza Kuu la jumuiya hiyo ya CCM.

"Kuna watu wanakaa wawili au watatu wanatengeneza jambo lao huko nje wanaleta ndani na kudai ni jambo la kikao. Hapana, kila kitu lazima kiamuliwe na kikao na kijadiliwe kwa kina," alisema na kusisitiza kuwa shughuli zote za chama ni za vikao na uamuzi si wa mtu mmoja au kikundi cha watu.

"Kwenye chama huwezi kusema mimi nimesema. Hii ni kauli inayotolewa kwenye vikosi vya jeshi. Kwenye chama unaleta ajenda, unajenga hoja, ukishindwa unakwenda kujiandaa upya na kuiwasilisha. Kuna kitabu kinasema tujisahihishe, ukisoma kinasema mwenzako akikushinda kwa hoja salimu amri, rudi nenda kajiandae, washawishi wenzako itapita," alisema.

Aliwasisitiza kutenda haki bila kumuonea mtu na kuwapongeza viongozi wa UWT kuwa tangu wamechaguliwa kwenye ngazi mbalimbali za uongozi hajawasikia wakifarakana. Pia alisema CCM itaunga mkono UWT ili moto usipoe na kufanikisha ushindi wa CCM kwenye uchaguzi ujao.

"Hakuna jumuiya yenye nguvu iliyojipanga na inayoaminika yenye kauli, mshikamano na ya kutegemea kama UWT. Hii ni nguzo kuu ya Chama Cha Mapinduzi na kina uhakika na kazi zinazofanywa na jumuiya hii," alisema huku akiweka bayana kwamba CCM inategemea mchango na juhudi za UWT kwa kuwa inajituma na kujitolea.

Aliwahimiza viongozi wa UWT kukisemea chama na serikali kwa kila mafanikio huku akisema kila kata nchini ina alama kubwa sana ya maendeleo.

"Tunataka sasa kusikia maneno mawili kila mahali chama na (Rais) Samia (Suluhu Hassan). Tusikie mafanikio ya Rais na wala msione haya kumsemea Rais Samia. Ukienda duniani kote marais wanasifiwa," alisema.

Kinana alisema demokrasia imepanuka, uhuru umekuwa mkubwa wa kujieleza, haki imezingatiwa, hivyo kuna kila sababu ya kusifia uongozi wa Rais Samia.

"Hongereni sana Jumapili mlifanya tukio kubwa mliwashirikisha kinamama bila kujali itikadi zao. Lilikuwa jambo kubwa si kwa Tanzania tu, lilikuwa jambo lililofurahisha dunia na huu ndio uongozi wa UWT tunaoutarajia kwa sasa. Mlimheshimisha Rais aliona fahari kuwa na jumuiya kufanya hivi na ni mara ya kwanza kwenye historia ya chama hiki," alisema.

Aliwasisitiza kubeba ajenda za wanawake za kitaifa na kuwa mstari wa mbele kuwatetea na kuwasemea na CCM itawaunga mkono.

"Kuna ajenda tunazungumza kila mwaka ya 50 kwa 50 njia moja kubwa kuifikia ni wanawake kugombea nafasi zote katika vyombo vya serikali na uchaguzi wa mwakani himizeni kinamama na wasichana wagombee,"alisema.

Pia aliwataka katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025, UWT ihakikishe wanawake wanagombea nafasi zote za ubunge na chama kitawawezesha watakaokwenda kugombea kwenye majimbo.

Mwenyekiti wa Taifa wa UWT, Mary Chatanda, alisema mwaka 2025 UWT wako na Rais Samia na watamdhamini na kumchukulia fomu.

**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

**UTARATIBU WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA AJIRA ZA MUDA KWA KAYA ZA WALENGWA**

Miradi ya ajira ya muda kwa walengwa wa TASAF ni utaratibu wa utekelezaji miradi ya jamii yenye kutumia nguvu kazi, inayoshirikisha walengwa kufanya kazi na kulipwa ujira. Miradi hiyo inawezesha jamii kupata rasilmali /miundombinu inayotoa huduma na ujuzi kwa jamii kupitia ushiriki wao katika kutekeleza miradi hiyo.

Washiriki wa kazi zinazotoa ajira ya muda kwa walengwa ni watu wenye uwezo wa kufanya kazi wenye umri wa kati ya miaka 18 hadi 65. Kila kaya ambayo inashiriki katika ajira za muda kwa walengwa inaandikisha watu wawili, ambapo mtu mmoja kutoka kwenye kaya ndiye atashiriki kazi kwa wakati mmoja. Utekelezaji wa miradi ya ajira ya muda huchukua miezi sita ambapo walengwa hufanya kazi kwa siku kumi tu kwa kila mwezi. Kwa siku mlengwa anatakiwa kufanya kazi kwa muda usiozidi masaa manne ili aweze kupata muda wa kufanya shughuli nyingine.

Wazee, watu wenye ulemavu, wakina mama wajawazito na wenye watoto wadogo ambao hawajatimiza miaka miwili hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira za muda kwa walengwa. Wasimamizi wanaopanga kazi za walengwa hawatakiwi kuwapangia kazi watu hao na wanapaswa kutoa taarifa kwa wajumbe wa kamati ya usimamizi wa mradi (CMC) na Waratibu ili majina ya watu hao yaondolewe kwenye orodha ya watu walioandikishwa kufanya kazi za ajira ya muda. Kaya yenye watu ambao hawaruhusiwi kufanya kazi za ajira ya muda watapokea ruzuku ya msingi.

Uongozi wa TASAF umetoa waraka kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na Maafisa Ufuatiliaji kupitia orodha za watu walioandikishwa kufanya kazi kwenye miradi ya ajira za muda na kuwaondoa wale ambao hawaruhusiwi kufanya kazi kwenye miradi hiyo. Aidha utoaji wa elimu kwa viongozi wa jamii, wasimamizi na walengwa kuhusu taratibu za utekelezaji wa miradi ya ajira za muda kwa kaya za walengwa utaendelea kutolewa katika kipindi chote cha utekelezaji.

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano**
**MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TASAF**

217333102

HABARI KITAIFA

# Mpango akemea mamlaka za maji kufanya kazi kwa mazoea

Na Joseph Mwendapole

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango amezikemea mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira nchini kwa tabia ya kufanya kazi kwa mazoea na kuzitaka kuacha mara moja na kuongeza kasi ya utoaji wa huduma kwa ubora na kwa ufanisi.

Dk. Mpango alitoa kauli hiyo jana katika hafla ya uzinduzi wa taarifa ya utendaji wa mamlaka hizo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema licha ya juhudi kubwa zinazofanywa na serikali za utoaji wa huduma bora za majisafi, bado kuna baadhi ya mamlaka ambazo utendaji wake hauridhishi kutokana na kufanya kazi kwa mazoea na kuzoea shida za wananchi badala ya kuzitatua ipasavyo.

"Utendaji kazi wa namna hii umekuwa ukizorotesha juhudi halali za serikali za kutoa huduma ya maji kwa Watanzania. Niwatake viongozi wa wizara kuzisimamia mamlaka zinazorudisha nyuma kasi ya serikali," alisema Dk. Mpango.

Pia alitoa maagizo mbalimbali ya utekelezaji ikiwamo kudhibiti uwapo wa vishoka wanaorubuni wateja na kuwaunganisha wateja na huduma kinyume cha sheria kwa lengo la kujipatia fedha.

Dk. Mpango pia alizitaka mamlaka za majisafi na usafi wa mazingira kujiendesha kibiashara ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja pamoja na kumudu gharama za uendeshaji wa ofisi sambamba na kuhakiki ubora na usalama wa maji yanayosambazwa kwa wananchi.

Utoaji wa taarifa hiyo ya utendaji kazi kwa mamlaka ulienda sambamba na utoaji wa tuzo na vyeti kwa mamlaka za maji zilizofanya vizuri kwenye makundi mbalimbali katika mwaka wa fedha 2021/22.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) iliibuka kidedea kwa upande wa mamlaka zinazolipa tozo za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kwa wakati na kupewa cheti na tuzo.

Naibu Waziri wa Maji Maryprisca Mahundi, alisema wizara imewezesha upatikanaji wa maji kufikia asilimia 87 kwa maeneo ya vijijini na miradi 996 ya majisafi inatekelezwa.

"Utendaji kazi wa mamlaka kwa mwaka 2021/22 umeimarika kulinganisha na miaka ya nyuma huduma ya maji imeendelea kupatikana kwa wananchi wengi ingawa bado kuna kazi ya kufanya kuhakikisha huduma ya maji safi inamfikia kila Mtanzania," alisema.

Alizitaka mamlaka zote zizingatie utendaji bora wa kazi kwa kutoa huduma yenye ufanisi kwa wateja wote na kwa kuzingatia viwango vilivyopo kisheria.

Maadhimisho ya Wiki ya Maji kitaifa yalianza Machi 16 na yanafikia tamati leo yakiwa na kaulimbiu isemayo "Kuongeza Kasi ya Mabadiliko Katika Sekta ya Maji kwa Maendeleo Endelevu ya Uchumi".

# Waandishi Nipashe washinda tuzo

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Merck Foundation ambalo ni tawi la Merck KGaA, kwa kushirikiana na Wake wa Marais wa Afrika limewatangaza waandishi wa habari wa gazeti la Nipashe linalochapishwa na kampuni ya The Guardian Ltd, Christina Mwakangale na Marco Maduhu, kuwa washindi wa kwanza, Tuzo ya Afya ya mwaka 2022 kwa nchi za Afrika Mashariki.

Kadhalika, Watanzania wengine watano walioshinda tuzo hiyo ni Veronica Mrema kutoka blog ya matukio na maisha kipengele mtandaoni pamoja na Adam Gabriel Hhando kutoka CG Fm, na Mwanaisha Makumbuli kutoka Highlands Fm, kwa upande wa redio kwa nchi za Afrika Mashariki.

Habari iliyoandikwa na Maduhu na kushinda ni afya ya uzazi katika kukabiliana na vifo vya mama na mtoto na ndoa za utotoni huku Christina akishinda ripoti iliyohusu athari zinazowakumba wanaougua magonjwa yasiyoambukiza hususan presha na kisukari na mbinu za kukabiliana nayo. Shirika hilo ambalo lilitangaza kuanza kwa mashindano hayo mwaka jana na kutoa fursa kwa nchi za Afrika kushiriki, kutoka kanda mbalimbali kuwania tuzo kwa waandishi wa habari kutoka nchi za Kusini mwa Afrika; Afrika Mashariki na Afrika Magharibi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa shirika hilo, Seneta Dk. Rasha Kelej, akitangaza majina ya washindi hao jana, kwenye mkutano uliowakutanisha washindi wote, alisema lengo la mashindano hayo ni kukuza uelewa na kutoa elimu husan kwenye sekta ya afya, ili jamii kuacha unyanyapaa dhidi ya ugumba na kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa yasiyoambukiza (NCD).

Alisema washiriki wa tuzo hizo ni kutoka nchi za barani Afrika zipatazo 21 huku waliowania tuzo ya kutambua mchango wa vyombo vya habari ya 'More Than a Mother' kupinga ukatili, kusaidia elimu ya msichana, kumwezesha mwanamke washindi ni 56 na tuzo kutoa elimu kuhusu presha na kisukari ni 28.

"Washindi wa tuzo hizi wana mchango mkubwa kwenye kuelimisha umma, kuhusu ugonjwa wa presha na kisukari ili kubadili mtindo wa maisha pia katika kupiga vita unyanyapaa dhidi ya ugumba, umuhimu wa elimu ya msichana, kuwezesha wanawake."

"Washindi wote watakabidhiwa tuzo ikiwamo fedha, medali pamoja na cheti na tunawakaribisha wengine wote kushiriki na kutuma maombi ya kuwania tuzo hizo za mwaka 2023," alisema Dk. Rasha ambaye ni Rais wa Kampeni ya 'More Than a Mother' iliyoasisiwa na shirika hilo.


TRA

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

## TANGAZO KWA UMMA

**Utaratibu wa Kushughulikia Uingizaji wa Mizigo Nchini kwa Utaratibu wa Kuchangia Makasha "Cargo Consolidation & De-Consolidation"**

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuwakumbusha wananchi kwa ujumla na waagizaji wa mizigo kutoka nje ya nchi kupitia utaratibu wa kuchangia Makasha (Containers) ujulikanao kama "Cargo consolidation & De-consolidation" kwa kutumia mawakala wanaofanya shughuli hizi, juu ya umuhimu wa kuzingatia **Sheria, Kanuni na Taratibu** zinazosimamia utaratibu huo kama zilivyoainishwa kwenye sheria na kanuni; ***The Tanzania Shipping Agencies (Cargo Consolidator and De-Consolidator Regulation), G.N. No. 337 of 2018" hususani kifungu Na. 4 (1) (b), (c) na (m).***

Ni takwa la kisheria kwa mwagizaji wa mzigo anayetumia utaratibu huu kuhakikisha yafuatayo:-

**(i)** Wakala atakayemtumia kusafirisha mzigo wake ana leseni hai ya uendeshaji wa shughuli za "Cargo Consolidation & De-consolidation" inayotolewa na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC) kabla ya kuanza kufanya naye biashara,
**(ii)** Anatumia Wakala wa Forodha mwenye Leseni hai inayotolewa na TRA kupitia kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa,
**(iii)** Wakala wa Usafirishaji (Consolidator) anatoa nyaraka za kusafirisha mizigo kwa kila mchangiaji kwenye Kasha husika. Nyaraka hizi ambazo zinajulikana kama House Bill of Lading ndizo zitakazotumika kugomboa mizigo ya kila mchangiaji,
**(iv)** Anapata risiti sahihi ya huduma ya kusafirisha mizigo (EFD) kutoka kwa Wakala wa Usafirishaji pamoja na risiti ya huduma ya kugomboa mizigo bandarini ambayo inatolewa na Wakala wa Forodha.

Kwa upande wa Consolidators na De-Consolidators, wazingatie yafuatayo:-

**(i)** Kuhakikisha anafuata matakwa ya sheria tajwa hapo juu ambayo ni pamoja na kuwasilisha leseni yake ya uwakala wa usafirishaji (Consolidation & De-consolidation) kwa Kamishna wa Forodha na Ushuru wa Bidhaa ili kukamilisha taratibu za kiforodha,
**(ii)** Kuhakikisha anakuwa na nyaraka kuu ya kusafirishia mizigo husika (Master Bill of Lading),
**(iii)** Anawapatia wamiliki wa mizigo nyaraka husika ili waweze kugomboa mizigo yao bila usumbufu baada ya kuwasili bandarini,
**(iv)** Kutimiza wajibu mwingine wowote kwa mujibu wa sheria za kodi nchini zikiwemo kuwasilisha ritani za VAT, ritani za kodi ya mapato na kutoa risiti sahihi za EFD,
**(v)** Kuwa ni kosa la kisheria kwa Consolidator au De-consolidator kugomboa na kulipia kodi mizigo ya watu wengine inayoingia nchini kwa kutumia jina la Consolidator au De-consolidator badala ya jina la mwenye mzigo.

Wafanyabiashara na Umma kwa ujumla unajulishwa juu ya kuzingatia tangazo hili ili kuisaidia TRA kutimiza wajibu wake ikiwa ni pamoja na kutunza taarifa sahihi za waliopakodi nchini. Katika hatua nyingine tutafanya ukaguzi maeneo ya biashara ikiwa ni muendelezo wa ukaguzi wa kawaida kufuatilia namna wafanyabiashara wanavyoingiza mizigo yao nchini pamoja na kuhakiki nyaraka husika.

***Utekelezaji wa maagizo yaliyoko kwenye tangazo hili unaanza mara moja kwa mizigo inayoagizwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.***
***Aidha kwa wale ambao mizigo yao ipo njiani, wanapewa siku tisini (90) kuanzia tarehe ya tangazo hili wakamilishe taratibu za ugombowaji ikijumuisha ulipaji wa kodi stahiki.***

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**
**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPA KODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217327202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ubovu wa miundombinu kilio kinachoibuka mvua inaponyesha

**KILA** mvua inaponyesha baadhi ya barabara hujaa maji na kushindwa kupitika ndipo kilio cha ubovu wa miundombinu kinapoibuka.

Jumapili Jiji la Dar es Salaam lilipata baraka ya mvua katika maeneo mengi, lakini iligeuka karaha baada ya barabara nyingi kushindwa kupitika kutokana na mitaro inayopitisha maji kuziba na kushindwa kuyasafirisha sehemu husika.

Kila mvua inaponyesha watu ndio hutoa malalamiko ya ubovu wa miundombinu kushindwa kutengenezwa kwa ubora na kuleta madhara kwa jamii.

Eneo la Kariakoo ambako ni maarufu kwa biashara za maduka ya nguo na soko la vyakula, lilikumbwa adha ya kufurika kwa maji yaliyoingia kwenye maduka hayo na kusababisha hasara kubwa kwa wenye maduka hayo.

Wengine walikuwa wameagiza mzigo wa nguo wakati hata hawajaufungua ukakumbwa na dhoruba ya kuvamiwa na maji na kuleta hasara kubwa.

Wafanyabiashara hao wameilalamikia Manispaa ya Ilala kwa kushindwa kuboresha miundombinu ya mifereji ambayo hupitisha maji yasijae kwenye barabara na vile vile kusafisha mifereji hiyo kwa kuondoa taka.

Hata hivyo, Manispaa hiyo imewatupia lawama wafanyabiashara hao kwa tabia yao ya kutupa uchafu kwenye mitaro ya mifereji hiyo hali inayosababisha kuziba na maji kushindwa kupita.

Baadhi ya wafanyabiashara wanadaiwa kutupa malapulapu ya nguo kwenye mifereji hiyo na kuziba njia ya maji ambayo husababisha kujaa na kufurika barabarani.

Danadana hii ya lawama lazima ifanyiwe kazi ili kuepusha kila mvua inaponyesha ndipo kauli kama hizo kujitokeza.

Jukumu la utunzaji wa miundombinu ni la kila mtu kwa sababu madhara yakitokea hayachagui nani amesababisha hali hiyo kutokea.

Kila mmoja anatakiwa kulinda mazingira kwa kutoiharibu au kutupa taka.

Wafanyabiashara wanadai wanalipa ushuru kwa hiyo jukumu la kuhakikisha kuwa mifereji na barabara wanazotumia zinakuwa bora na salama ni la manispaa.

Lakini sisi tunasema kulipa ushuru hakuhalalishi mtu kuharibu mazingira kwa makusudi kwa kutaka kuona pesa iliyotolewa inafanyakazi gani.

Huo ni ukosefu wa uelewa na kujiangamiza mwenyewe kwa kukosa maarifa. Maji yanapofurika yanasomba vitu vingi ikiwamo uchafu wa majitaka ambayo huleta magonjwa ya mlipuko.

Maeneo mengi ambayo yametengenezwa barabara na kupendezesha mji, yanaharibiwa na baadhi ya watu kwa kugeuza mitaro ya kupitishia maji kama dampo.

Baadhi ya wafanyabiashara ndogo ndogo wanapomaliza kazi zao uchafu wote wanaumwaga kwenye mitaro hiyo na mvua inaponyesha na maji kushindwa kupita wanakuwa wa kwanza kulalamika na lawama zote zinakwenda kwa serikali.

Chakushangaza wanaofanya vitendo hivyo ni wazima wenye akili timamu. Wengine huthubutu kuchuka viroba vya taka na kwenda kuvitupa kwenye mitaro hiyo.

Viongozi wa serikali za mitaa ni wajibu wenu kusimamia mitaa yenu na kuhakikisha vitendo hivyo vinakomeshwa ili kuepusha athari za mafuriko ya kulazimishwa.

Usafi wa mitaro usisubiri kipindi cha karibu na mvua ndio isafishwe. Kila mmoja anatakiwa kuwa mlinzi wa mwenzake kuhakikisha mazingira hayachafuliwi ili kuepusha athari kujitokeza.

Mvua kubwa ikinyesha siku moja tu athari inayojitokeza ni kubwa na watu wengine kuachwa wakihangaika baada ya nyumba zao kujaa maji au kukosa njia ya kupita.

Kwa pamoja madhara haya yanaweza kuepukwa na kuwa na miundombinu salama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




**Muungwana Lazima Nilonge**



Na Sabato Kasika

# Ubia UWT, BAWACHA ufunguo enzi mpya

**MIONGONI** mwa yaliyovuta hisia hivi karibuni kwenye maadhimisho ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan, ikulu ni uwapo wa vyama vya upinzani kwenye jumuiko la kumpongeza Mama.

Kinamama hao bila kujali wanahudhuria maadhimisho hayo yaliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake -UWT, ambaye ni mpinzani wao kisiasa, wanaungana kumpongeza Rais.

Ni Jumapili iliyopita Machi 19, wanachama wa walipojumuika kuadhimisha miaka miwili ya Rais Samia ya kuliongoza taifa baada ya kifo cha John Pombe Magufuli, Machi 17, 2021.

Katika maadhimisho hayo yaliyofanyika Dar es Salaam, viongozi na wanachama wa BAWACHA -Baraza la Wanawake CHADEMA akiwamo Kaimu Mwenyekiti Sharifa Suleiman, Devotha Minja na Spika wa Bunge la Wanawake wa CHADEMA, Susan Lyimo, wanashiriki.

Hatua hiyo ya vyama kualikana, imeonyesha kuwa siasa si uadui, bali ni kupingana kwa hoja au ubishi wa kisiasa unaolenga, kuimarisha na kuleta maendeleo.

Aidha, siasa si ugomvi, badala yake ni kushirikiana, kufanikisha malengo ya kuwatumikia wananchi bila kujali itikadi za vyama ambazo wakati mwingine huchangia ubaguzi hata utengano.

Tukio la ushiriki huo limeonyesha siasa za chuki hazina nafasi, bali ushirikiano kwa lengo la kujenga nchi, hivyo kukaa pamoja na kubadilishana mawazo na uzoefu.

Lakini pia, hatua hiyo, inasaidia kupeleka Watanzania katika siasa za ushindani wa hoja na si za chuki na kisasi, ambazo kimsingi hazina manufaa kwa maendeleo ya taifa na watu wake .

Kwenye suala la maendeleo, kila mwananchi ana wajibu kwa kuzingatia kwamba maendeleo hayaletwi na siasa za chuki au uadui, bali kwa utangamano wa kisiasa bila kubaguana.

Hilo ndilo ambalo Rais Samia, analisisitiza tena kwa vitendo ikiwamo kuwateua baadhi ya wanachama wa vyama vya upinzani kushika nafasi mbalimbali za uongozi.

Pamoja na msisitizo huo wa Rais, kuna jambo la kihistoria ambalo alilifanya hivi karibuni la kuhudhuria mkutano wa BAWACHA, Siku ya Wanawake Duniani, unaofanyika mjini Moshi.

Vyama kuendelea kushirikiana, ni wazi nchi inakwenda kuzika siasa za chuki, uadui, kukamiana na kutishia demokrasia , mambo yaliyopitwa na wakati.

Mambo hayo yalisababisha baadhi ya watu kuchukiana na kuumizana, hasa kwenye kampeni za uchaguzi.

Ninaamini kuwa suala la mshikamano na maridhiano ya kisiasa ni la msingi na lingefaa kuwa wimbo wa kila mwanasiasa, ili kuendeleza upendo, amani na utulivu nchini kwa kuepuka siasa za kuwagawa Watanzania.

Kwa kuwa Rais Samia amekubali siasa za maridhiano ambazo vyama vya upinzani vimekuwa vikizitaka, ni vyema viongozi wa vyama hivyo kushirikiana ili lengo litimie.

Vyama vya siasa kualikana katika matukio mbalimbali ni msingi wa utangamano wa kisiasa unaofaa kupigiwa chapuo na kila kiongozi kwani ndiko kuimarisha umoja wa kitaifa.

Sio siri kwamba Rais ameleta suluhu kwa kuwaunganisha Watanzania bila kujadili itikadi zao za kisiasa, dini au jinsia katika kuliongoza taifa.

Rais amebainisha kuwa anaongozwa na mambo manne makuu akitaja maridhiano, ustahimilivu, mageuzi na kujenga Tanzania mpya.

Kupitia maridhiano amewaleta wote pamoja bila kujali tofauti zao akihimiza utawala wa sheria, usawa na kutobaguliwa lakini pia kuwapo fursa sawa kwa wote.

Aidha, kwa upande wa ustahimilivu,Rais anaamini katika kustahimili kwa kuhakikisha kila mmoja anapatanishwa na kupata ili kuponya majeraha na kuacha uhasama ili kuganga yajayo.

Vilevile mageuzi ya msingi ni muhimu ya kiuchumi, kisiasa na uchaguzi ambavyo vyote vitahakikisha sheria na haki zinapatikana ili Tanzania iendelee kukua na kuwezesha raia wake kumudu maisha yao.

Katika kuijenga Tanzania mpya, lengo ni kukuza uchumi, kuzalisha ajira kwa vijana, wajasiriamali, wanawake na wenye mahitaji maalumu na kudumisha uhuru na maridhiano.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# IDARA YA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA

# TAARIFA KWA UMMA

Umma unatangaziwa kwamba madai ya kurejeshewa fedha yaliyo orodheshwa hapa chini yatatambuliwa kuwa yamefutwa endapo mwombaji hatowasilisha ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai yake katika kipindi cha siku thelathini (30) tangu tarehe ya tangazo hili. Baada ya kuisha kwa kipindi tajwa, madai haya hayatakubalika tena.

| SN | CLAIMANT'S NAME | DATE CLAIM RECEIVED | AMOUNT OF CLAIM |
|---|---|---|---|
| 1 | BENEFITS LOGISTICS COMPANY LIMITED | Dec-17 | 1,809,648.00 |
| 2 | BG TANZANIA LIMITED | Dec-17 | 5,696,804.00 |
| 3 | KUEHNE + NAGEL | Dec-17 | 2,749,205.00 |
| 4 | MINISTRY OF DEFENCE & NATIONAL SERVICES | Dec-17 | 80,695,854.00 |
| 5 | RAMADHAN SALEHE | Dec-17 | 24,960,691.00 |
| 6 | SPEDAG INTERFREIGHT | Dec-17 | 3,583,229.18 |
| 7 | TATA AFRICA | Dec-17 | 52,185,352.00 |
| 8 | TOYOTA TANZANIA LIMITED | Dec-17 | 8,634,286.00 |
| 9 | TOYOTA TANZANIA LIMITED | Dec-17 | 12,520,665.00 |
| 10 | FREIGHT WORLD LIMITED | Nov-17 | 1,214,773.00 |
| 11 | FREIGHT WORLD LIMITED | Nov-17 | 388,639.30 |
| 12 | GODCHANCE GODWIN MSANGI | Nov-17 | 12,000,000.00 |
| 13 | TANESCO LIMITED | Nov-17 | 475,484,220.00 |
| 14 | WOOLWORTH TANNZANIA LIMITED | Nov-17 | 2,201,338.00 |
| 15 | EMMANUEL EDWARD LYAWERE | Sep-17 | 6,000,000.00 |
| 16 | KASSIMU MWINCHUMU | Sep-17 | 6,000,000.00 |
| 17 | KASSIMU MWINCHUMU | Sep-17 | 4,600,000.00 |
| 18 | METAL PRODUCTS | Sep-17 | 30,601,908.50 |
| 19 | MOGAS TANZANIA LIMITED | Sep-17 | 187,287,702.00 |
| 20 | QUALITY AUTOMOTIVE MECHANIZATION | Sep-17 | 112,294,726.00 |
| 21 | SHOMARI ATHUMANI | Sep-17 | 4,500,000.00 |
| 22 | ALAF LIMITED | Aug-17 | 11,921,640.00 |
| 23 | ALAF LIMITED | Aug-17 | 169,856,077.00 |
| 24 | EAST COAST OILS & FATS LIMITED | Aug-17 | 349,655,844.00 |
| 25 | KIOO LIMITED | Aug-17 | 45,000,000.00 |
| 26 | KWANZA INDUSTRIES LIMITED | Aug-17 | 4,107,721.84 |
| 27 | ORYX COMAPANY LIMITED | Aug-17 | 2,240,839,748.00 |
| 28 | VIGU TRADING COMPANY LIMITED | Aug-17 | 4,600,000.00 |
| 29 | BARNABAS J. MANDE | Jul-17 | 4,800,000.00 |
| 30 | DHL LOGISTICS | Jul-17 | 492,829.00 |
| 31 | SOLOMON IGNASS MBUNDA | Jul-17 | 4,600,000.00 |
| 32 | AZAM BAKERIES LTD | Jun-17 | 83,591,239.00 |
| 33 | RAINBOW | Jun-17 | 5,006,905.00 |
| 34 | TANZANIA BREWERIES | Jun-17 | 60,790,997.00 |
| | | | **4,020,672,041.82** |

| SN | CLAIMANT'S NAME | DATE CLAIM RECEIVED | AMOUNT OF CLAIM |
|---|---|---|---|
| 1 | AG ENERGIES CO. LTD. | Dec-18 | 32,144,142.00 |
| 2 | ALLMOL FREIGHT SERVICES | Dec-18 | 59,572,101.00 |
| 3 | BUSINESS CONGOLESE INTERNATIONAL | Dec-18 | 15,444,000.00 |
| 4 | CHABRUMA & CO. LTD. | Dec-18 | 9,916,357.50 |
| 5 | REYNOLD CONSTRUCTION CO. LTD. | Dec-18 | 20,448,000.00 |
| 6 | TATA AFRICA HOLDING (T) LTD. | Dec-18 | 23,785,798.00 |
| 7 | ABB | Nov-18 | 46,319,344.00 |
| 8 | CHINA RAILWAY SEVENTH GROUP CO. LTD. | Nov-18 | 2,552,927.00 |
| 9 | HENGAN SANITARY & BABY PRODUCTS CO. LTD. | Nov-18 | 18,506,765.44 |
| 10 | LABAN L. MWALUGAJA | Nov-18 | 500,000.00 |
| 11 | METEPLAN INTERNATIONAL LTD. | Nov-18 | 2,290,830.00 |
| 12 | METRO AGRO MACHINERY AND SPARES | Nov-18 | 10,529,290.00 |
| 13 | PROFESSIONAL FREIGHT FORWARDERS | Nov-18 | 6,088,072.00 |
| 14 | RURAL ENERGY AGENCY | Nov-18 | 1,868,821,710.00 |
| 15 | COCA-COLA KWANZA LIMITED | Oct-18 | 10,443,813.00 |
| 16 | DHL | Oct-18 | 10,642,027.00 |
| 17 | GREATLAKES FREIGHT LIMITED | Oct-18 | 221,610.17 |
| 18 | J. D. PHARMACY | Oct-18 | 838,217.00 |
| 19 | KIJITONYAMA PENTECOST CHURCH | Oct-18 | 453,522.00 |
| 20 | SUMITOMO MITSUI CONSTRUCTION CO. LTD | Oct-18 | 158,585,362.88 |
| 21 | SUMITOMO MITSUI CONSTRUCTION CO. LTD | Oct-18 | 349,834,887.04 |
| 22 | VITAFOAM (T) LTD | Oct-18 | 4,161,722.00 |
| 23 | YAPI YAPI MERKEZ | Oct-18 | 429,910,532.60 |
| 24 | 21ST CENTURY FOOD & PACKAGING LTD | Sep-18 | 8,538,534.00 |
| 25 | 21ST CENTURY FOOD & PACKAGING LTD | Sep-18 | 3,029,919.70 |
| 26 | ACCESS AGRO | Sep-18 | 44,126,422.00 |
| 27 | ASSOCIATION OF JEHOVAH'S WITNESSES OF TANZANIA | Sep-18 | 2,000,331.00 |
| 28 | KCB BANK | Sep-18 | 19,344,643.00 |
| 29 | LAST CHOICE CLEARING AND FORWARDING | Aug-18 | 1,432,487.00 |
| 30 | MOGO FORWARDERS LTD | Aug-18 | 15,371,613.00 |
| 31 | MOGO FORWARDERS LTD | Aug-18 | 17,376,606.00 |
| 32 | OM MANUFACTURER & TRADERS | Aug-18 | 68,949,578.80 |
| 33 | POWER CORNER | Aug-18 | 52,208,131.00 |
| 34 | TANZANIA COMMODITIES TRADING | Aug-18 | 5,489,408.00 |
| 35 | TANZANIA PRESBETARIAN CHURCH | Aug-18 | 48,660,062.00 |
| 36 | AGRIPRO TANZANIA LTD | Jul-18 | 3,070,201.00 |
| 37 | GRAND MOVERS CO. LTD | Jul-18 | 682,341.00 |
| 38 | ACER PETROLEUM (T) LTD | Jun-18 | 541,174.00 |
| 39 | AFRICA PROPER EDUCATION NETWORK | Jun-18 | 2,651,396.00 |
| 40 | CYCLE WORLD TRADING COMPANY | Jun-18 | 409,378.00 |
| 41 | JAMES WILBERT KAJI | Jun-18 | 550,000.00 |
| 42 | ANCHOR CLEARING AND FORWARDING | May-18 | 4,094,259.00 |
| 43 | BAM INTERNATIONAL | May-18 | 36,319,056.00 |
| 44 | BAM INTERNATIONAL | May-18 | 46,673,128.00 |
| 45 | RIM ZONE TRADING CO. LTD | May-18 | 1,973,880.00 |
| 46 | RUDOLF VICTORIA TEMBA | May-18 | 760,000.00 |
| 47 | SPEDAG INTERFREIGHT | May-18 | 5,170,631.00 |
| 48 | TOPMAX TANZANIA LTD | May-18 | 29,640,922.00 |
| 49 | TRADE KINGS TANZANIA PTY LTD | May-18 | 279,249,693.00 |
| 50 | Z & A TRADING COMPANY LTD | May-18 | 23,777,553.94 |
| 51 | EPIROC | Apr-18 | 10,244,580.00 |
| 52 | FORWARD AIR | Apr-18 | 641,716.00 |
| 53 | K & K CARGO LOGISTICS (T) LTD | Apr-18 | 541,914.80 |
| 54 | POSITIVE INTERNATIONAL | Apr-18 | 10,138,723.00 |
| 55 | STAR OIL (T) LTD | Apr-18 | 65,009,071.00 |
| 56 | SULEIMAN MARANDO | Apr-18 | 450,000.00 |
| 57 | TANESCO | Apr-18 | 3,969,523.00 |
| 58 | TWIGA CEMENT COMPANY | Apr-18 | 67,847,555.17 |
| 59 | BAM | Mar-18 | 35,618,712.00 |
| 60 | BAM | Mar-18 | 50,766,136.00 |
| 61 | BENEFITS LOGISTICS CO. LTD | Mar-18 | 3,243,536.00 |
| 62 | BENJAMIN MASOTA INVESTMENT | Mar-18 | 47,326,071.00 |
| 63 | BERNABEU COMPANY LTD | Mar-18 | 11,943,382.00 |
| 64 | EFATHA MINISTRY | Mar-18 | 611,499,600.00 |
| 65 | EVERWELL & ENGINEERING LTD | Mar-18 | 21,422,141.00 |
| 66 | MOSHI LEATHER INDUSTRIES LTD | Mar-18 | 3,355,717.00 |
| 67 | MOUNT MERU PETROLEUM LIMITED | Mar-18 | 5,398,294.00 |
| 68 | MOUNT MERU PETROLEUM LIMITED | Mar-18 | 6,368,210.00 |
| 69 | TANPACK TISSUES LIMITED | Mar-18 | 3,743,192.00 |
| 70 | THE JANE GOODALL INSTITUTE TANZANIA | Mar-18 | 6,533,770.00 |
| 71 | TOYOTA TANZANIA LIMITED | Mar-18 | 7,795,124.81 |
| 72 | TRANSNET FREIGHT | Mar-18 | 5,955,656.00 |
| 73 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | Mar-18 | 7,224,442.00 |
| 74 | ALPHA CHOICE LTD | Jan-18 | 9,129,476.00 |
| 75 | DR. JOB GAYO OOGA | Jan-18 | 404,692.00 |
| 76 | EAST COAST OILS AND FATS LTD | Jan-18 | 128,406,730.39 |
| 77 | EMIL & JOAS LOGISTICS (EA) LTD | Jan-18 | 27,563,759.00 |
| 78 | ENGEN PETROLEUM | Jan-18 | 12,288,746.82 |
| 79 | IMPACT TRADING AND INVESTMENT | Jan-18 | 9,606,534.00 |
| 80 | JENIFA ABRAHAM KIMARIYO | Jan-18 | 60,014,677.00 |
| 81 | KENTAN LOGISTICS LTD | Jan-18 | 686,669.00 |
| 82 | NAHASHA S. MWASOYA | Jan-18 | 270,000.00 |
| 83 | NIC BANK | Jan-18 | 26,939,412.00 |
| 84 | NYOTA TANZANIA LTD | Jan-18 | 16,949,800.00 |
| 85 | OLAM | Jan-18 | 20,864,021.00 |
| 86 | SANDVIK | Jan-18 | 17,371,157.00 |
| 87 | SENKONDO'S EXPORT & IMPORT | Jan-18 | 166,139.00 |
| 88 | SGA SECURITY | Jan-18 | 13,144,731.75 |
| 89 | SHANGDOM INVESTMENT CO. LTD | Jan-18 | 50,522,690.80 |
| 90 | TANZANIA CHINA FRIENSHIP TEXTILE | Jan-18 | 152,490,787.00 |
| 91 | TOYOTA TANZANIA LIMITED | Jan-18 | 31,708,848.00 |
| | | | |
| | | | **5,369,668,316.61** |

| SN | CLAIMANT'S NAME | DATE CLAIM RECEIVED | AMOUNT OF CLAIM |
|---|---|---|---|
| 1 | ACER PETROLEUM (T) LTD | Nov-19 | 7,298,813.00 |
| 2 | DAR ES SALAAM GLASS WORKS LTD | Nov-19 | 1,512,960.00 |
| 3 | GIBONCE AKIMU KAJIGILI | Nov-19 | 7,713,929.65 |
| 4 | BOSS SHOPPING CENTRE LTD | Nov-19 | 42,985,234.62 |
| 5 | LAKE CEMENT LTD | Nov-19 | 2,515,413.00 |
| 6 | LIJE JOVI INVESTMENT CO. | Nov-19 | 3,551,860.00 |
| 7 | MOTAENGIL AFRICA | Nov-19 | 1,185,368.00 |
| 8 | MWAGY INVESTMENT COMPANY LTD | Nov-19 | 444,988.25 |
| 9 | NYANZA BOTTLING CO. LTD | Nov-19 | 8,394,396.45 |
| 10 | PZM ASSOCIATES/MULTCHOICE | Nov-19 | 8,491,824.00 |
| 11 | SPRINT CARGO LIMITED | Nov-19 | 1,438,382.00 |
| 12 | SHINE BLUE PETROLEUM LTD | Oct-19 | 17,394,000.00 |
| 13 | TASAC | Oct-19 | 12,776,297.07 |
| 14 | VIN MART LTD | Oct-19 | 4,950,000.00 |
| 15 | WUZHOU INVESTMENT CO. LTD | Oct-19 | 4,249,086.00 |
| 16 | ARYSTA | Sep-19 | 3,026,170.00 |
| 17 | JAFRICA COMPANY LIMITED | Sep-19 | 4,584,026.00 |
| 18 | TANGA MODERN C & F CO. LTD | Sep-19 | 9,271,727.00 |
| 19 | TRISTARS INVESTMENS CO. LTD | Sep-19 | 1,795,896.00 |
| 20 | 21ST CENTURY | Aug-19 | 22,218,017.00 |
| 21 | 21ST CENTURY | Aug-19 | 10,245,659.02 |
| 22 | A ONE PRODUCTS & BOTTLERS LTD | Aug-19 | 1,068,720.00 |
| 23 | A ONE PRODUCTS & BOTTLERS LTD | Aug-19 | 3,919,497.00 |
| 24 | ACER PETROLEUM (T) LTD | Aug-19 | 20,333,869.00 |
| 25 | ALISTAR | Aug-19 | 30,000,000.00 |
| 26 | CHINA HENAN INTERNATIONAL COOP (CHICO) | Aug-19 | 1,490,608.00 |
| 27 | E. A. STEEL WOOL INDUSTRIES LIMITED | Aug-19 | 38,574,833.00 |
| 28 | HAROLD F. MAMKWE | Aug-19 | 94,800,000.00 |
| 29 | KENNETH ENOCK | Aug-19 | 3,947,856.00 |
| 30 | NEMART'S LTD | Aug-19 | 5,521,104.00 |
| 31 | TANGA CAR DEALS LIMITED | Aug-19 | 659,676.00 |
| 32 | TEDDY JUNIOR LIMITED | Aug-19 | 5,918,921.00 |
| 33 | URHOME COMPANY LTD | Aug-19 | 8,041,105.00 |
| 34 | KEKO PHARMACEUTICAL INDUSTRIES | Jun-19 | 10,679,957.00 |
| 35 | KIMAMBI J. KIMAMBI | Jun-19 | 10,794,941.00 |
| 36 | LAST CHOICE C & F | Jun-19 | 5,796,227.00 |
| 37 | MITCHEL GROUP INC | Jun-19 | 9,413,925.84 |
| 38 | SOL CALIBRATION SYSTEM | Jun-19 | 909,184.50 |

# TANGAZO

| | | | |
|---|---|---|---|
| 39 | SOL CALIBRATION SYSTEM | Jun-19 | 899,878.00 |
| 40 | BOLLORE LOGISTICS | May-19 | 8,515,304.00 |
| 41 | BOLLORE LOGISTICS | May-19 | 966,168.00 |
| 42 | GETCA INTERNATIONAL LTD | May-19 | 27,000,000.00 |
| 43 | HONOMU FREIGHTERS LTD. | May-19 | 9,168,356.00 |
| 44 | KUEHNE + NAGEL | May-19 | 1,322,403.00 |
| 45 | LAST CHOICE C&F | May-19 | 4,706,126.98 |
| 46 | MTIRO C & F | May-19 | 3,034,886.00 |
| 47 | TANELEC LIMITED | May-19 | 38,106,413.96 |
| 48 | BOLLORE | Apr-19 | 3,613,825.00 |
| 49 | MINING AND INDUSTRIAL SOLUTIONS | Apr-19 | 535,729.00 |
| 50 | MPEPA TRADERS CO. LTD | Apr-19 | 917,940.00 |
| 51 | TD UNITED INVESTMENT LTD | Apr-19 | 4,184,996.00 |
| 52 | WELLS CARGO | Apr-19 | 1,058,272.00 |
| 53 | ACACIA BULYANHULU GOLD MINE | Mar-19 | 21,356,232.00 |
| 54 | ASSOCIATED SUPPLIES LTD | Mar-19 | 2,285,549.00 |
| 55 | BAM INTERNATIONAL | Mar-19 | 103,178,336.00 |
| 56 | BAM INTERNATIONAL | Mar-19 | 42,609,088.00 |
| 57 | BAM INTERNATIONAL | Mar-19 | 27,422,472.00 |
| 58 | CHINA RAILWAY CONSTRUCTION ENGINEERING CO. | Mar-19 | 14,788,051.00 |
| 59 | ECOAE RESOURCES SUPPLIES LTD | Mar-19 | 3,265,978.00 |
| 60 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 6,078,708.00 |
| 61 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 8,748,938.00 |
| 62 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 4,180,104.00 |
| 63 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 1,061,572.00 |
| 64 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 1,714,045.00 |
| 65 | ENGEN PETROLEUM (TANZANIA) LTD | Mar-19 | 2,727,075.00 |
| 66 | LONAGRO TANZANIA LTD | Mar-19 | 20,778,492.00 |
| 67 | OCENAIR FREIGHT LTD | Mar-19 | 1,980,000.00 |
| 68 | ORTEC SERVICES INDUSTRIE TANZANIA | Mar-19 | 120,775,165.00 |
| 69 | SERENGETI BREWERIES LTD | Mar-19 | 395,920.00 |
| 70 | STEPHEN TUMAINI LEONE MUSHI | Mar-19 | 1,947,093.00 |
| 71 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | Mar-19 | 10,176,881.00 |
| 72 | UKOD INTERNATIONAL CO. LTD | Mar-19 | 5,714,205.84 |
| 73 | YAPI YAPI MERKEZ | Mar-19 | 22,400,428.00 |
| 74 | AIRSEA C&F | Feb-19 | 990,000.00 |
| 75 | BARAKA LTD | Feb-19 | 1,370,000.00 |
| 76 | CUSNA INVESTMENT LTD | Feb-19 | 2,970,000.00 |
| 77 | KAS FREIGHT LTD. | Feb-19 | 756,671.94 |
| 78 | LILY EQUIPMENTS & CON SUPPLIES | Feb-19 | 1,245,899.00 |
| 79 | MASHAURI MASWE BAYAI | Feb-19 | 482,738.00 |
| 80 | STAR OIL | Feb-19 | 4,234,474.25 |
| 81 | STAR OIL | Feb-19 | 61,746,198.55 |
| 82 | TANGANYIKA BUS SERVICE CO. LTD. | Feb-19 | 748,653.00 |
| 83 | ACCESSAGRO CO. LTD | Jan-19 | 44,126,422.00 |
| 84 | ADVENT CONSTRUCTION LTD | Jan-19 | 6,985,015.00 |
| 85 | AKO GROUP LTD | Jan-19 | 5,554,132.00 |
| 86 | CHARLES JOEL LOSIRA | Jan-19 | 3,898,600.00 |
| 87 | DHL | Jan-19 | 9,178,281.00 |
| 88 | DHL | Jan-19 | 605,915.00 |
| 89 | DHL | Jan-19 | 857,831.00 |
| 90 | GEITA GOLD MINING LTD | Jan-19 | 21,960,808.65 |
| 91 | HYATT REGENCY | Jan-19 | 1,421,002.00 |
| 92 | NEXT STAR CLEARING AND FORWARDING | Jan-19 | 323,480.00 |
| 93 | NEXT STAR CLEARING AND FORWARDING | Jan-19 | 300,000.00 |
| 94 | RAINBOW BEVERAGE T LTD | Jan-19 | 4,690,493.00 |
| 95 | SHIVA SOLAR | Jan-19 | 51,118,678.84 |
| 96 | THE MEDICAL HOUSE LTD | Jan-19 | 22,916,394.00 |
| 97 | UBA | Jan-19 | 1,350,394.00 |
| | | | |
| | | | **1,205,361,183.41** |

| SN | CLAIMANT'S NAME | DATE CLAIM RECEIVED | AMOUNT OF CLAIM |
|---|---|---|---|
| 1 | 21ST CENTURY FOOD AND PACKAGING LTD | Dec-20 | 10,285,041.40 |
| 2 | BAJUTA INTERNATIONAL (T) LTD | Dec-20 | 2,353,315.00 |
| 3 | BARNABAS W. KAPANGE | Dec-20 | 1,833,837.00 |
| 4 | CANDYMAN LIMITED | Dec-20 | 19,564,776.00 |
| 5 | CANDYMAN LIMITED | Dec-20 | 11,521,394.00 |
| 6 | CYBER PLANET LIMITED | Dec-20 | 619,760.00 |
| 7 | MANSOOR DAYA CHEMICALS LIMITED | Dec-20 | 5,152,981.60 |
| 8 | MAWENI LIMESTONE LIMITED | Dec-20 | 17,572,744.00 |
| 9 | RASHID SAID SELEMANI | Dec-20 | 1,273,817.00 |
| 10 | SUNDA INTERNATIONAL | Dec-20 | 39,932,130.00 |
| 11 | TANZANIA ZAMBIA RAILWAY AUTHORITY | Dec-20 | 84,543,023.00 |
| 12 | YAPI MERKEZ | Dec-20 | 5,731,400.00 |
| 13 | YAPI MERKEZ | Dec-20 | 13,762,294.00 |
| 14 | YAPI MERKEZ | Dec-20 | 5,328,244.00 |
| 15 | YAPI MERKEZ | Dec-20 | 12,032,298.00 |
| 16 | YAPI MERKEZ | Dec-20 | 28,169,379.00 |
| 17 | 21ST CENTURY FOOD AND PACKAGING LTD | Nov-20 | 28,229,067.92 |
| 18 | MALAI FREIGHTER FORWARDERS LIMITED | Nov-20 | 4,880,000.00 |
| 19 | TULAIBI NOMANI MANG'UNA | Nov-20 | 300,000.00 |
| 20 | Z & A TRADING COMPANY LIMITED | Nov-20 | 8,616,272.00 |
| 21 | BNM COMPANY LIMITED | Nov-20 | 415,635.00 |
| 22 | BNM COMPANY LIMITED | Nov-20 | 969,827.00 |
| 23 | INSIGNIA | Nov-20 | 18,061,776.00 |
| 24 | MANSOOR DAYA CHEMICALS LIMITED | Nov-20 | 4,191,228.36 |
| 25 | MANSOOR DAYA CHEMICALS LIMITED | Nov-20 | 4,593,645.32 |
| 26 | MLAU A. MASHOMBO | Nov-20 | 42,098,555.00 |
| 27 | OLYMPIC PETROLEUM TANZANIA LIMITED | Nov-20 | 788,073,917.08 |
| 28 | ORION LUBRICANTS | Nov-20 | 1,502,096.00 |
| 29 | RAMADHANI BADY RAMADHANI | Nov-20 | 1,875,750.00 |
| 30 | SUNKIST BAKERY LIMITED | Nov-20 | 18,469,679.00 |
| 31 | TARGET INTERNATIONAL (T) LTD | Nov-20 | 11,760,110.00 |
| | | | |
| 32 | CRDB/PACHAMU INVESTMENT | Oct-20 | 3,150,000.00 |
| 33 | KEDA (TANZANIA)CERAMICS CO. LIMITED | Oct-20 | 29,859,743.77 |
| 34 | MAKYUS COMPANY/SAID OMARY TAMIMU | Oct-20 | 13,426,478.00 |
| 35 | MARINAIR FREIGHT | Oct-20 | 2,062,003.00 |
| 36 | METEPLAN INTERNATIONAL CO. LTD | Oct-20 | 2,887,190.00 |
| 37 | STRONGSPUR LIMITED | Oct-20 | 4,231,279.00 |
| 38 | STRONGSPUR LIMITED | Oct-20 | 9,819,049.00 |
| 39 | ALLMOL FREIGHT SERVICES LTD | Sep-20 | 7,759,685.00 |
| 40 | COHERENT INVESTMENT LIMITED | Sep-20 | 146,019,303.00 |
| 41 | GEOSA ENTERPRISES | Sep-20 | 16,930,786.00 |
| 42 | HIGHLAND ESTATES LIMITED | Sep-20 | 2,730,940.00 |
| 43 | KIOO LIMITED | Sep-20 | 7,705,434.39 |
| 44 | TAZAMA PIPELINES LTD | Sep-20 | 53,845,673.00 |
| 45 | AFROIL INVESTMENT LIMITED | Aug-20 | 167,135,516.00 |
| 46 | AM-PM LIMITED | Aug-20 | 461,854.00 |
| 47 | A-ONE PRODUCTS & BOTTLERS | Aug-20 | 135,302,592.00 |
| 48 | BATMAC COMPANY LIMITED | Aug-20 | 4,371,440.00 |
| 49 | ELIAWON AIWINIA KISHIMBO | Aug-20 | 7,986,000.00 |
| 50 | HX INTERNATIONAL (TANZANIA) LIMITED | Aug-20 | 8,808,901.00 |
| 51 | PATERSON FORWARDERS LIMITED | Aug-20 | 7,583,589.00 |
| 52 | SHINYANGA EMPORIUM (1978) LTD | Aug-20 | 1,687,548.00 |
| 53 | STAR OIL TANZANIA LTD | Aug-20 | 140,776,026.00 |
| 54 | TANGANYIKA KENNEL LTD | Aug-20 | 5,427,970.00 |
| 55 | TANZANIA BREWERIES LTD | Aug-20 | 86,290,898.00 |
| 56 | TANZANIA SHIPPING AGENCIES CORPORATION | Aug-20 | 5,924,902.34 |
| 57 | BOLLORE LOGISTICS/VODACOM (T) LTD | Jul-20 | 118,420,731.00 |
| 58 | DEL-EX-CARGO LIMITED | Jul-20 | 1,295,633.00 |
| 59 | JULIUS JAMES MASOLWA | Jul-20 | 103,320,001.00 |
| 60 | L & Y FREIGHT FORWARDERS | Jul-20 | 1,600,000.00 |
| 61 | NYAKATO STEEL MILLS LTD | Jul-20 | 29,333,636.00 |
| 62 | BOLLORE TRANSPORT & LOGISTICS (T) LTD | Jun-20 | 659,583.00 |
| 63 | DOMUS INTERNATIONAL LTD | Jun-20 | 1,919,374.49 |
| 64 | KUEHNE+NAGEL | Jun-20 | 1,656,238.00 |
| 65 | KUEHNE+NAGEL | Jun-20 | 368,927.00 |
| 66 | KUEHNE+NAGEL | Jun-20 | 368,927.00 |
| 67 | KUEHNE+NAGEL | Jun-20 | 368,927.00 |
| 68 | MSD | Jun-20 | 84,007,469.00 |
| 69 | PETER K. MARO | Jun-20 | 295,000.00 |
| 70 | CAPITAL DRILLING | May-20 | 3,070,765.00 |
| 71 | KANSAI PLASCON TANZANIA LTD | May-20 | 3,555,495.00 |
| 72 | MOIVO INTERNATIONAL LOGISTICS | May-20 | 626,035.00 |
| 73 | NORTH MARA | May-20 | 179,593,876.00 |
| 74 | PETER K. MARO | May-20 | 295,000.00 |
| 75 | RATEGO FREIGHT FORWARDERS | May-20 | 7,372,737.00 |
| 76 | TRIPPLE R | May-20 | 345,140.00 |
| 77 | VALENTINA BALTAZAR | May-20 | 852,000.00 |
| 78 | MOHAMED ENTERPRISES TANZANIA LIMITED | Apr-20 | 30,664,329.00 |
| 79 | MWANZA AUTOMOBILE & HARDWARE LTD | Apr-20 | 10,500,846.00 |
| 80 | NYANZA BOTTLING CO. LTD | Apr-20 | 57,344,172.00 |
| 81 | SIMBA TRAILERS MANUFACTURING LIMITED | Apr-20 | 9,844,629.00 |
| 82 | SOAP AND ALLIED | Apr-20 | 1,632,147.00 |
| 83 | SUNDA TANZANIA INVESTMENT | Apr-20 | 5,057,283.00 |
| 84 | TOTAL | Apr-20 | 188,381,715.00 |
| 85 | TOTAL | Apr-20 | 81,431,328.00 |
| 86 | FAST FORWARD INTERNATIONAL (T) LTD | Mar-20 | 990,000.00 |
| 87 | GATEWAY LOGISTIC SERVICES | Mar-20 | 413,000.00 |
| 88 | LIBERTY INTERNATIONAL LIMITED | Mar-20 | 4,053,728.00 |
| 89 | LIJEJOVI INVESTMENT COMPANY LTD | Mar-20 | 3,079,000.00 |
| 90 | LONAGRO TANZANIA | Mar-20 | 1,837,714.00 |
| 91 | MARINAIR FREIGHT | Mar-20 | 1,632,147.00 |
| 92 | MOBISOL | Mar-20 | 32,241,751.00 |
| 93 | SALAMA PHARMACEUTICALS LIMITED | Mar-20 | 4,273,733.00 |
| 94 | TANELEC LIMITED | Mar-20 | 23,905,832.00 |
| 95 | TANZANIA PORTLAND CEMENT CO. LTD/TWIGA | Mar-20 | 2,554,086.00 |
| 96 | UNICEF | Mar-20 | 6,277,000.00 |
| 97 | LONG-WIDE TRADERS | Feb-20 | 37,014,497.00 |
| 98 | SPRINT CARGO LTD | Feb-20 | 13,104,637.00 |
| 99 | TANGA MODERN C&F CO. LTD | Feb-20 | 22,968,703.00 |
| 100 | TRIPPLE R LOGISTICS | Jan-20 | 1,924,365.00 |
| | | | |
| | | | **3,146,350,929.67** |

**Imetolewa na:**

**IDARA YA FORODHA NA USHURU WA BIDHAA**



## HABARI KANDA KASKAZINI

# RC Mongella aongoza mamia kupanda miti miaka 2 ya Samia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amewaongoza mamia ya wakazi wa Jiji la Arusha, kupanda miti ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani.

Akizungumza jana na wakazi hao, Mongella alisema serikali katika kipindi cha miaka miwili, imefanya mambo mengi makubwa ikiwapo ujenzi wa madarasa kwa kila wilaya, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati, hospitali za wilaya na kutoa vifaa tiba kwa sekta ya afya.

Aidha, alisema Rais Samia amezidi kuifungua Tanzania katika kukuza sekta ya utalii, akieleza kwamba filamu yake ya The Royal Tour, aliyoicheza imechangia kuleta watalii wengi nchini, ambao wanachochea ukuaji wa pato la taifa.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili, taifa limepiga hatua katika ukuaji wa demokrasia, kwa kuwa ameweza kuviunganisha vyama mbalimbali vya siasa na kuruhusu mikutano ya hadhara na kushiriki makongamano ya vyama hivyo.

Kadhalika, alisema kwa Mkoa wa Arusha katika kipindi cha miaka miwili, Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), imekusanya maduhuli ya zaidi ya Sh. bilioni 533, sawa na asilimia 107.13 ya lengo la makusanyo waliopangiwa.

"Hii ilitokana na mazingira mazuri ya kibiashara yaliyowekwa na serikali hasa katika uongozi wa Rais Samia," alisema.

Pia alisema halmashauri za Mkoa wa Arusha, zimefanikiwa kuchangia miradi ya maendeleo zaidi ya Sh. bilioni 50, sawa na asilimia 86.9 ya makusanyo.

Mongella alisema halmashauri hizo zimefanikiwa kutoa mikopo ya asilimia 10 kutokana na mapato ya ndani kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu zaidi ya Sh. bilioni sita.

**Kadhalika, alisema kwa Mkoa wa Arusha katika kipindi cha miaka miwili, Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA), imekusanya maduhuli ya zaidi ya Sh. bilioni 533, sawa na asilimia 107.13 ya lengo la makusanyo waliopangiwa**

# Bandari ya Tanga yapokea meli iliyobeba mzigo wa tani 50

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MELI kubwa ya mizigo kutoka Marekani imewasili katika Bandari ya Tanga ikiwa na shehena ya tani 50 za malighafi ya uzalishaji bidhaa za viwandani.

Meli hiyo ya M/V Metsovo, yenye urefu wa mita 189.99 ilitia nanga bandarini humo wiki iliyopita, baada ya kufanyika upanuzi mkubwa wa Bandari ya Tanga uliogharimu Sh. bilioni 429.1.

Akizungumzia matokeo hayo jana, Mkuu wa Idara ya Masoko ya Bandari ya Tanga, Rose Tandiko, alisema bandari hiyo inaendelea kuandika historia inayotokana na matunda ya uwekezaji uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan wa kuifungua nchi.

Alisema kutokana na uwekezaji huo, bandari hiyo imeendelea kupokea meli kubwa ambazo zimeendelea kuvunja rekodi kwa kutia nanga moja kwa moja gatini.

Hata hivyo, baadhi ya wamiliki wa kampuni zinazonufaika na uwekezaji huo ikiwamo kampuni ya usafirishaji wa mizigo ya Mr & Sons Limited, wamempongeza Rais Samia kwa maboresho hayo.

Kampuni hiyo ya usafirishaji ya Mr& Sons Limited, ni miongoni mwa kampuni zilizojikita kuhakikisha zitumia maboresho hayo katika Bandari ya Tanga, kutanua wigo wake kibiashara na kiuchumi. Meneja wa kampuni hiyo, Seph Issa, alisema meli hiyo ilikuwa imebeba shehena ya tani 50,000 za peticoc, ambayo ni mali ya Kiwanda cha Neelkant cha Amboni.

Awali, Mkurugenzi wa Kampuni ya Mr & Sons Limited, Mohamed Remtullah, alimpongeza Rais Samia kwa kuwajali Watanzania.




Meneja Mauzo wa Kampuni ya bia ya Serengeti (SBL) Kanda ya Kaskazini, Abel Mushi (kulia), akikabidhi zawadi ya televisheni kwa Frank Yohana (kushoto), baada ya kuibuka mmoja kati ya washindi wa promosheni ya bia ya Pilsner ijulikanayo kama Kapu la Wana jijini Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# WWF yazindua mradi wa kuelimisha kuishi na wanyama

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

MFUKO wa Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori Duniani (WWF), umezindua mradi mpya wa kuelimisha jamii zinazoishi kando kando ya shoroba za wanyamapori namna ya kuishi na wanyama wakali ili wasiwadhuru.

Wanyamapori hao ni wale wanaotembea kutafuta malisho kwenye mapito yao maarufu kama shoroba na kisha kufika kwenye makazi ya binadamu.

Mkurugenzi Mkazi wa mfuko huo nchini, Amani Ngusaru, alisema uamuzi wa kuja na mradi huo mkoani Arusha, unatokana na matokeo chanya ya kukua kwa ofisi waliyoifungua miaka miwili iliyopita.

"Tumezindua mradi huu ili kuwasaidia zaidi wananchi wapate elimu ya namna gani wanaweza kujikinga na hawa wanyama wanaopita kwenye shoroba na kutokea katika makazi ya watu.


"Lakini tuliangalia mazingira, ikiwamo maji yanavyopatikana katika vyanzo mbalimbali na kuona namna ya kusaidia uchimbaji wa mabwawa panapouhitaji na vilevile, kutoa elimu namna gani ya kutunza hayo maji ili yaweze kuwasaidia," alisema.

Aidha, alisema mradi huo wa miaka mitatu uliopewa jina la BMZ, unatekelezwa kwa Sh. bilioni saba.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, mfuko huo unatarajia kuzindua miradi mingine nchini, baada ya Rais Samia Suluhu Hassan, kufungua sekta ya utalii kwa njia mbalimbali ikiwamo Filamu ya The Royal Tour.

"Baada ya Rais (Samia) kuifungua nchi hasa katika sekta ya utalii, hata sisi tunatarajia kufungua miradi mingi hapa nchini katika mikoa mbalimbali,"alisema Ngusaru.

Mradi huo wa BMZ ulioanza kuzinduliwa mkoani Arusha, utazinduliwa pia wakati wowote katika Wilaya ya Rombo na Mwanga mkoani Kilimanjaro.





# Waomba sheria kudhibiti vyanzo vya maji iwekewe mkazo

**Na Restuta Damian,**
KYERWA

WANANCHI wa Kijiji cha Katunguru Kata ya Katunguru wilayani Kyerwa mkoani Kagera wameiomba serikali kuweka mkazo kwenye sheria ya katazo la shughuli za kibinadamu ndani ya mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji ili kuzuia uharibifu.

Walitoa ombi hilo wakati wa maadhimisho ya wiki ya maji wilayani Kyerwa, wakisema shughuli za kibinadamu zinazofanyika karibu na vyanzo vya maji zimekuwa zikiathiri vyanzo hivyo na kusababisha ukosefu wa huduma na kuiingizia hasara serikali.

Mmoja wa wakazi hao kutoka Kata ya Katunguru, Jovin Barthazari, alisema shughuli za kilimo na ufugaji kwenye maeneo ya karibu na vyanzo vya maji hususani zinazofanyika ndani ya mita 60 zimekuwa zikiharibu vyanzo hivyo na kusababisha ukosefu wa maji.

“Katika chanzo cha Kilela wafugaji wanaingiza mifugo yao pamoja na shughuli za kilimo bila kujali wao ndiyo wanufaika wa maji hayo, shughuli hizo zinaharibu miundombinu ya mabomba ya maji,”alisema.

Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani Kyerwa, Mhandisi Shukrani Tungaraza, alisema huduma ya maji imefikia vijiji 44 kati ya 99 vilivyoko wilayani hapo ikiwa vijiji 18 vyenye visima virefu na vifupi 37 havifikiwi.

Aidha alisema kwa mwaka wa fedha 2022/2023 RUWASA imepanga kufikia kata na vijiji ambavyo havina maji ili kufikisha huduma hiyo kwa wananchi wote.

Alisema katika chanzo cha maji Kilela kilichoko katika Kata ya Katunguru kinahudumia wananchi 22,000 kwenye Kata ya Katunguru, Isimgiri na Kaisho, hivyo kuwataka wananchi kutunza vyanzo hivyo ili kuepusha upotevu wa maji na rasilimali fedha zitumikazo kurekebisha miundombinu hiyo.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kyerwa, Benjamin Mwikasyege, alisema kuwa sheria iliyowekwa ya mita 60 imetolewa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa wananchi kutofanya shughuli za kibinadamu ndani ya vyanzo vya maji, hivyo ni lazima ifuatwe na kutiliwa mkazo.

## Wajawazito wasisitizwa kumeza vidonge vya vitamini B9

**Na Neema Emmanuel,**
NYAMAGANA

WAJAWAZITO wametakiwa kutilia mkazo matumizi ya vidonge vya vitamini B9 ‘folic acid’ ili kudhibiti tatizo la kuzaliwa kwa watoto wenye mgongo wazi na vichwa vikubwa.

Wito huo ulitolewa juzi na Meneja Msimamizi wa Kituo cha Nyumba ya Matumaini, Getruda Butondo, akisema tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi kwa watoto husababishwa na ukosefu wa madini ya folic acid ambayo mjamzito anapatiwa wakati akiwa kliniki.

Kadhalika, alisema wanawake wengi wanachelewa kwenda kliniki na kukosa lishe bora wakiwa wajawazito na hawazingatii matumizi ya vidonge hivyo hali inayosababisha tatizo hilo kuendelea kuwa kubwa nchini.

Alisema katika kituo hicho wamekuwa wakipokea wazazi wenye watoto hao kutoka mikoa tofauti ikiwa ni pamoja na Geita, Tabora, Mwanza, Kagera na Simiyu.

“Tunawashukuru waandishi wa habari wanawake kwa msaada huu, kituo hiki kinapokea wazazi ambao hawana uwezo wa kuwahudumia watoto hao sambamba na wale wasiokuwa na maeneo ya kukaa wakati wakisubiri huduma za upasuaji unaofanyika katika Hospitali ya Rufani Kanda ya Bugando,” alisema.

Akizungumza baada ya kukabidhi misaada iliyotolewa na waandishi wa habari wanawake, Katibu wa Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Mwanza (MPC), Blandina Aristides, alisema kufuatia uhitaji uliopo katika kituo hicho ni jukumu la kila taasisi kutoa walichonacho ili kuwasaidia kuendelea kuhudumiwa.

“Mahitaji tuliotoa ni mchele kilo 100, sukari kilo 50, sabuni za vipande boksi 10, mafuta ya kupikia dumu lita 40, juisi katoni 15 pamoja na mafuta kwa ajili ya kupaka mwilini katoni 2 vyenye thamani ya Sh. 800,000,”alisema Aristides.

Mmoja wa wazazi wenye mtoto mwenye kichwa kikubwa na mgongo wazi kutoka Mpanda mkoani Katavi, Tausi Shija, alisema kuwa moja ya sababu ya kupata mtoto mwenye tatizo la kichwa kikubwa na mgongo wazi ni kutokana na kuchelewa kuhudhuria kliniki, kwamba alianza kwenda kliniki mimba ikiwa na miezi mitano.

Alisema: “Elimu inatakiwa kuanza kutolewa kwa mabinti ambao tayari wamefikia umri wa kubeba ujauzito ili kuwasaidia kipindi wawapo na ujauzito waache kupuuzia dawa hizi.”



Lori likimwaga mchanga kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Mtiro mkoani Mara hivi karibuni, baada ya harambee ya uchangiaji wa ujenzi huo, ilioendeshwa na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watoto 60 wenye utapiamlo hupokelewa Hospitali ya Sekou Toure kila mwaka

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

WASTANI wa watoto 60 wenye umri chini ya miaka mitano kila mwaka hufikishwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa Sekou Toure wakiwa na tatizo la utapiamlo.

Kadhalika, kwa mwezi hupokea wastani wa watoto sita hadi 10 wenye tatizo hilo.

Takwimu hizo zilitolewa na Dk. Adventina Gwassa kutoka katika hospitali hiyo, anayeshughulikia utoaji huduma za utapiamlo, wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake.

Alisema hospitali hiyo inaendelea kutoa huduma hiyo wakati wote, hivyo kuwataka wazazi kuwafikisha watoto ili wapatiwe huduma kuepusha tatizo hilo kuwa kubwa.

Dk. Gwassa alisema kuwa tatizo hilo linaendelea kuwa kubwa mkoani humo kutokana na idadi kubwa ya watoto kuwa na lishe duni na kuitaka jamii kuwakazania watoto kula vyakula vyenye lishe kwa kufuata maelekezo ya kliniki za watoto.

Alisema hatua zinazochukuliwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wajawazito wanaokwenda kliniki, zahanati na vituo vya afya, kabla na baada ya kujifungua.

Mganaga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Bahati Msaki, alitaja dalili za utapiamlo kuwa ni pamoja na ngozi ya mwili kuwa kavu, mwili kuchoka, mgonjwa kukosa furaha wakati wote na nywele kubadilika rangi kuwa nyepesi.

Dalili zingine ni mwili kujaa maji, kukonda sana, kupungukiwa damu, tumbo kuuma kila mara, kupata homa, nimonia, kutoongezeka uzito, kinga ya mwili kuwa chini, kudumaa kukua, hali hiyo huwapata zaidi watoto wasiopata chakula cha protini, upungufu wa madini na vitamini inayotakiwa.

Dk. Bahati alisema ugonjwa wa utapiamlo pacha wake ni kwashakoo kutokana na dalili zake kufanana, ambao husababishwa na upungufu wa protini mwilini itokanayo na vyakula kama vile nyama, samaki, maharage, mayai pamoja na maziwa.



Ukurasa 12

**Anayoyafanya Rais yanaonekana mchana, hata gizani kwa ukamilifu**




Ukurasa 14

Japo ametangulia ameacha zawadi nono

siasa
JUMATANO MACHI 22, 2023
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe



Ukurasa 13

**Utata uliojivika katika siasa ya uchumi kati ya Russia na Ulaya**

# Kambaya anapochomoka akitimkia rasmi CHADEMA

## • Awatabiria kifo 'watesi' wake CUF, Msajili, CUF wamjibu aambiwa 'shiii'

**Na Sabato Kasika**

"NI maamuzi magumu, ila imebidi iwe hivyo, kwani muda muafaka ndiyo umewadia, sijali wangapi watalia, lakini ni lazima maisha ya siasa yaendelee hata kupitia vyama vingine, si lazima kufanyia ndani ya CUF tu".

Hivyo ndivyo mwanasiasa machachari Abdul Kambaya, ambaye amewahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi, katika Chama cha Wananchi (CUF), kabla ya yeye na wenzake kutimuliwa mwanzoni mwa mwaka 2021.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam, Kambaya ambaye sasa amejiunga na CHADEMA, anasema ameachana na kesi aliyofikisha katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, akipinga kuvuliwa uanachama wa CUF na sasa anasonga mbele.

"Kesi inakaa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa zaidi ya mwaka mmoja bila kutolewa uamuzi, nimeona isiwe shida , niachane nayo na nijiunge na chama kingine niendelee na harakati zangu za kisiasa," anasema Kambaya.

Mwanasiasa huyo aliyejiunga na CHADEMA hivi karibuni Machi 11, anasema wapenda haki wenzake waliokuwa wanachama wa CUF 400 mkoani Dar es Salaam wameungana naye katika uamuzi huo.

Anadai wanachama hao wamemfuata CHADEMA licha ya kwamba , haijathibitika rasmi uwapo wa takwimu hizo kutoka uongozi wa chama hicho.

"Muafaka ndiyo umewadia, sijali wangapi watalia, lakini ni lazima maisha ya siasa yaendelee kupitia huku niliko sasa, lakini ofisi ya Msajili ijue kumkumbatia Mwenyekiti wa CUF Profesa Ibrahimu Lipumba, si kukisaidia ni kukiua," anasema.

Katika ufafanuzi wake anasema, ruhusa ya mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa imeonyesha jinsi ambavyo wanachama wa CUF wasiopenda dhuluma wamekimbia na kujiunga na vyama vingine.



Abdul Kambaya (mwenye shati jekundu) na Mweyekiti wa CHADEMA Freeman Mbowe, baada ya kumpokea kuwa mwanachama. **PICHA: CHADEMA**

"Hivi karibuni tulishuhudia wanachama wa CUF mkoani Dar es Salaam wakijiunga na vyama vingine. Hizo ni salamu kwa Msajili kuwa, kumkumbatia Mwenyekiti Lipumba siyo kusaidia, bali kuondoa CUF kwenye ramani ya siasa na dunia," anasema.

**HAKIFI KITU**

Wakati Kambaya akikitabiria chama hicho kifo, Naibu Katibu Mkuu wa CUF, Bara, Magdalena Sakaya, anasema chama hakitakufa, kwa kuwa kimejengwa katika misingi imara isiyoyumba.

"Kwanza Kambaya si mwanachama wa CUF, hivyo si sahihi kuzungumzia sana, aiache CUF tena asitegemee kwamba chama kitakufa, imejengwa kwenye ngome madhubuti. Hata mimi nikiondoka siwezi kusababisha ikafa," anasema Magdalena bila kueleza uimara wa ngome ya chama chao ni nini.

Aidha, anasema wapo wanachama wengi ambao wamekuwa viongozi wa serikali ambao walikikimbia na kukiacha kikiwa imara, huku akimtaka Kambaya aendelee na siasa huko aliko, si kuzungumzia CUF.

Naibu Katibu Mkuu huyo anasema kauli ya Kambaya haiwezi kuyumbisaha wanachama wa CUF kwa mambo yasiyokuwa na msingi na kwamba badala yake wataendelea kuungana katika kukiimarisha chama hicho.

"Chama hiki kiko imara na kitaendelea kuimarika kutokana na uwezo wa viongozi wake ambao wamepata sifa kutokana na umahiri wao wa masuala ya uchumi na siasa," anaeleza.

Anasema chama hicho siku zote kimekuwa mstari wa mbele, katika kusimamia misingi ya haki na usawa kwa wote na kwamba kitaendelea kufanya hivyo kwa wanachama wake na wapenzi wa CUF.

**KIGUGUMIZI MSAJILI**

Hata hivyo, Msajili wa Vyama vya Siasa Jaji Francis Mutungi, anapoulizwa kuhusu tuhuma zinazoelekezwa kwake, kuhusu kumkumbatia, Profesa Lipumba, anasema kwa kifupi kuwa 'no comments'.

"Huyo mtu wako si kashahamia CHADEMA? Mambo ya CUF awaachie wenyewe. Kakwambia kwamba Jaji kukumbatia migogoro siyo kumsaidia Lipumba, nasema no comment,"

Mwaka 2021, CUF ilitangaza kuwavua uanachama viongozi wake saba, wakiwamo 14 waliokuwa wakikabiliwa na tuhuma mbalimbali kama madai ya kula njama za kukihujumu chama hicho.

Baadhi yao walikuwa ni Mjumbe wa Baraza Kuu, Abdul Kambaya, mjumbe mwenzake Hamis Mohamed Faki, aliyekuwa mbunge wa Mchinga mkoani Lindi na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana wa chama hicho, Hamidu Bobali.

INAENDELEA UK. 12

USHUHUDA WADAU, WANASIASA

# Anayoyafanya Rais yanaonekana mchana, hata gizani kwa ukamilifu

• Kushirikiana na upinzani, shule nyingi ghorofa, kuimarika utulivu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

VIONGOZI na wadau wa kisiasa Zanzibar wanayaelezea mafanikio ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu, hasa kuwa yanaonekana gizani na kwenye mwanga, si jambo la kutafuta au kusaka kwa bidii.

"Maendeleo tunayoyashuhudia CCM hatuna wasiwasi na jambo lolote na muelekeo wetu ni sawa na kula ngisi au pweza gizani, tuna mambo mengi ya maendeleo ya kuzungumza kwa wananchi bila kificho,"anasema Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi na Habari wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis.

Anafafanua kuwa mafanikio hayo yanaonekana kwa wazi bila kizuizi, iwe mchana au usiku, kwa mgeni au mwenyeji, mtoto na kijana wanakitambua kinachoendelea visiwani humo.

Akizungumzia tathmini ya miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia, anasema amedhihirisha kasi ya kuleta maendeleo Bara na Visiwani na kuongeza:"Mungu ametupatia zawadi, Mama ameupiga mwingi na kila mwenye macho anashuhudia maendeleo yanayojitokeza."

Khamis anasema barabara za kuunganisha mikoa zinajengwa kwa kasi lakini pia nguvu zinaelekezwa ujenzi wa miundombinu ya vijijini, ili kuimarisha huduma za usafiri kunufaisha sekta zote kuanzia wakulima, wafugaji na wafanyabiashara.

Mradi unaoendelea wa ujenzi wa reli ya treni ya umeme utakapokamilika utafungua mlango wa kiuchumi ndani na nchi jirani kama Rwanda,DRC na Burundi kwa kuimarika sekta ya usafirishaji zaidi, anaongeza.

Aidha, anasema fedha za UVIKO-19 zimefanikisha miradi mingi ya maendeleo sekta ya afya, elimu na Zanzibar imekuwa mnufaika mkubwa kutokana na shule za kisasa za ghorofa zilizojengwa na hospitali za wilaya Unguja na Pemba.

Anaongeza kuwa chini ya Rais Samia, uhusiano wa kimataifa unaendelea kuimarika pamoja na serikali kurejesha uhuru wa vyombo vya habari uliokuwa unazorota hapo awali,

Akizungumzia maendeleo yaliyopatikana Zanzibar katika uongozi wa Rais Dk Hussein Ali Mwinyi, akishirikiana na Rais Samia, anasema miradi mingi ya afya, elimu, uvuvi pamoja na kuweka misingi ya utawala bora, kukomesha ubadhirifu na ufisadi wa mali za umma imefanikiwa.

Anasema licha ya kujitokeza mfumko wa bei, Zanzibar ina uhakika wa chakula na kwamba umeanza kupungua baada ya mvua kunyesha Bara na yapo matumaini ya bei kushuka baada ya wakulima kuanza kuvuna.

"Mfumuko wa bei Zanzibar ulisababishwa na ukame wa mwaka jana, mtikisiko wa uchumi duniani uliosababishwa na UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine," anasema Khamis.



Katibu wa Idara ya Itikadi, Uenezi Na Habari wa CCM Zanzibar, Khamis Mbeto Khamis. **PICHA : RAHMA SULEIMAN**

> Mfumuko wa bei Zanzibar ulisababishwa na ukame wa mwaka jana, mtikisiko wa uchumi duniani uliosababishwa na UVIKO-19 na vita vya Russia na Ukraine.

### FEDHA ZA UVIKO-19

Aidha, Khamis anazungumzia fedha za UVIKO -19 akisema SMZ imezitumia kumaliza upungufu wa maji baada ya kuipatia mamlaka ya maji (ZAWA) Shilingi bilioni 34.5 kujenga matangi ya kuhifadhi lita 1,000,000 kutandaza mabomba ya kusambaza maji na kuchimba visima 120 pamoja na kununua pampu 55 za huduma za dharura Unguja na Pemba.

Akizungumzia kuendeleza wajasiriamali, anasema wamejengewa masoko ya kisasa maeneo ya Mwanakwerekwe, Jumbi na Mbuzini ujenzi ambao unatarajiwa kukamilika mwakani.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu Dk.Aboud Suleiman Jumbe, akizungumzia mafanikio anasema miaka miwili ya Rais Samia uchumi wa buluu unapata mafungamano bora ya uhusiano wa kidiplomasia ili kufanikiwa.

Anawasifu Rais Samia na Dk. Mwinyi kuwa ni mabingwa wa diplomasia na kwamba Mwinyi ndiye mwasisi wa dhana ya uchumi wa buluu ambao ni miongoni mwa kazi za ilani ya CCM 2020-2025.

"Niseme miaka miwili ya Rais Samia madarakani diplomasia ya kimataifa ya uchumi wa buluu imefunguka na kuna mapinduzi makubwa ya sera za taifa na kimataifa zinazowezesha fursa mbalimbali kuibuka,"anasema Dk.Jumbe.

Aidha, anasema SMZ inatekeleza miradi ya uvuvi wa bahari kuu,nishati ya mafuta na gesi pamoja na ujenzi wa bandari za mizigo na ya kutengeneza vyombo vya baharini.

Jumbe aliyataja mashirika ya kimataifa pamoja na nchi zilizofunguwa milango ya kuisaidia Zanzibar katika sekta ya uchumi wa buluu ikiwemo Benki ya Dunia itakayotoa Dola milioni 120 kuendeleza mradi uliojikita katika kujenga miundombinu zikiwamo huduma mbalimbali za samaki, viwanda vya kusindika pamoja na kilimo cha mwani.

### UHUSIANO KIMATAIFA

Aidha, anasema Benki ya Uwekezaji ya Ulaya imetoa Yuro milioni 540 kwa ajili ya mikopo katika maeneo mbalimbali ya wajasiriamali zikiwa na lengo la kuwanyanyua na kuwajengea uwezo kufanya miradi yao.

Rais Samia ameonesha uwezo mkubwa katika kulitumikia taifa na kuimarisha uhusiano wa kimataifa, anasema Katibu Mkuu wa CUF Zanzibar, Hamad Masoud.

Anaeleza kuwa chini ya uongozi wake wananchi wameshuhudia miradi mikubwa katika sekta ya afya, elimu pamoja kupunguza gharama za pembejeo kwa wakulima jambo ambalo litaongeza uzalishaji na kubadili sekta ya kilimo.

Masoud anasema Rais Samia amefunguwa milango ya demokrasia na hivyo kujenga mazingira mazuri kwa wanasiasa kufanya shughuli zao za kisiasa kwa amani na utulivu.

"Ameanza vizuri miaka miwili ameifungua demokrasia iliyokuwa ikilalamikiwa na viongozi wa vyama vya siasa, anafahamu kuwa mikutano ya kisiasa ndiyo uhai wa vyama," anasema.

Mwenyekiti wa Baraza la Vyama vya Siasa, Juma Ali Khatib anaitaja miaka miwili ya Rais Samia kuwa imefungua zaidi demokrasia ya vyama vingi akilenga kusaidia serikali iliyopo madarakani kwa kuikumbusha mambo ya msingi kama ahadi zake kwa wapiga kura.

Khatib anamsifia Rais kwa kutumia zaidi busara na kuwa msikilizaji wa changamoto za wanasiasa, ameunda kamati ya wanasiasa iliyokuja na maazimio ya nini kifanyike katika uendeshaji wa siasa za kistaarabu nchini.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Chama Cha ACT-Wazalendo Salim Bimani, anasema Rais Samia katika kipindi hicho amekuwa karibu zaidi na wanasiasa kwa ajili ya kutafuta maridhiano ya kudumu yatakayoimarisha amani na utulivu wa taifa.

"ACT-Wazalendo tumeingia maridhiano na CCM ambapo tunashukuru amani na utulivu vimeimarika katika kipindi cha miaka miwili huku tukimshuhudia Rais Samia akifuatilia maridhiano hayo," anasema.

## Kambaya anapochomoka akitimkia rasmi CHADEMA

**INATOKA UK. 11**

Mbali na hao, wengine waliofukuzwa ni Hamida Abdallah Huweishi, mgombea mwenza wa Profesa Lipumba katika uchaguzi wa mwaka 2020.

Chande Naibu Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Vijana ya CUF (JUVICUF).

Katika kundi hilo, walikuwamo pia Ali Makame Issa, Mtumwa Ambari Abdallah , Mohamed Vuai Makame na Dhifaa Bakari ambao wote nao walikuwa ni wajumbe wa Baraza Kuu la CUF.

Kitendo hicho cha kufukuzwa kiliwafanya wabishe hodi katika ofisi za Msajili wa Vyama vya Siasa, jijini Dodoma Desemba 2021, ili kusaka haki yao, lakini Kambaya anadai kuwa hadi sasa ofisi hiyo imekuwa kimya.

Kwa uamuzi huo wa Kambaya, ni wazi sasa sintofahamu hiyo ya waliokuwa wanachama wa CUF inaweza kuwa imeshia hapo, baada ya kinara wao kubwaga manyanga na kujiunga na CHADEMA.

# Utata uliojivika katika siasa ya uchumi kati ya Russia na Ulaya

## • Mjadala; anayewajibika uhaba wa chakula duniani

Na Petrov Nikolai

HADI sasa Umoja wa Ulaya unaendelea na kampeni yake kusambaza habari, ikielekeza lawama Russia, katika zama iliyopo mwaka mmoja wa vita kati yake na Ukraine, kwamba inasababisha uhaba wa chakula na hasa kwa nchi maskini duniani.

Hilo linatokea sambamba na kupatikana ufafanuzi kwamba, inatoa mchango mkubwa katika kuvuka kikwazo cha uhaba wa chakula uliopo duniani.

Lakini ikivaliwa miwani, ukweli unaoashiria ni kwa EU inatumia tatizo la upatikanaji chakula duniani, kutimiza malengo binafsi ya kisiasa, pasipo kutathmini matokeo hasi yanayoweza kuathiri mataifa yanayoendelea, hasa barani Afrika.

Kuna mifano ya hivi karibuni kutoka kwenye mkutano wa Halmashauri ya Kilimo na Uvuvi ya Umoja wa Ulaya uliofanyika Januari 30 mwaka huu, nchi kama Austria, Ubelgiji, Croatia, Cyprus, Jamhuri ya Czech, Ugiriki, Hungary, Latvia, Malta, Poland, Romania na Slovenia, ziliwasilisha taarifa isiyo rasmi.

Ni taarifa iliyopewa jina "Kuhakikisha uthabiti na uwezo wa ushindani wa kimataifa wa Umoja wa Ulaya: haja ya msaada wa dharura na msimamo wa kimkakati wa kuendesha biashara ya kilimo".

Kimsingi, ni aina ya waraka unaoeleza sababu ya wakulima katika Umoja wa Ulaya kwa jumla, kushinikizwa kwa njia zisizo na mifano. Bila shaka sasa kuna tathmini kutoka Umoja wa Ulaya, inayotamka "matatizo ya leo yanasababishwa na uvamizi haramu wa nchi ya Russia."

### MZIZI WA MKASA

Sababu halisi zinazounda hali ya sasa zinapaswa kuanikwa na vigezo kadhaa vinavyobeba ukweli kama; mlipuko ugonjwa UVIKO-19; mfumuko wa bei mkubwa, kuongezeka bei za rasilimali za nishati, nikiamini hazihusiki kabisa au moja kwa moja na kinachoitwa "uvamizi haramu wa nchi ya Russia."

Pia, ni ngumu kusahaulika maendeleo makubwa yanayohusu kujengwa uchumi wa kijani na kidigitali, hali kadhalika ushindani wa kimataifa.

Ni sababu zilizoongeza thamani ya uzalishaji na kusambaza mazao ya kilimo. Kwa kifupi, hali ngumu ya sasa, ni matokeo ya mambo kadhaa ikiwamo siasa ya Umoja wa Ulaya wenyewe.

Inapozungumziwa uhaba wa nishati, jamii inapaswa kutilia maanani hali ya uhaba wa nishati ulioanzia Marekani kuagiza Umoja wa Ulaya usitishe matumizi ya nishati kutoka Russia na badala yake, ununue gesi bei ya juu zaidi Marekani.

Uhalisia unaotawala, umoja huo una mikabala miwili tofauti ya kutatua matatizo ya kilimo nchini kwao na katika nchi nyinginezo.

Kwa upande mmoja, EU inatamani kuchambua sababu halisi za matatizo hayo, ili kupata uamuzi sahihi. Lakini, kwa upande mwingine zinaangukia kujengwa sura ya kushitakiwa Russia kulingana na hali inayoendelea katika siasa yake na Ukraine.



Shamba la ngano nchini Russia.



Kansela Mkuu mstaafu wa Ujerumani Angela Merkel (kushoto,) akiwa na Rais wa Russia Vladimir Putin, walipokutana mwaka 2017. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

> Licha ya miito mingi ikiwamo kutoka EU na jumuiya nyingine za dunia, umoja huo haukufanya chochote kuboresha hali ya leo, huku ukiendelea kutangaza vikwazo vingi dhidi ya Russia.

Pia, ni wakati EU inaendelea kulazimisha nchi nyingine duniani zifuate siasa yao, ambayo imeshaleta matokeo ya kutia shaka kwa uimara wa sekta kilimo duniani. Bei kubwa za mbolea na vyakula au tatizo la kugawa chakula, mara zote si kitu kingine, yasipokuwa matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo haramu dhidi ya nchi ya Russia vinavyozuia usafirishaji mbolea na kudhoofisha masoko ya nishati.

Licha ya miito mingi ikiwamo kutoka EU na jumuiya nyingine za dunia, umoja huo haukufanya chochote kuboresha hali ya leo, huku ukiendelea kutangaza vikwazo vingi dhidi ya Russia.

### MIKAKATI TATA

Wenyeji wa Ulaya wanapendelea kuzungumzia fidia za pesa kwa wakulima wao na njia za kuhakikisha uwezo wa ushindani wa EU kwenye masoko ya kimataifa.

Jambo la kuvutia ni kwamba, nchi zilizoshiriki katika mkutano wa Halmashauri ya EU ya Kilimo na Uvuvi ya Januari 30, mwaka huu zimeendana na mawazo ya Rais Vladimir Putin.

Hapo inaunda ujumbe kwamba kukosekana chakula ni matokeo ya moja kwa moja ya vikwazo dhidi ya Russia na siasa zinazoendeshwa na nchi tajiri zaidi duniani, kununua chakula kwa fedha taslimu, pia kwenye siasa ya vizuizi nishati.

Ni hali inayojionyesha kwenye waraka unaoitwa: "Matatizo yanayohusika na ongezeko la uingizaji wa bidhaa za kilimo kutoka nchi ya Ukraine".

Ni waraka uliowasilishwa na ujumbe wa Poland kwa niaba ya nchi kama Bulgaria, Jamhuri ya Czech, Hungary, Poland, Romania, Slovakia kwenye mkutano huo huo wa Halmashauri ya Umoja wa Ulaya ya Kilimo na Uvuvi uliofanyika mnamo Januari 30 mwaka huu.

Waraka huo unaendana na pendekezo liitwalo "solidarity lanes initiative" lililolenga kuwezesha usafirishaji bidhaa za kilimo hasa mazao ya nafaka kutoka nchi jirani za Umoja wa Ulaya, kwenda nchi nyingine zinazokabiliwa na ukosefu wa chakula.

Iko wazi kwamba, waraka unafichua hatua zilizochukuliwa mwezi Juni mwaka jana, kuwezesha uingizaji bidhaa kutoka Ukraine kwenda Ulaya, ikiwamo kuondolewa kwa mwaka mmoja ushuru wa forodha wa bidhaa zinazotoka Ukraine, ili kuchangia kuongezeka chakula.

Kinachopelekwa kutoka Ukraine kwenda Ulaya, kinajumuisha mazao ya nafaka, sukari, nyama ya ndege wa kufugwa, unga na vyakula kadhaa vinavyotengenezwa kwa maziwa, asali, juisi ya tufaha, mbegu za alizeti na mizabibu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyosambazwa katika nchi wanachama wa EU, uingizaji ngano kutoka Ukraine uliongezeka maradufu kati ya mwaka 2021 na sasa hali inaonekana ngumu, hata nchi za Ulaya zilizotajwa mapema.

Leo likofika, zinatoa madai ya kutia saini waraka maalum, bidhaa za kilimo zitokazo Ukraine kupitia EU kufikia masoko yanayolengwa, kupita masoko ya nje ya umoja huo, jambo linalotajwa linaweza kuleta vurugu katika masoko hayo na ndani ya Ulaya.

Maudhui ya nyaraka hizo, yanatambulisha kwamba: Kwanza, kinyume cha matangazo bora kuhusu upatikanaji chakula katika nchi maskini nchi za Ulaya zinanunua kwa kasi bidhaa za kilimo kutoka nchi ya Ukraine, ili kujihifadhi na kuhakikisha ustawi wao.

Pili, inaelezwa kwamba nchi za Umoja wa Ulaya zikisafirisha vyakula katika nchi maskini zenye mahitaji makubwa na zinazitumia nchi maskini kama mahali daraja na kujinufaisha kwenye sekta ya kilimo.

Kwa mujibu wa gazeti moja la Austria (jina tunalo) ni kwamba nafaka kutoka Ukraine ilisafirishwa katika nchi za Uhispania, yanayotumika kuwa malisho kwa nguruwe.

Sababu ya kufanyika hivyo, ni majibu kwamba Uhispania, ilipatia Ukraine pendekezo la kibiashara bora, hivyo ikaijibu kwa kuipatia nafaka kwenda Hispania.

**• Makala hii ni maoni ya uchambuzi binafsi wa mwandishi, ambaye pia ni Mkurugenzi wa Masuala ya Uhusiano na Afrika, katika Kituo cha Utamaduni cha Russia.**

MIAKA MIWILI BILA JPM

# Japo ametangulia ameacha zawadi nono

• Ni maajabu daraja la Wami, wingi wa tembo, Tuzo ya Afrika

**Na Gaudensia Mngumi**




Ndilo daraja jipya la Wami linaloharakisha usafiri wa Dar na mikoa ya kaskazini. **PICHA: MTANDAO**

MACHI 17 ndiyo kumbukumbu ya miaka miwili ya mwanamapinduzi na mtetezi wa Tanzania yenye maendeleo endelevu, viwanda, uchumi wa kati na inayojitegemea isiyohusishwa na umaskini , Dk. John Magufuli.

Ibada inafanyika nyumbani kwake Chato mkoani Geita kwa maombi na sala. Magufuli mhandisi na daktari msomi mbobezi wa kemia, Naibu na Waziri wa Ujenzi kwa miaka mingi, kadhalika Waziri Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na Mifugo na Uvuvi na kubwa zaidi Rais wa Tanzania kuanzia 2015 hadi 2021, alitwaliwa akiwa katika awamu ya pili ya uongozi wake.

Ijumaa iliyopita, Watanzania, serikali, wana CCM, marafiki zake, wadau mbalimbali wanatoa heshima zao kwa shujaa aliyetamani kuiona Tanzania yenye maendeleo endelevu .

Shujaa aliyepigania kuwa na uchumi imara , ameondoka amewaachia Watanzania urathi (legacy) wakiendelea kuamini kuwa kwa juhudi na kufanyakazi kwa nguvu na bidii zaidi, kila kitu kinawezekana kufikiwa.

La, msingi ni jitihada, maarifa, kujitoa na wakati mwingine kuacha hofu na kuwa jasiri katika kutaka kuwa na kasi ya maendeleo, akitumia kibwagizo cha hapa kazi tu.

Kazi zake zinaonekana kuanzia kuimarisha usafiri kwa kujenga miundombinu imara, kuhimiza viongozi kujituma kuhudumia na kutatua matatizo ya watu, kujenga shule nyingi za msingi na sekondari, kuanzisha viwanda na kujitoa mhanga kuhoji mikataba, kazi za uwekezaji na kutaka rasilimali za taifa zilete maendeleo ya nchi.

Ndivyo vilikuwa vita vya Magufuli kila siku mpya inapoanza na ndoto alizokuwa anaziota na kuona dhahabu, tanzanite, almasi na wanyama wa Tanzania wanaiondoa nchi kwenye umaskini.

Katika hamu yake ya kuwaandaa Watanzania wenyeji na wageni kuona ambacho hawajakiona na kula ambacho hawajakionja, aliongeza kasi ya kufanikisha ziara za utalii.

Kusafiri kwa wepesi nje na ndani ya Tanzania ndicho , alichokifanya kwa kusimamia ununuzi wa ndege na kukamilisha ujenzi wa uwanja wa kimataifa wa Dar es Salaam.

Magufuli alitamani kuona maelfu ya wasafiri wa kimataifa, wakitua Dar, kutembelea vivutia watalii na wengine wakiunganisha ndege kuelekea mataifa mbalimbali.

Alitaka watimize ndoto yao ya kuona kile ambacho hawajawahi kukiona kwa kufika Serengeti, Selous, Manyara, Mkomazi na Ngorongoro huku wakila na kunywa vyakula ambavyo hawajawahi kuvionja na kuifanya nchi kuwa moja ya mataifa barani Afrika yapendwayo na kutembelewa na wageni wengi.

Nguli huyu wa usafiri alipigania kuwapo na uwanja wa ndege wa kisasa wa Msalato International Airport mkoani Dodoma, ambao awamu ya sita inaendelea kuujenga.

> Ujenzi wa miundombinu kuanzia madaraja, makalvati, kuunganisha mikoa yote kwa lami pamoja na baadhi ya wilaya, kujenga reli ya kisasa ni mambo ambayo ulimwengu wa Afrika haukuyafumbia macho.



Hakufanya ajizi alipambana na ujangili akiukomesha na idadi ya tembo ikaongezeka , inaelezwa na Taasisi ya Africa Wild Life Foundation kwamba tembo waliongezeka kutoka mwaka 2014 wakiwa 43,000 na kufikia ndovu 60,000 mwaka 2021.

2019, Magufuli anaagiza Wizara ya Maliasili na Utalii kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya 'Nyerere National Park kwenye ukanda wa juu wa pori la Selous lengo ni kuenzi mawazo na kazi kubwa ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, kualinda na kuhifadhi mazingira na kuwa na utalii bora.

Katika juhudi za kulinda na kutunza wanyama adimu ambao hawapatikani popote kwingine kama nzohe, pongo na tohe, alianzisha pori la Burigi ambako wanapatikana kwa wingi.

Pori la Burigi linaanzia hifadhi ya taifa Rubondo, iliyo kwenye Ziwa Victoria kukiwa na wanyama wa aina mbalimbali.

**KUKOMESHA FOLENI**

Magufuli hakupenda kuona foleni barabarani . Alianza kukinai kilichokuwa kinatokea kwenye barabara za Dar es Salaam, kuanzia Ubungo hadi Chalinze.

Licha ya kuwa barabara muhimu kwa wachukuzi wa Mashariki na Kusini mwa Afrika, Barabara ya Morogoro ilikera kila mtumiaji kutokana na kuwa na foleni siku zote 365 za mwaka. Lakini Tinga Tinga kama alivyokuwa anitwa kwenye mataifa jirani alimaliza tatizo hilo.

Akiharibu kwa muda mfupi kazi zote za kiuchumi na uwekezaji zilizofanyika ndani ya miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika, Magufuli alilaumiwa kubomoa nyumba, viwanda, vitega uchumi vyote upande wa kulia na kushoto wa Barabara ya Morogoro, kuanzia Kimara hadi Kimara, akisafisha mita 241 za hifadhi ya barabara aliyodai ilivamiwa.

Ni kutoka Kimara Stop Over hadi Kibaha Maili moja na kuvunja msongamana akijenga barabara yenye njia nane ikijumuisha ya mwendo kasi ambazo zimeondoa foleni kwenye barabara ya Morogoro hasa kuanzia Mailimoja hadi Mbezi.

Wakazi wa Mbagala zote ikiwamo Rangi Tatu , maeoe ya Kilwa Road , Kurasini na ukanda wa bandarini waliokuwa wanachoshwa na foleni hakuwaacha, aliwagusa kwa kuanzisha mradi wa mabasi yaendayo haraka.

Kuanzia Mbagala hadi Kariako, Kivukoni kashi kuungana na yale yanayohudumu barabara za Morogoro na Kawawa kote wakifurahia mabasi ya mwendo kasi.

Kadhalika, ilikuwa nia yake kuufikisha mwendo kasi Tegeta Nyuki kwenye Barabara ya Bagamoyo na kufuta kilio cha foleni jijini Dar es Salaam ambacho watafiti wanasema iliigharimu jijini mabilioni ya hasara za kiuchumi na kijamii.

Mkoani Arusha wanapokumbuka kifo cha Magufuli wanafahamu kuwa anaishi wanasherehekea uwepo wa barabara ya mzunguko ya bypass ya Arusha Tengeru ambayo ni kubwa kwa Afrika Mashariki.

Kadhalika, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam, ni miji ambayo ilikuwa kwenye ramani za kuwa na barabara za mzunguko.

Magufuli hata kabla hajawa Rais alisikika akisema kuwa ujenzi wa barabara imara ni kufunga mlango wa umaskini.

Akisimamia Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuonoda Umaskini (MKUKUTA), aliamini kuwa uwepo wa barabara bora utawaondoa kwenye umaskini maelfu ya Watanzania mijini na mashambani kwa kulima, kununua, kusafirisha na kuuza bidhaa za aina mbalimbali bila kukwama.

Alijipatia sifa ya kuitwa mmoja wa askari shujaa wa miavuli kutokana na kuchapa kazi heshima anayopewa na Benjamin Mkapa, Rais wa awamu ya tatu.

Ni kiongozi aliyeendeleza dhana ya kuwa na nchi inayopitika, inayosafirika wakati wote kwa kusimamia uwapo wa Tanzania iliyoungana na wananchi wake wasafiri kutoka Mtwara hadi Mara halafu Tanga mpaka Tabora kwa taksi.

**AITIKISA AFRIKA**

Ujenzi wa miundombinu kuanzia madaraja, makalvati, kuunganisha mikoa yote kwa lami pamoja na baadhi ya wilaya, kujenga reli ya kisasa ni mambo ambayo ulimwengu wa Afrika haukuyafumbia macho.

Ni katika mkutano wa Umoja wa Afrika unaofanyika mwaka jana, Rais wa Samia Suluhu Hassan, anapokea Tuzo ya Maendeleo ya Ujenzi wa Miundombinu, Tanzania ikiwa mshindi wa mwaka 2022 wa 'Africa Road Builders-Babacar Ndiaye Trophy.'

Ni tuzo inayotolewa kwa viongozi wakuu barani Afrika ambao wameonyesha uthabiti wa kujenga na kuwa na maendeleo ya miundombinu ya usafirishaji kwenye nchi zao.

Moja ya kazi za kukumbukwa na ujenzi wa daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 513.5 (nusu kilometa) na barabara ya kuunganisha ya kilometa 3.8 iliyokamilika mwaka jana . Ujenzi huo umeondoa kero ya miaka kadhaa ya kuzunguka kona nyingi za korongo la mto Wami, zinazpfanana kama herufi 'S' zilizotesa madereva, abiria na magari kwa miongo mingi.

Rais Samia anapoipokea Tuzo ya Afrika, anakiri kuwa ni heshima ya taifa inayopatikana kutokana na kazi kubwa aliyoifanya mtangulizi wake John Magufuli, aliyeaga dunia Machi 17, 2021.

Magufuli anayetimiza miaka miwili tangu kuondoka duniani aliyaishi mafanikio na juhudi ambaozo hata sasa zinaonekana. Katika imani yake aliamini Waraka wa Wafilipi 1:21-27,kuwa 'kwangu, kuishi ni Kristo na kufa ni faida zaidi, afurahie uzima wa milele na Kristo. Amina.



# Watatu kortini tuhuma kutengeneza stakabadhi bandia

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Dodoma imewafikisha mahakamani wakurugenzi watatu wa Kampuni ya Corsyne Consult Limited kwa makosa matatu ikiwamo kutengeneza stakabadhi bandia za kielektroniki na kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 100.7.

Makosa mengine ni ulipaji wa kodi na matumizi yasiyo halali ya mashine za kutolea risiti za kielektroniki.

Ofisa Sheria wa TRA Mkoa wa Dodoma, Erasto Mtondokoso, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapo, alisema washtakiwa hao walitenda makosa hayo kati ya Julai hadi Desemba mwaka jana na kufanikiwa kutengeneza stakabadhi bandia 22 za vifaa vya ujenzi.

"Kimsingi kwa makosa hayo matatu washtakiwa wameisababishia hasara serikali ya Sh.milioni 100.7. Kwa leo tumefanikiwa kumsomea shtaka mshtakiwa wa kwanza ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni hiyo Biswalo Peter (38) ambaye hajakiri kutenda kosa hilo,"alisema.

Kwa mujibu wa Wakili Mtondokoso washtakiwa wengine watasomewa mashtaka Aprili 6, mwaka huu.

Aliwataja washtakiwa wengine ni Denisi Kisoka (38) na Ezekieli Mayunga ambao wote ni wakazi wa Mkoa wa Mwanza.

Kwa upande wake Meneja wa Idara ya Upelelezi wa Kodi Kanda ya Kati, Nicholous Njovu, alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakitengeneza stakabadhi bandia ili kukwepa kulipa kodi.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara wanaohujumu serikali kwa kutoa stakabadhi bandia kuwa TRA wako macho na imeimarisha mifumo yake kuhakikisha inawanasa watuhumiwa wote wanaokwepesha mapato ya serikali

"Natoa rai kwa wote waliokuwa na mpango wa kutengeneza risiti bandia waache mara moja, na wananchi wanatakiwa kudai risiti za kielektroniki pindi wanapofanya manunuzi,"alieleza.

Kadhalika, Njovu aliwataka wananchi kuhakiki risiti wanazopewa kama ni halisi au bandia kwa kutumia simu zao za mkononi ama kufika katika ofisi za TRA kuuliza.

Alisema: "Ofisi zetu ziko wazi muda wote, kama mwananchi ana wasiwasi na stakabadhi aliyopewa anaruhusiwa kuja kuuliza lakini anaweza kuangalia kupitia simu yake ya mkononi kwa wale wanaomiliki simu janja".

# AAFP yashauri sheria kali wanaobaka, kulawiti watoto

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wanawake wa AAFP, Shani Kitumbua, ameiomba serikali kubadilisha sheria ya adhabu kwa wanaume wanaokutwa na hatia ya kubaka au kulawiti watoto, kwamba nao wahasiwe.

Aliyasema hayo wakati wa uzinduzi wa mikutano ya hadhara uliozinduliwa kitaifa na kufanyika viwanja vya Chaduru B Kata ya Makole jijini hapo.

Kitumbua alisema adhabu hiyo itasaidia kukomesha vitendo hivyo vya kikatili kwa wanaobaka na kuwalawiti watoto.

Alisema jamii imekuwa ikishuhudia na kusikia mara kwa mara vitendo vya kikatili ambavyo vinafanywa na wanaume kwa kuwabaka na kuwalawiti watoto wadogo, huku wengine wanafanya hivyo hata kwa watoto wao wa kuwazaa.

Kiongozi huyo alisema kuwa serikali sasa inatakiwa kuangalia upya adhabu hiyo badala ya adhabu ya miaka 30 jela.

"Hata kwa wale wanaohukumiwa kutokana na makosa hayo bado wakitoka kumaliza vifungo vyao bado wanarudia makosa hayo hayo, hivyo wakibadilishiwa adhabu hiyo nafikiri itakuwa ni funzo kwa wale wanaotamani kufanya tabia hiyo ya kinyama dhidi ya watoto wadogo," alisema.

Pamoja na hayo, Mwenyekiti huyo aliwataka wanawake kujiunga na vyama vya siasa ili kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

"Hii ni fursa pekee ya kinamama kujiunga katika vyama vya siasa kwani kwa kufanya hivyo unapata uwanja mpana wa kuweza kuwasemea kinamama ambao wanakumbana na madhira mbalimbali ambayo wakati mwingine kinababa hawayajui,"alisema.

Mwenyekiti huyo pia aliwataka Watanzania wote bila kujali itikadi ya kidini, chama, rangi, kabila kuhakikisha wanajenga amani, umoja na mshikamano kwa faida ya vizazi vijavyo na siyo vinginevyo.



Meneja Matengenezo kituo cha kutunza taarifa cha Kampuni ya Vodacom Tanzania mkoani Dodoma, Mhandisi Josiah Kizinda (kulia), akitoa ufafanuzi kuhusu namna mitambo inavyofanya kazi kwa wanafunzi wa kike 96 kutoka baadhi ya shule za sekondari zilizoko mikoa ya Kanda ya Kati katika ziara iliyoandaliwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) juzi, kuwahamasisha wasichana kupenda masomo ya Sayansi na TEHAMA chini ya mpango wa 'Girls in ICT' unaoratibiwa na serikali kupitia mfuko huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# H/shauri ya Dodoma yapokea bil.14/- miaka miwili ya Samia

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imepokea Sh. bilioni 14.48 katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Joseph Mafuru, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumzia mafanikio ya miaka miwili ya serikali.

Mafuru alisema fedha hizo zimeelekezwa kwenye sekta ya afya, elimu, miundombinu na huduma zingine za kijamii.

Alisema pamoja na miradi hiyo serikali inaendelea kutekeleza miradi mingine mikubwa katika halmashauri hiyo ikiwamo pia ya ujenzi wa barabara ya mzunguko, reli ya kisasa ya mwendokasi na ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato.

Alieleza kuwa utekelezaji huo wa miradi hiyo imelenga kuboresha maisha ya wananchi kwa ajili ya maendeleo yao.

Kuhusu sekta ya elimu alisema kuwa halmashauri yake pia ilipokea Sh.bilioni 3.52 kutoka serikalini kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 172 na samani zake.

"Pia tulipokea Sh.milioni 954 kutoka kwa wahisani wa SEQUIP kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Mtemi Chiloloma, mabweni mawili na madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Bihawana na mabweni mawili, madarasa mawili na madawati 60 kwenye Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Bunge,"alisema.

Aidha, alisema Sh.milioni 750 zimepokelewa kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya ya mchepuo wa kingereza (Msangalale English Medium), huku eneo lingine ambalo lililopokea Sh. milioni 858.25 ni kwa ajili ya uboreshaji miundombinu ya elimu ya msingi.

"Hapa lazima niipongeze serikali yetu chini ya uongozi wa Rais Samia kwa kutupatia halmashauri yetu fedha nyingi zilizotolewa na awamu hii ya sita kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo,"alisema.

Alisema kuwa fedha hizo zitaleta mapinduzi makubwa katika huduma za jamii na maendeleo ya watu na halmashauri yake hiyo itaendelea kusimamia fedha hizo ili zilete matokeo makubwa na kuonyesha thamani ya fedha kwenye miradi hiyo.





# Serikali yashauriwa kujengea uwezo kampuni za mbegu

**Na Nebart Msokwa,** MBOZI

SERIKALI imeshauriwa kuzijengea uwezo kampuni za ndani zinazozalisha mbegu za mazao ili kuwa na uhakika wa upatikanaji wa mbegu kwa wakulima na kuinua uchumi.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Kukuza Mifumo ya Chakula ya Afrika (AGRA), ambaye ni Waziri Mkuu Mstaafu wa Ethiopia, Hailemariam Desalegn, alitoa ushauri huo alipotembelea mashamba ya kuzalisha mbegu ya Kampuni ya Meru AGRO yaliyopo Mbozi mkoani Songwe.

Mashamba hayo yanamilikiwa na Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendeshaji wa Mbegu za Kilimo (ASA), ambapo kampuni hiyo inazalisha mbegu za mazao mbalimbali ikiwamo za nafaka, mbegu za mafuta na mazao mbalimbali jamii ya mikunde.

Desalegn alisema kampuni za ndani zikiimarishwa nchi itakuwa na uhakika wa mbegu bora na za aina mbalimbali ambazo zitatosheleza mahitaji ya taifa kuliko kutegemea kampuni za nje ambazo wakati mwingine huwa zinazalisha mbegu za zao moja moja.

Mbali na kuwa na uhakika wa mbegu pia mwenyekiti huyo alisema serikali itaokoa kutumia fedha nyingi kuagiza mbegu nje kwa maelezo kuwa utaratibu huo pia unadidimiza uchumi wa taifa.

"Nawapongeza sana Meru AGRO kwa uzalishaji huu wa mbegu, uzalishaji huu utalisaidia taifa kuongeza kiwango cha mbegu zinazozalishwa ndani, lakini naishauri serikali kuendelea kuiwezesha kampuni hii na mengine ili kuwa na uhakika zaidi wa mbegu," alisema Desalegn.

Alisema AGRA itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuimarisha mifumo ya chakula hasa kwa kuzisaidia kampuni zinazozalisha mbegu za mazao mbalimbali.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Meru AGRO, Watanga Chacha, alisema kampuni hiyo inazalisha mbegu kwa wingi lakini bado hawakidhi mahitaji ya wakulima kutokana na uhaba wa mashamba ya kuzalishia mbegu hizo.

Alisema kwa sasa mahitaji ya mbegu za mazao ya kilimo nchini yanakaribia tani 160,000 lakini uwezo wa nchi kuzalisha mbegu hizo ni tani 60,000 pekee jambo ambalo alisema linahitaji ushirikiano kati ya serikali na kampuni binafsi katika kuongeza uzalishaji.

Aliiomba serikali kuisaidia kampuni yake kupata mashamba zaidi kwa ajili ya kuzalishia mbegu ili watosheleze mahitaji ya wakulima na kupunguza uagizaji wa mbegu hizo kutoka nje ya nchi.

Alisema endapo nchi itakuwa na uhakika wa utoshelevu wa mbegu, uzalishaji utaongezeka na nchi itakuwa na uhakika wa chakula na pia itaongeza pato la taifa kwa kuuza ziada nje ya nchi.

Mkurugenzi wa ASA, Dk. Sophia Killenga, alisema kwa sasa uzalishaji wa mbegu nchini umefikia asilimia 70 na wanaendelea na mikakati mbalimbali ili kufikia asilimia 100 ya mbegu zinazotumika nchini ziwe zinazalishwa ndani.

Alisema serikali inashirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa mbegu za mazao nchini na kwamba katika shamba la taasisi hiyo kuna kampuni nane ambayo yanazalisha mbegu.

Alisema Ethiopia ni moja ya mataifa ambayo Tanzania inajifunza kwenye uzalishaji wa mbegu hasa za ngano kwa maelezo kuwa ndani ya miaka mitatu taifa hilo limemaliza tatizo la uhaba wa ngano baada ya kuweka mikakati thabiti.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Husein Mohamed Omary, alisema Tanzania itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa kilimo kutoka ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha inakuwa na utoshelevu wa mbegu.

Alisema Wizara ya Kilimo inaendelea na michakato mbalimbali ya kuhakikisha inawawezesha wadau mbalimbali hasa sekta binafsi kwa kuweka mifumo rafiki itakayosaidia kuimarisha upatikanaji wa mbegu.

Mbali na kutembelea mashamba hayo pia Mwenyekiti huyo wa Bodi ya AGRA, alitembelea maghala ya kuhifadhia mbegu ya kampuni hiyo ya Meru pamoja na kiwanda cha kuzalisha mbegu kilichopo Iwambi jijini Mbeya.



Mwenyekiti wa Taasisi ya kukuza mifumo ya chakula ya Afrika (AGRA) ambaye pia ni Waziri Mkuu mstaafu wa Ethiopia, Hailemariam Desalegn (wa pili kulia), akikagua mbegu za mahindi zinazozalishwa na kiwanda cha Kampuni ya Meru AGRO cha jijini Mbeya mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkurugenzi wa Wakala wa Mbegu za mazao ya kilimo nchini (ASA), Dk. Sophia Killenga. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## CCM yaipongeza serikali kubadili mfumo wa ulipaji kodi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeipongeza serikali kwa kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara kwa kubadili mfumo wa ulipaji kodi uliokuwa unawasumbua na kuleta ambao ni rafiki zaidi.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) anayewakilisha Mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela, alitoa pongezi hizo juzi wakati wa maadhimisho ya miaka miwili ya Rais Samia Suluhu Hassan madarakani ambayo kitaifa yalifanyika jijini Mbeya.

Mwaselela alisema awali wafanyabiashara walikuwa wanakadiriwa kodi kabla hawajaanza kufanya biashara jambo ambalo lilikuwa linawakwaza na kuwafanya wengi kutafuta mbinu za kukwepa.

Alisema kwa sasa serikali imebadili utaratibu huo na kuwafanya wafanyabiashara kufanya kwanza biashara ndipo walipe kodi wanayostahili baada ya kufanya hesabu na kupata faida.

Alisema hali hiyo inawafanya wafanyabiashara kuwa huru na kufanya biashara zao kwa amani bila kusumbuliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema utaratibu huo utasaidia pia kuongeza idadi ya wafanyabiashara nchini na kuongeza pato la taifa hasa kutokana na makusanyo hayo ya kodi.

**Mwaselela alisema awali wafanyabiashara walikuwa wanakadiriwa kodi kabla hawajaanza kufanya biashara jambo ambalo lilikuwa linawakwaza na kuwafanya wengi kutafuta mbinu za kukwepa.**

# Wakulima chai wahamasishwa kuvuna kwa zana za kisasa

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imeanza kuwahamasisha wakulima wa chai nchini kuanza kuvuna zao hilo kwa kutumia zana za kisasa badala ya kutumia mikono.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Chai nchini (TRIT), Dk. Emmanuel Simbua, aliyasema hayo wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo kwa jina la AGRI-CONNECT.

Programu hiyo inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa katika mikoa, maeneo mbalimbali nchini ikiwamo mikoa mitano ya Nyanda za Juu Kusini na Zanzibar.

Dk. Simbua alisema tatizo la upungufu wa nguvu kazi ya kuchuma chai ilianza kuibuka baada ya kuanzishwa kwa shule nyingi za kata nchini hali iliyosababisha vijana wengi kuendelea na masomo ya sekondari baada ya kuhitimu darasa la saba.

Alisema mbali na sababu hiyo pia upungufu huo unasababishwa na vijana wengi kutopenda kufanya kazi za shambani na hivyo kukimbilia maeneo ya mjini na kutelekeza mashamba.

Alisema kwa sasa wameanza kuhamasisha matumizi ya zana za kisasa ili kurahisisha uvunaji pamoja na kuwahamasisha vijana kurudi kwenye kilimo akidai kuwa vijana wanapenda teknolojia.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Chai cha Masebe (Masebe AMCOS), Sales Mwakanyamale, alisema matumizi ya mashine hizo yamewasaidia kurahisisha uvunaji wa chai tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema kwa sasa watu wawili wana uwezo wa kuvuna zaidi ya ekari moja kwa siku tofauti na ilivyokuwa awali ambapo walikuwa wanahitaji nguvukazi kubwa zaidi.

Mwakanyamale alisema baada ya kuletewa vifaa hivyo, baadhi ya wakulima wameanza kupanua mashamba yao kwa sababu wana uhakika wa kumudu kuvuna kwa wakati.

Vilevile alisema hata vijana waliokuwa wameacha kulima chai wameanza kurejea na hata waliokuwa wametelekeza mashamba yao wameanza kuyafufua.

Alisema mashine walizopelekewa na programu hiyo, wameanza kuwafundisha vijana namna ya kuzitumia ili wazitumie kama ajira yao rasmi.

Ofisa Kiungo wa Programu ya AGRI-CONNECT kutoka katika Wizara ya Kilimo, Daines Mtei, alisema utaratibu huo wa kutumia mashine kwenye uvunaji wa chai bado upo kwenye hatua za majaribio na uhamasishaji kwa wakulima.

Alisema baadhi ya mashine hizo zimekuwa zikitumiwa na wakulima wakubwa lakini kwa wakulima wadogo zilikuwa bado hazijafikishwa lakini sasa zimeanza kuingia.

Mwakilishi wa EU, Andrea Maccarelli, alisema jumuiya hiyo inaridhika na namna ambavyo programu hiyo inatekelezwa hasa kwa kuwagusa moja kwa moja wakulima wadogo wa chai.

Alisema EU itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kuboresha sekta ya kilimo na lishe ili kuinua uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na taifa.





## SMZ yaahidi kuwaunga mkono kinamama wanaolima mwani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imesema itaendelea kutekeleza programu mbalimbali za mwani katika visiwa vya Unguja na Pemba ili kuwaunga mkono kinamama wanaojishughulisha na kilimo hicho.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi aliyasema hayo juzi wakati akizindua mpango mkakati wa miaka mitatu pamoja na mradi wa "Tumaini kit" kwa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora Foundation (ZMBF) iliyotimiza mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake.

Dk. Mwinyi alisema jukumu la kuleta maendeleo, kuwawezesha wanawake na vijana kiuchumi, ulinzi wa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili na kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto siyo la serikali peke yake bali la kila mtu. Alisema ZMBF imegusa maeneo umuhimu yanayoungwa mkono na serikali kwa ustawi mkubwa wa jamii na kuwaahidi kushirikiana nao kwenye mapambano ya kumaliza vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia kwa watoto Zanzibar.

Alisema ZMBF imegusa maeneo umuhimu yanayoungwa mkono na serikali kwa ustawi mkubwa wa jamii na kuwaahidi kushirikiana nao kwenye mapambano ya kumaliza vitendo vya udhalilishaji nchini.

Kuhusu udumavu, Dk. Mwinyi alieleza wastani wa watoto wawili kati ya 10 Zanzibar wamedumaa, hivyo aliipongeza taasisi hiyo kuangalia umuhimu wa lishe kwa watoto na kuweka mkazo kwenye eneo hilo ili kuwanusuru watoto wengi dhidi ya janga hilo kwa kuokoa kizazi cha baadaye.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alieleza janga la udumavu kwa watoto linaepukika ikiwa jamii inawekeza kwenye lishe bora kwa wajawazito na watoto wachanga tokea wanapozaliwa hadi wanapofika umri wa miaka miwili.

Msarifu na Mwenyekiti wa Bodi ya ZMBF ambaye ni Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, alisema mwaka mmoja tokea kuanzishwa kwa taasisi hiyo wamefanikiwa kuisimamisha taasisi hiyo.

Alisema wameweza kuweka sawa mifumo ya uendeshaji, kusimamia matumizi sahihi ya fedha za taasisi kwa kufanikisha vyema malengo ya taasisi hiyo.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohamed, alizitaka asasi nyingine za kiraia kuiga mfano wa ZMBF kwa kuwatumikia watu.

# 'Wafanyabiashara changamkieni fursa za uwekezaji DR Congo'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA na wawekezaji kutoka Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar wametakiwa kuchangamkia fursa za kibiashara na uwekezaji zilizopo katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) kwa sababu nchi hiyo ipo salama.

Wito huo umetolewa jana Mjini Zanzibar na Ofisa Ubalozi wa Tanzania nchini Congo, Asha Abdallah Mlekwa, wakati wa mkutano wa majadiliano kati ya Taasisi ya Uwekezaji DRC (ANAPI), Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Zanzibar.

Alisema DRC inafursa nyingi za kibiashara, hivyo wafanyabiashara na wawekezaji wasiogope na taarifa zinazotolewa katika vyombo vya habari kuhusu matatizo ya hali ya kiusalama nchini humo.

Alisema DRC ina majimbo 26 na matatizo ya kiusalama ni kwa majimbo mawili pekee ikiwamo Boma na kwamba jambo la msingi ni kabla ya kuwekeza ni kutafuta taarifa ya aina ya biashara. "Taarifa hizo wanaweza kuzipata kutoka Ubalozi wa Congo nchini Tanzania au kutoka ofisi za uwakilishi kwa maana ya Ubalozi wa Tanzania nchini DRC na serikali imefungua ubalozi mdogo katika Mji wa Lubumbashi DRC,"alisema.

Aidha, alisema dagaa kutoka Zanzibar ni maarufu nchini DRC na ni moja ya chakula kinachopendwa.

Mkurugenzi wa Utawala wa ZIPA, Vuai Yahya Lada, alisema ujio wa taasisi hiyo ya uwekezaji kutoka DRC kufika Zanzibar lengo ni kuhamasisha uwekezaji na kutangaza fursa za uwekezaji na biashara zinazopatikana nchini humo.

"Pia wamekuja kufanya kazi pamoja na ZIPA ili sisi tujifunze kutoka kwao kwa ajili ya kuimarisha vituo vya uwekezaji ambapo vyote vina lengo moja la kuvutia uwekezaji katika nchi,"alisema.

Mkurugenzi huyo alisema ZIPA imefarajika na ujio huo na wamejifunza vitu vingi kutoka ANAPI, ambavyo vitasaidia katika kukuza uwekezaji kwa sababu DRC kuna fursa nyingi za uwekezaji.

Alisema watakapotumia fursa hizo watatanua fursa za kiuchumi ya Zanzibar ambapo DRC wana ardhi kubwa ya kilimo ambayo inauwezo wa kubeba uzalishaji wa mazao kupitia umwagiliaji maji.

Hivyo, aliwataka wafanyabiashara kuzitumia fursa hizo ili kutanua wigo wa biashara baina ya nchi hiyo na Tanzania kwa sababu DRC inafursa nyingi ikiwamo madini na kilimo.

Alisema pia Zanzibar kuna fursa nyingi za uwekezaji na biashara, hivyo ni vyema wafanyabiashara na wawekezaji wa DRC wakazitumia ikiwamo katika sekta ya utalii na mazao ya baharini.

Mkurugenzi Mtendaji wa ANAPI, Antony Nkizo Kamole, alisema kilichowafanya kufika Tanzania ni katika mpango wa Rais wa DRC ambaye ametaka kufungua njia za kidiplomasia na ushirikiano wa nchi mbalimbali.

"Tumekuja hapa leo kufanya mkutano huu wa kiuchumi ili kufungua njia ya kuleta maendeleo ya kiuchumi baina ya nchi zetu mbili hizi DRC na Tanzania ikiwamo Zanzibar,"alisema.



Mmiliki wa hoteli ya Baobab ya Kizimkazi, Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Ameri Juma (katikati), akizungumza na waandishi wa habari jana, kuhusu jengo lake alilojenga ufukweni kwa ajili ya wageni kupumzika baada ya kuogelea baharini, lililobomolewa na Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Halmashauri yatoa ufafanuzi sababu kuvunja hoteli ufukweni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja, Suluhu Ali Rashid, amesema kuvunjwa kwa jengo lililojengwa katika ufukwe eneo la Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja wamezingatia taratibu za kisheria.

Alitoa ufafanuzi huo wakati akizungumza na waandishi wa habari kufuatia mgogoro uliojitokeza baina ya mmiliki wa mgahawa wa Baobab na wananchi.

Alisema moja ya sheria zinazohusiana na ujenzi katika ufukwe panatakiwa pawepo na mita 30 ya mpaka ya mwisho wa wimbi la bahari.

"Ujenzi ule uliojengwa ufukweni upo kinyume na sheria na halmashauri hatujatoa kibali cha ujenzi lakini jambo la kushangaza mmiliki wa mgahawa wa baobao amejenga katika eneo la ufukwe na kutakiwa abomoe, lakini alishindwa kufanya hivyo na ndiyo maana tumechukua uamuzi wa kubomoa," alisema.

Alisema hawakubomoa jengo hilo kwa kumwonea bali kulifuatwa sheria ya ujenzi katika kulinda bahari na ufukwe ili kudhibiti athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema halmashauri hiyo imechukua maamuzi hayo baada ya awali kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi wa kijiji hicho kulalamikia ujenzi huo, hivyo maamuzi yaliochukuliwa ni halali kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi huyo alisema ujenzi ambao unaruhusiwa kujengwa katika ufukwe ni majengo ambayo siyo ya kudumu ambayo hayatumii mawe, matofali, mchanga na saruji.

Alisema eneo la Kizimkazi lenye mgogoro huo hauruhusiwi hata kujenga ujenzi ambao si wa kudumu kwa sababu eneo hilo kasi ya maji ni kubwa hasa wakati wa maji ya bahari yanapojaa.

Hata hivyo alisema halmashauri hiyo itafanya operesheni ya kukagua maeneo yote ya ufukwe ambayo yana majengo ambayo ujenzi wake haujafuata sheria na tathmini ya kimazingira kuyabomoa majengo hayo.

Mkurugenzi huo alisema kama mmiliki huyo anataka kuendelea na shughuli zake za kuwahudumia watalii katika eneo la ufukwe afuate sheria na anaweza kuweka jengo la kuhamishika ambalo halitoaathiri hali ya kimazingira.

Alisema lengo la halmashauri ni kuwajengea mazingira bora wananchi ya biashara na wanampango wa kujenga maeneo ambapo wafanyabiashara watafanya biashara zao bila ya kubuguziwa.

Mmiliki wa Hoteli ya Baobao, Suleiman Ameri Juma, alisema lengo la ujenzi wa jengo hilo ni kwa ajili ya wageni kupumzika baada ya kumaliza kuogelea baharini na kuangalia jinsi jua linapozama.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**HERIETH STUART** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba : **S 1080-0020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MUHEZA MUSLIM SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013.kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: DAR/CHA/RB/101922/2023**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU DENNIS KALISTI TILISHO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI (PIKIPIKI YA DOMINICK DENNIS) AINA YA SANYA YENYE NAMBA ZA USAJILI **T944 BXC.** AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **DSM/PHQ/RB/189984/2022.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE AU APIGE SIMU NAMBA **0765341010.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NDUGU ROMAN EDWARD SARU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA PIKIPIKI AINA YA **SUNLG** YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 369 BQU,** AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **KAG/BIH/RB/189995/2022.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI AU APIGE SIMU NAMBA **0765341010**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**JEMINA KAIZILEGE CYPILIAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index number **S3266.0008** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **NGENGE SEKONDARI mwaka 2017.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/88897/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**IVON JOHN MALAI** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 405 DLB – TVS. Chassis namba MD625AF48N1D067991. Engine namba DF4DN1806140.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **KW/RB/1211/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI , NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

Anuani ya Simu "WARAKA — Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W)
Simu 212009 — S.L.P 5058
Telefax 2124576 — TANGA
(Makao makuu)
Simu 027-2642622-(Tanga) — 20/3/2023

**YAH.SHAURI NAMBA 7 LA MWAKA 2023**

**YASSIN IDDY TIMBANGA ....................................MDAI WA KWANZA**
**HAWA MUSSA TIMBANGA ..........................................MDAI WA PILI**
**DHIDI YA**
**ESSAEL LUCAS SWAI ..................................MDAIWA WA KWANZA**
**HAMISI MUSSA TIMBANGA ..................................MDAIWA WA PILI**

**KWA: ESSAEL LUCAS SWAI NA HAMISI MUSSA TIMBANGA**

**POPOTE MLIPO.**
**YASSIN IDDY TIMBANGA NA HAWA MUSSA TIMBANGA**

Wamefungua Shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga. Shauri husika limepangwa kutajwa Tarehe 22/3/2023 saa tatu kamili asubuhi ( 3:00 ).
Hivyo basi ,unatakiwa kuleta majibu yako ndani ya siku 21 kuanzia tarehe ya Tangazo hili kutolewa .Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya ,shauri hili litasilizwa upande mmoja na maamuzi kutolewa dhidi yako.
AMRI hii imetolewa na kutiwa saini muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 20/3/2023.

**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**TANGA**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 226/2021**
**MDAI: TKT COMP LTD**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: RASHIDI MWARAMI RASHIDI**

**KWA: RASHIDI MWARAMI RASHIDI**
Ombi la Mdai **TKT COMP LTD**
Madai ya Pesa **6,194,491**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe **04** Mwezi **04** Mwaka **2023** Saa **09:00** Asubuhi
Angalia kama hukuhudhuria/ Hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu , Mahakama ikithibitisha kama ulipokea/Umepokea kuitwa shaurini , hii itaweza kutoa hukumu kuwa mmeshindwa / umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na Chapa ya Mahakama hii leo Tarehe **21** mwezi **03** mwaka **2023**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KAHAMA OIL MILLS LTD** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.530 DTC**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KWA RB NAMBA **MWA/NY/RB/92667/2023.**

---

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha: KINGOLWIRA**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. ..../2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU**
**ASHA ALLY TEMBO WA KINGOLWIRA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SALUM SELEMAN GOGO**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 12 / Mwezi 04 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 21 mwezi 03 mwaka 2023**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA**
**WILAYA YA KIBAHA**
**SHAURI LA ARDHI NAMBARI 170 LA 2022**
**TUJIJENGE TANZANIA LIMITED............**
**MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**SALOME DANIEL.........WAJIBU MAOMBI**

**TANGAZO**

Wewe **SALOME DANIEL** popote pale ulipo unaamriwa na Baraza hili la Ardhi na Nyumba Kibaha kuhudhuria hapa kwenye Baraza mnamo tarehe 12.04.2023, kama hautahudhuria basi Baraza hili litasikiliza upande mmoja na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 15 mwezi machi, 2023
**MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**KIBAHA-PWANI**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA
NYUMBA LA WILAYA YA
KIBAHA
TANZANIA

---

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## Mauzo nafaka nje yaongezeka

**Na Restuta James**

TANZANIA imeongeza mauzo ya nje ya nafaka, matunda na mboga yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 6.6 katika kipindi cha miaka mitano.

Takwimu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) na Wizara ya Kilimo, zilizotolewa juzi jijini Dar es Salaam zinaonyesha Tanzania imeuza mazao hayo katika nchi za Afrika Mashariki, Kusini mwa Afrika, Pembe ya Afrika na sehemu mbalimbali duniani.

Takwimu hizo zinaonesha kuwa Tanzania iliuza mboga zenye thamani ya Dola za Marekani bilioni 1.01 (Sh. trilioni 2.4) kati ya mwaka 2018 hadi 2022.

Mchele na mahindi yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 999 (Sh. trilioni 2.3) viliuzwa katika kipindi hicho.

Kwa mujibu wa takwimu hizo, mauzo ya nje ya nchi ya samaki na bidhaa za samaki yalifikia Dola za Marekani milioni 800 (Sh. trilioni 1.9) na matunda yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 71.4 (Sh. bilioni 170) kati ya 2018 na 2022.

Takwimu hizo zinaonesha kuwa Tanzania ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa watano wa mchele barani Afrika na ndio mzalishaji mkubwa zaidi wa mchele Afrika Mashariki.

BoT ilieleza kwamba katika msimu wa 2020/21, Tanzania ilizalisha tani milioni 1.85 za mchele, wakati mahitaji ya nchi kwa mwaka ni takribani tani milioni moja hivyo kuwa na ziada ya tani 850,000 za zao hilo.

Takwimu hizo zinaonyesha kwamba katika msimu huo, Tanzania ilizalisha tani milioni 6.5 za mahindi, ukilinganisha na nahitaji ya taifa ya tani milioni sita kwa mwaka.

Kwa mujibu wa BoT, uzalishaji huo umetokana na ongezeko la bajeti ya kilimo uliofanywa na serikali kupitia ruzuku ya mbegu, mbolea na kilimo cha umwagiliaji.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (mwenye suti nyeusi), akiwa na baadhi ya vijana ambao ni washiriki wa programu ya kilimo biashara 'Building a Better Tomorrow' BBT, baada ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuzindua programu hiyo Chamwino mkoani Dodoma juzi. TADB imetoa zaidi ya shilingi milioni 500 kununua zana na vitendea kazi vya kilimo kwa ajili ya vijana 812 waliojiunga na programu hiyo kwa awamu ya kwanza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mfuko WCF watambulika kimataifa

**Na Joseph Mwendapole**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), umetambulika kimataifa kama mfano wa kuigwa katika kutoa huduma kwa wafanyakazi wanaopata ulemavu na majanga mbalimbali wakiwa kazini.

Kutokana na umahiri wa mfuko huo, nchi mbalimbali za Afrika zimekuja nchini kujifunza namna mfuko huo ulivyofanikiwa kutoa huduma hizo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Uendeshaji wa mfuko huo, Anselim Peter, wakati wa mkutano na wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF), uliofanyika wilayani Bagamoyo, Pwani.

Alisema hata Shirika la Kazi Duniani (ILO), limechukua mfuko huo kuwa wa mfano kwa mataifa mbalimbali ya Afrika na nje kutokana na kuonyesha umahiri kwenye utoaji wa huduma kwa wafanyakazi wanaoumia kazini.

"ILO wameshamkaribisha Mkurugenzi mkuu wa WCF mara mbili kwenye mikutano yao kwenda kutoa uzoefu wake namna mfuko huo ulivyoanzishwa na unavyofanyakazi, lakini ILO iliwahi kuiagiza Kenya ije kujifunza hapa namna ya kuanzisha mfuko kama WCF," alisema.

Alisema Kenya tayari ilishaleta watumishi wake wengi wa serikali kuja kujifunza kuhusu kuanzisha mfuko wa aina hiyo na kuongeza kwamba Zambia nao wameshakuja kujifunza.

"Malawi waliomba kuja kujifunza, lakini bado hawajaja tunaamini watakuja na kwa kweli tumejitahidi kutoa huduma zetu kwa mtandao asilimia zaidi ya 80 ya huduma zetu zinatolewa kwa njia ya mtandao," alisema. Wakati huo huo, alisema hatua ya serikali kupunguza riba ya wanaochelewesha michango WCF kutoka asilimia 10 hadi asilimia mbili imeleta mafanikio makubwa kwenye mfuko huo kwa kuwa watu wengi waliokuwa wamechelewesha malipo walifikisha kwa wakati.

Alisema hatua hiyo ilisababisha ahueni kubwa kwa waliokuwa wakidaiwa fedha nyingi zilizotokana na riba ambao baada ya punguzo hilo waliwasilisha michango yao.

Alisema ndani ya mwaka mmoja tangu kutolewa kwa punguzo hilo WCF ilifanikiwa kukusanya michango inayofikia Sh. bilioni 15.

"Unakuta mtu alikuwa anadaiwa mchango shilingi milioni mbili, lakini riba milioni 20 kwa hiyo kwa kusamehe ile riba waajiri wengi walilipa kwa wingi kwa hiari na tangu hapo watu wakaendelea kulipa kwa wakati bila usumbufu wowote," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, John Mduma, alisema majukumu ya WCF ni kuwafidia wafanyakazi wanaopata majanga wakati wanatekeleza majukumu yao ya kazi.

Alisema serikali imefanya mambo makubwa kwa miaka yake miwili madarakani ikiwamo kuwapunguzia sekta binafsi michango kutoka asilimia moja ya mshahara wa mfanyakazi mpaka kufikia asilimia 0.6 na baadaye ikashushwa mpaka asilimia 0.5.

Alisema riba hiyo kubwa ilisababisha waajiri wengi ambao walikuwa hawajajisajili WCF kusita kwenda kujisajili kwa hofu ya kukutana na riba kubwa ambayo wengi wasingemudu kuilipa.

"Pia serikali ya awamu ya sita si tu kwamba ilipunguza riba ya kuchelewesha bali iliamua kufuta yale madeni ya riba kwa hiyo waajiri sekta binafsi wakabaki wanalipa madeni msingi tu lakini madeni yale ya riba yalifutwa yote," alisema.

# Kigamboni kutambua machimbo ya vifusi

**Na Beatrice Shayo**

WILAYA ya Kigamboni imesema imeanza mchakato wa kuyatambua maeneo yote ya machimbo ya vifusi vya kokoto yaliyopo Mbutu ili kulipa fidia kwa wananchi wenye maeneo hayo.

Akihojiwa na waandishi wa habari, Ofisa wa Idara ya Mazingira katika halmashauri hiyo, Juvenalis Mauna, alisema serikali ipo katika harakati ya kuyatambua maeneo yote kwenye machimbo hayo ili mchakato wa ulipaji wa fidia uanze.

Alisema kinachofanyika sasa ni kuhakikisha eneo lote la uchimbaji linakuwa maalum kwa shughuli za machimbo na kwamba idara ya madini, ilifanikiwa kufika katika machimbo hayo na imeshawafungia leseni waliosababisha kutokea kwa ajali iliyoua watu watatu hivi karibuni.

"Kuna mambo mawili hapa katika suala la ulipaji fidia yanaweza kufanyika, kuna wale ambao watalipwa na kukubali kuondoka moja kwa moja na wapo ambao watayatoa maeneo yao kwa kampuni za uchimbaji ambao watawalipa na baadaye wanarudishiwa maeneo yao, lakini ikumbukwe kwamba mchakato umeanza ila hauwezi kuisha kwa mara moja," alisema.

Asha Omary ni mkazi wa Mbutu na mchimbaji wa kokoto alisema licha ya serikali kujipatia mapato kutokana na mradi huo wanaiomba kuiboresha barabara iliyopo katika machimbo hayo, ili kupunguza vumbi linalowapata kila siku.

"Pia tunaiomba serikali kutuletea maji na umeme katika eneo hili la Mbutu ambalo ni maarufu kwa utoaji wa vifusi vya kokoto ambavyo vinatumika kuteketeza miradi mikubwa ya serikali, tunafahamu wanataka kuyatambua maeneo yote hivyo tuombe mchakato wa fidia kama upo basi ufanyike kwa haraka na wakati," alisema.


Mchungaji Stephen Mshana ambaye ni mchimba kokoto katika eneo hilo, alisema kuna kinamama wengi wanaohitaji kupatiwa mikopo na kuomba halmashauri iwakumbuke.

"Hapa kuna kinamama wengi wanafanya kazi ya kuchimba kokoto na kuziponda, ipo mikopo ya halmashauri ni vema na wao wakakumbukwa na kuangaliwa kwa jicho la tatu ili wasifanye kazi hii kwa muda mrefu," alisema.

Septembe 30, mwaka jana Waziri Jafo akiwa katika machimbo hayo hakufurahishwa na shughuli za uchimbaji zinavyofanyika kutokana na kutozingatia utunzaji na uhifadhi wa mazingira huku mmiliki wa machimbo kutofanya tathmini ya athari kwa mazingira na wala hana cheti cha mazingira kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



HABARI MICHEZO

# SINGIDA BIG STARS WATAKA KUKIPIGA MICHUANO CAF

**Na Shufaa Lyimo**

WAKATI Tanzania ikiwa na uhakika wakuingiza tena timu nne kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu msimu ujao, uongozi wa Klabu ya Singida Big Stars, umesema malengo yao ni kuibuka na ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup pamoja na kumaliza nafasi tatu za juu Ligi Kuu Bara ili kuwa miongoni mwa zitakazopata nafasi hiyo.

Timu tatu zitakazomaliza nafasi za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara, zitakata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho.

**Hata hivyo, timu itakayomaliza nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, inaweza kupata nafasi ya kushiriki michuano hiyo ya CAF, endapo tu timu itakayotwaa Kombe la FA, itakuwa ndiyo iliyobeba ubingwa wa Ligi Kuu Bara, jambo ambalo limeongeza ushindani mkubwa kwenye ligi hiyo kila moja ikiwania nafasi hiyo ya kushiriki michuano ya kimataifa.**

Bingwa wa Ligi Kuu na mshindi wa wa pili huiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati mshindi wa Kombe la FA na itakayoshika nafasi ya tatu, hupeperusha bendera ya nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Singida Big Stars, John Kadutu, alisema mikakati yao ni kuhakikisha wanashika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na kutwaa Kombe la Shirikisho, FA Cup.

"Malengo yetu ni kushika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na ubingwa wa Kombe la Shirikisho la Azam," alisema Kadutu.

Mtendaji huyo aliweka wazi kuwa kila mchezo kwao ni fainali na kuahidi kupata pointi tatu kwenye michezo iliyobakia kabla ya ligi hiyo kufikia ukingoni.

Alisema kutokana na juhudi zinazoonyeshwa na wachezaji wao wana matumaini ya kushiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hapo mwakani.

"Tutapambana kuhakikisha mwakani tunashiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, hakuna linaloshindikana," alisema mtendaji huyo.

KIKAPU...



Mchezaji wa Shule ya Sekondari, Don Bosco (jezi nyeupe), akimiliki mpira huku akipata upinzani mkali kutoka kwa wachezaji wa timu ya Shule ya Sekondari Mtakuja, jana katika michuano ya Kikapu kwa Shule za Sekondari inayoendelea kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Taifa Stars kamili kuivaa Uganda*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Hemed Morocco, amesema maandalizi yanaendelea vizuri na wanamatumaini makubwa ya kufanya vizuri katika mchezo wa kutasaka nafasi ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023 dhidi ya Uganda.

Kikosi cha Stars kimekamilika baada ya kundi la pili la wachezaji akiwamo kiungo Feisal Salum (Fei Toto), kuungana na wachezaji wenzake kujiandaa na mchezo huo utakaopigwa keshokutwa, Ijumaa katika Uwanja wa Suez Canal, Ismailia nchini Misri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Morocco alisema maanadlizi yako vizuri baada ya kufanya mazoezi ya gym ya kutafuta stamina na uwanjani, wachezaji watakuwa fiti kwa ajili ya mchezo huo.

Alisema wachezaji wameanza kuelewana licha ya kukutana muda mfupi, wanaimani nao kupambana katika mchezo huo ili kupata matokeo mazuri .

"Tunatambua mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu ya ugumu wa mchezo hasa tunapokutana na Uganda, ni imani yangu kwa wachezaji tuliokuwa nao tutapata matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Alisema wanaendelea kufanya mazoezi ya nguvu kuhakikisha wanapata matokeo katika mchezo huo ili kupata kujiweka katika nafasi nzuri ya kufuzu.

Morocco alisema anatumai wanaweza kupata matokeo katika mcheo huo na ule wa marudianoa utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumanne ijayo.

Katika msimamo wa Kundi F, Algeria ipo kileleni ikiwa na pointi sita ikifuatiwa na Niger yenye alama mbili huku Taifa Stars na Uganda zikifuata kutokana na kulingana kila kitu kila moja akiwa na pointi moja.

Timu mbili zitakazoshika nafasi ya juu kutoka katika kila kundi zitafuzu kushiriki michuano hiyo ya Afcon itakayofanyika nchini Ivory Coast baadaye mwaka huu.

## 35 Ligi Kuu waitwa timu zao za taifa

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya wachezaji 35 wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara, wameitwa kuzitumikia timu zao za taifa kwenye michuano ya kusaka tiketi ya kufuzu michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2023, pamoja na mechi mbalimbali za kirafiki zilizo kwenye Kalenda ya FIFA.

Taarifa iliyotolewa na Bodi ya Ligi, kati ya wachezaji hao, 19 wameitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, inayojiandaa na mechi dhidi ya Uganda Cranes, ikiwa ni ya kufuzu Afcon 2023 kwenye Kundi F.

Stars inacheza na Uganda keshokutwa, Ijumaa nchini Misri na kurudiana Jumanne ijayo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wachezaji hao wamechaguliwa kutoka klabu mbalimbali zinazocheza Ligi Kuu nchini, huku 16 waliobaki ni wale wa kigeni wanaocheza soka la kulipwa nchini ambao wameitwa kuyatumikia mataifa yao, baadhi wakienda nao kucheza mechi za Afcon na wengine mechi za kirafiki.

Wakati Tanzania ikiwa na wachezaji 19 waliokwenda Stars, nchi inayofuata kuwa na wachezaji wengi kwenye timu yake ya taifa walioitwa wakitokea Ligi Kuu Bara ni Burundi ambayo imeita wachezaji wanne.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo na Zambia kila moja imeita wachezaji wawili kutoka Ligi Kuu ya Tanzania.

Nchi zingine ambao zimeita wachezaji mmoja mmoja wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara, ni Burkina Faso, Comoro, Kenya, Malawi, Mali, Rwanda, Senegal na Uganda.

## Sayari Women yaibukia Ligi Mkoa

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya kwanza ya mpira wa miguu ya wanawake nchini, Sayari Women (zamani Sayari Queens), imeibukia Ligi ya Mkoa wa Dar es Salaam baada ya kupotea kwa muda mrefu kwenye ramani ya mchezo huo.

Timu hiyo iliyokuwa mzizi wa soka la wanawake nchini, imeibukia kwenye ligi hiyo, ambapo imeanza tena safari yake ya kurejea kwenye ramani ya soka, ikicheza mechi tatu, ikishinda mbili na kupoteza moja, ikiwa na pointi sita na kushika nafasi ya tatu kwenye ligi hiyo.

Mbali na timu hiyo, wapinzani wao, Tanzanite Princess nao wamo kwenye ligi hiyo wakishika nafasi ya 11 kati ya 12 zinazoshiriki, ikipoteza mechi zote tatu ilizocheza.

Kwa mujibu wa Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), Ligi ya Mkoa Dar es Salaam imeanza huku Mbagala Queens ikiongoza kwa kuwa na pointi tisa, ikicheza mechi tatu na kushinda zote, huku Youngstars Queens ikishika nafasi ya pili ikiwa na pointi saba, ikishinda mbili na sare moja.

## ZISIKUPITE

### KANE SOKONI KWA MIL. 100

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka pauni milioni 100 ili kumwachia mshambuliaji wa England, Harry Kane ikiwa watafikiria kumuuza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, msimu huu wa majira ya joto wakati atakuwa amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake. ***(Times)***

### BELLINGHAM AWANIWA CITY

MANCHESTER City inazidi kujiamini kuwa inaweza kumpata, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19, msimu huu wa majira ya joto, lakini Real Madrid wanabaki kwenye mbio za kumnunua kiungo huyo wa kati wa Borussia Dortmund. ***(ESPN)***

### UNITED NA BEI YA KIJINGA

BILIONEA anayetaka kuinunua Manchester United, Sir Jim Ratcliffe, amesema hataki kulipa "bei ya kijinga" kwa klabu hiyo. ***(Wall Street Journal)***

### CONTE KUONDOKA SPURS

TOTTENHAM Hotspur inatarajiwa kukubaliana na kuondoka kwa kocha wao, Antonio Conte, mwenye umri wa miaka 53 wiki hii, huku mchezaji wa zamani wa timu hiyo, Ryan Mason (31), akitarajiwa kuchukua usukani hadi mwisho wa msimu. ***(Telegraph)***

### ODEGAARD MKATABA MPYA

ARSENAL iko tayari kumpa mchezaji wa Norway, Martin Odegaard, mwenye umri wa miaka 24, mkataba mpya wa kumbakisha katika klabu hiyo hadi mwaka 2030. ***(Football Transfers)***

### MCTOMINAY ATAKIWA UNITED

KLABU ya Newcastle United inamlenga kiungo wa Manchester United, Scott McTominay wakati wa kipindi cha majira ya joto na mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland mwenye umri wa miaka 26, anaaminika kuwa tayari kuhama. ***(Telegraph)***

### KANTE AOTA MBAWA JUVE

MATUMAINI ya Juventus kumsajili, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31, bila malipo msimu wa majira ya joto yamekatizwa, huku kiungo huyo wa kati wa Ufaransa akitarajiwa kusaini mkataba mpya wa miaka miwili na Chelsea. ***(Tuttomercato)***

### OKAFOR LULU SPURS, ARSENAL

KLABU za Arsenal, Tottenham Hotspur na West Ham zinamwania mshambuliaji wa Red Bull Salzburg, Noah Okafor, huku mkataba wa mchezaji huyo ukitarajiwa kumalizika msimu huu wa majira ya joto wa mwaka 2024. ***(Mail)***

### MARTINEZ KUBAKI VILLA

GOLIKIPA wa Aston Villa aliyeshinda Kombe la Dunia, Emiliano Martinez, mwenye umri wa miaka 30, amesisitiza kuwa anapanga kubaki katika klabu hiyo, licha ya kutakiwa sana na timu nyingine. ***(Mirror)***

### MENDY KUPELEKWA SOKONI

CHELSEA iko tayari kumuuza mlinda mlango wa Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 31, baada ya kuvunjika kwa mazungumzo ya kuongeza mkataba. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# DESCHAMPS: MBAPPE ANA SIFA KUWA NAHODHA WA UFARANSA

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe ana sifa za mawasiliano za kuwa nahodha wa Ufaransa, lakini Kocha Didier Deschamps, bado hajaamua nani wa kumpa nafasi hiyo wakati huu akitafuta mrithi wa Hugo Lloris.

**Kustaafu kwa Lloris katika soka la kimataifa kumeifanya 'Les Bleus' kuhitaji nahodha mpya, huku Mbappe akionekana kutajwa zaidi.**

Akizungumza na Telefoot wiki iliyopita, Lloris alisema: "Kuna mchezaji mmoja ambaye anakuwa na nguvu zaidi katika kila nyanja ndani na nje ya uwanja na hata kwenye vyumba vya kubadilishia nguo - huyo ni Kylian Mbappe."

Ufaransa itacheza na Uholanzi katika mechi ya kufuzu Euro 2024 Ijumaa, na Deschamps alikabiliwa na maswali ya mara kwa mara kuhusu utambulisho wa nahodha mpya.

**Nitatumia siku hizi chache za kwanza na kikundi kujadili na wachezaji wanaohusika...**

"Nitatumia siku hizi chache za kwanza na kikundi kujadili na wachezaji wanaohusika," alisema Deschamps.

"Ni wazi, Kylian ni mmoja wa wachezaji hao. Kwa hiyo, utajua zaidi wakati mwingine nitakapokuona. Kwa maneno mengine, siku moja kabla ya mchezo, Alhamisi.

"Nadhani kama yeye (Mbappe) ana sifa moja, pamoja na sifa zake nyingine zote, ni kwamba ni mtu mzuri sana, mzuri sana katika mawasiliano. Kwa hiyo, sidhani kama hilo ni tatizo kwa upande huo. Lakini siwezi kukuambia zaidi kwa sababu sijaamua leo."

Mbappe alikuwa nahodha wa PSG Jumapili walipopokea kichapo cha kushangaza cha mabao 2-0 wakiwa nyumbani dhidi ya Rennes.

Deschamps aliongeza: "Nina mazoea, na si sasa hivi nitabadilika, kwa kila mchezaji anapokuwa kwenye klabu yake, sina cha kuongeza.

"Ni kweli, mimi hutazama michezo. Lakini hali ya Kylian au hali ya mchezaji yeyote katika ngazi ya klabu si sawa na aliyonayo hapa na timu ya taifa, hivyo haitakuwa njia yangu ya kuchagua.

"Inahusisha majadiliano ya kina zaidi. Kuna aina tofauti za unahodha. Ni jukumu, anawekwa mbele. Kuna aina tofauti au tuseme uwezekano, na baadhi ya wachezaji wanajieleza zaidi au kidogo.

"Sitaangalia undani kwa sababu pia unapaswa kuzingatia hali ambayo klabu inaweza kujikuta. Haya ni mambo ambayo sina, sio kawaida yangu ya kila siku."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,093,3

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 23 NA 24 MACHI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/03/23 | 22:45 | Italy vs England | 2.76 | 3.25 | 2.63 |
| 02. 24/03/23 | 02:00 | La Equidad vs Chico | 2.52 | 2.90 | 2.80 |
| 03. 24/03/23 | 04:10 | America De Cali vs Junior Barranquilla | 2.21 | 3.14 | 3.35 |
| 04. 24/03/23 | 12:00 | Australia vs Ecuador | 2.69 | 3.17 | 2.69 |
| 05. 24/03/23 | 13:30 | Japan vs Uruguay | 2.85 | 3.23 | 2.50 |
| 06. 24/03/23 | 14:00 | South Korea vs Colombia | 3.02 | 3.13 | 2.44 |
| 07. 24/03/23 | 20:00 | Bulgaria vs Montenegro | 2.60 | 3.15 | 2.88 |
| 08. 24/03/23 | 20:00 | Denizlispor vs Boluspor | 2.77 | 3.23 | 2.28 |
| 09. 24.03/23 | 20:30 | Saint Brieuc vs Nancy | 2.68 | 2.95 | 2.68 |
| 10. 24/03/23 | 20:30 | Cholet vs FC Versailles 78 | 2.44 | 3.16 | 2.79 |
| 11. 24/03/23 | 20:30 | Paris 13 Atletico vs Bourg Peronnas | 2.67 | 2.98 | 2.67 |
| 12. 24/03/23 | 20:30 | Sedan vs Dunkerque | 2.43 | 3.11 | 2.85 |
| 13. 24/03/23 | 20:30 | Avranches vs Le Puy | 2.21 | 3.16 | 3.16 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DE JONG AJIONDOA KIKOSI CHA UHOLANZI



**AMSTERDAM,** Uholanzi

FRENKIE de Jong hatacheza katika mechi mbili za ufunguzi za Uholanzi za kufuzu Euro 2024 kutokana na jeraha.

Kiungo huyo wa kati wa Barcelona alicheza kwa dakika zote 90 wakati 'Blaugrana' hao walipoilaza Real Madrid mabao 2-1 katika mechi ya Jumapili ya El Clasico na kukaa kileleni kwa tofauti ya pointi 12.

Lakini aliachwa na maumivu ya msimu ya paja na Shirikisho la Soka la Uholanzi (KNVB), lilisema amejiondoa kwenye kikosi cha Oranje kwa mechi zao zijazo.

Mshambuliaji wa Ajax, Steven Bergwijn, pia amelazimika kujiondoa kutokana na jeraha la goti.

Kiungo wa kati wa PSV, Joey Veerman na Donyell Malen wa Borussia Dortmund wamechaguliwa na Ronald Koeman kama mbadala wa wawili hao.

Uholanzi wataanza kampeni yao dhidi ya Ufaransa mjini Paris Ijumaa, kabla ya kuwakaribisha Gibraltar katika Uwanja wa De Kuip siku tatu baadaye.

Safari ya Ijumaa kwenda Ufaransa itakuwa mechi ya kwanza ya kipindi cha pili cha Koeman kama kocha.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona, alithibitishwa kuwa kocha mkuu wa Oranje kabla ya Kombe la Dunia mwaka jana, baada ya Louis van Gaal kujiuzulu akitoka kuifikisha robo fainali ya Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar.



# Ratcliffe: Sitalipa bei ya kijinga kuinunua Manchester United

**LONDON,** England

BILIONEA wa Uingereza, Jim Ratcliffe, amesisitiza kuwa hatalipa "bei ya kijinga" kuinunua Manchester United huku muda wa mwisho wa zabuni ukikaribia.

Wamiliki walio madarakani, familia ya Glazer, waliiweka United sokoni Novemba mwaka jana na Ratcliffe alikuwa mtu wa kwanza kuonesha nia ya kuinunua kupitia Kampuni yake ya Kemikali ya INEOS yenye makao yake jijini London.

Baadaye alikuwa miongoni mwa wahusika wa kwanza kuwasilisha zabuni za awali kabla ya Februari, huku mfanyabiashara wa Benki wa Qatar, Sheikh Jassim bin Hamad Al Thani, naye akijitosa kutoa zabuni yake.

Ingawa thamani kamili ya zabuni hizo haijulikani, Glazers imeripotiwa kuwa inataka angalau pauni bilioni 5.9 kuiuza klabu hiyo, ambayo itakuwa ada mpya ya rekodi ya dunia k timu ya michezo.

Kwa mujibu wa Forb klabu hiyo ilikuwa na th mani ya pauni milioni n mwaka jana.

Ripoti za hivi majuzi z pendekeza wazabuni w nazidi kujiamini kuwa Gl ers ataidhinisha mauz huku Ratcliffe na Shei Jassim wakitarajiwa k wasilisha ofa rasmi wiki h

Lakini Ratcliffe amet dalili ya wazi zaidi kwam hatalipa kiasi kikubwa za cha fedha.

395,265/-

## SUPA JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/03/23 | 18:00 | Doncaster Rovers vs Northampton Town | 2.50 | 3.15 | 2.70 |
| 02. 25/03/23 | 18:00 | Peterborough United vs Derby County | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 03. 25/03/23 | 18:15 | Racing Santander vs Levante UD | 3.45 | 3.00 | 2.15 |
| 04. 25/03/23 | 18:15 | UD Ibiza vs Burgos CF | 2.33 | 2.80 | 3.30 |
| 05. 25/03/23 | 23:00 | Bogota FC vs Tigres FC | 2.27 | 2.85 | 2.90 |
| 06. 25/03/23 | 23:30 | Portland Timbers vs Los Angeles Galaxy | 2.14 | 3.30 | 2.70 |
| 07. 26/03/23 | 02:30 | DC United vs New England Revolution | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 08. 26/03/23 | 02:30 | Charlotte FC vs New York Red Bulls | 2.39 | 3.00 | 2.60 |
| 09. 26/03/23 | 02:30 | Columbus Crew vs Atlanta United FC | 2.40 | 3.10 | 2.50 |
| 10. 26/03/23 | 03:30 | Houston Dynamo vs New York City FC | 2.44 | 3.10 | 2.45 |
| 11. 26/03/23 | 03:30 | Sporting Kansas City vs Seattle Sounders | 2.21 | 3.15 | 2.70 |
| 12. 26/03/23 | 04:05 | CF Correcaminos UAT vs CD Mineros de Zacatecas | 2.16 | 2.95 | 2.95 |
| 13. 26/03/23 | 06:05 | Pumas de Tabasco vs Raya2 Expansion | 2.49 | 2.95 | 2.49 |
| 14. 26/03/23 | 08:00 | Iwaki FC vs Machida Zelvia | 2.50 | 2.95 | 2.47 |
| 15. 26/03/23 | 15:30 | FC Dordrecht vs Helmond Sport | 2.47 | 3.15 | 2.39 |
| 16. 26/03/23 | 17:15 | SD Ponferradina vs CD Mirandes | 2.07 | 3.10 | 3.50 |
| 17. 26/03/23 | 17:15 | Real Zaragoza vs Albacete Balompie | 2.10 | 3.00 | 3.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMATANO - 22/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1153 | Zlin U19 vs Brno U19 | 3.12 | 3.90 | 1.91 |
| 14:00 | 4802 | CS Maritimo U23 vs Portimonense U23 | 2.47 | 3.42 | 2.48 |
| 16:00 | 3429 | Israel U19 vs Poland U19 | 2.64 | 3.15 | 2.48 |
| 16:00 | 4332 | US Chaouia vs CR Belouizdad | 9.12 | 5.18 | 1.25 |
| 17:00 | 1558 | Iceland U19 vs Turkey U19 | 3.73 | 3.52 | 1.82 |
| 17:00 | 3005 | Norway U20 vs Romania U19 | 1.91 | 3.21 | 3.78 |
| 17:00 | 4679 | FC Rad vs FK Loznica | 1.66 | 3.34 | 4.83 |
| 17:00 | 4761 | Polonia Bytom SA vs Rekord Bielsko Biala | 1.82 | 3.45 | 3.35 |
| 18:00 | 1995 | Leixoes SC U23 vs CD Mafra U23 | 1.68 | 3.79 | 4.15 |
| 18:00 | 4172 | Slovenia U21 vs Slovakia U21 | 2.48 | 3.06 | 2.70 |
| 18:00 | 4807 | Benin vs Rwanda | 1.98 | 3.25 | 3.89 |
| 19:00 | 2840 | FK Trajal vs FK Radnicki Beograd | 2.67 | 2.72 | 2.72 |
| 20:00 | 1124 | France U19 vs Northern Ireland U19 | 1.13 | 6.81 | 15.49 |
| 20:00 | 3898 | Sierra Leone vs Sao Tome and Principe | 1.17 | 6.83 | 13.88 |
| 20:45 | 1080 | Lyon W vs Chelsea W | 2.16 | 3.42 | 2.90 |
| 21:00 | 1943 | Germania Halberstadt vs Hertha II | 3.94 | 3.73 | 1.73 |
| 21:30 | 1351 | Sportfreunde Baumberg vs VfB Homberg | 2.04 | 3.53 | 3.07 |
| 21:30 | 2373 | SC Union Nettetal vs TUS 64 Bosinghoven | 3.38 | 3.79 | 1.85 |
| 21:30 | 2379 | TVD Velbert 1870 vs Schwarz-Weiss Essen | 2.46 | 3.57 | 2.42 |
| 21:30 | 2525 | Oldenburger SV vs FC Dornbreite | 1.50 | 4.56 | 4.66 |
| 21:30 | 2863 | SC St Tonis 11/20 vs Ssvg Velbert | 5.07 | 4.14 | 1.51 |
| 21:30 | 2884 | MSV Dusseldorf vs Kray | 1.56 | 4.35 | 4.35 |
| 21:30 | 3577 | Cronenberger SC vs 1.fc Monheim | 4.11 | 4.16 | 1.62 |
| 21:30 | 4674 | FSV Duisburg vs VfB 03 Hilden | 13.50 | 6.65 | 1.14 |
| 21:30 | 5290 | SV Westfalia Rhynern vs SC Paderborn 07 II | 2.31 | 3.20 | 2.55 |
| 21:30 | 5525 | Spvg Schonnebeck 1910 vs Turu Dusseldorf 1880 | 1.66 | 3.85 | 3.60 |
| 21:30 | 5757 | Ratingen SV vs SF Hamborn 07 | 1.47 | 4.30 | 4.40 |
| 21:30 | 5871 | SV Sonsbeck vs 1 FC Kleve | 2.91 | 3.79 | 2.03 |
| 22:00 | 1007 | FC Luzern II vs SC Kriens | 1.50 | 4.22 | 4.83 |
| 22:00 | 1667 | Standard Liege W vs Anderlecht W | 3.52 | 3.78 | 1.81 |
| 22:00 | 3511 | Rapperswil vs FC Baden | 2.13 | 3.43 | 2.87 |
| 22:00 | 4227 | SV Neuhof-Rot vs Weiss Hadamar | 2.33 | 3.50 | 2.34 |
| 22:00 | 5924 | Ukraine U19 vs Luxembourg U19 | 1.33 | 4.56 | 7.88 |
| 22:30 | 1637 | England U20 vs Germany U20 | 2.11 | 3.41 | 3.00 |
| 22:45 | 2994 | Mansfield vs Grimsby | 1.83 | 3.36 | 3.91 |
| 22:45 | 5294 | Ireland vs Latvia | 1.35 | 4.75 | 9.28 |
| 23:00 | 5988 | Paris Saint Germain W vs Wolfsburg W | 2.25 | 3.36 | 2.79 |

### ALHAMISI - 23/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:00 | 3164 | Alacranes de Durango vs Pumas De Tabasco | 2.21 | 3.22 | 2.96 |
| 04:00 | 3014 | Millonarios FC vs Deportivo Pasto | 1.69 | 3.36 | 4.76 |
| 04:05 | 3486 | Raya2 Expansion vs Correcaminos Uat | 2.18 | 3.25 | 3.00 |
| 06:00 | 4721 | EL Salvador vs Honduras | 2.84 | 3.11 | 2.59 |
| 06:05 | 2718 | Venados FC vs CD Tapatio | 2.11 | 3.20 | 3.20 |
| 09:00 | 4647 | New Zealand vs China | 1.75 | 3.56 | 4.85 |
| 13:00 | 3468 | Malaysia vs Turkmenistan | 1.80 | 3.55 | 4.52 |
| 15:00 | 2987 | Hong Kong vs Singapore | 2.04 | 3.38 | 3.65 |
| 16:00 | 1275 | Madagascar vs Central African Republic | 1.76 | 3.45 | 4.68 |
| 18:00 | 3603 | Kazakhstan vs Slovenia | 3.90 | 3.42 | 2.00 |
| 20:00 | 1579 | Iran vs Russia | 2.27 | 3.17 | 3.28 |
| 21:00 | 5940 | Scotland U21 vs Sweden U21 | 3.01 | 3.12 | 2.23 |
| 21:30 | 5876 | Hungary vs Estonia | 1.46 | 4.25 | 7.10 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# TFF YAZIPONGEZA SIMBA, YANGA KUTETEMESHA CAF

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limezipongeza Klabu za Simba na Yanga kwa kufuzu robo fainali za michuano ya kimataifa, ikisema mafanikio hayo pamoja na mambo mengine yanatokana na kuimarika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, amesema mbali na kuzipongeza klabu hizo kwa kuliheshimisha taifa, lakini pia amewapongeza wadau wote wa soka, wakiwamo wadhamini wa Ligi Kuu, ambao nao wamechangia kwa kiasi kikubwa kuifanya kuvutia watu wengi ndani na nje ya nchi.**

Alisema wadhamini hasa wanaoonyesha mechi hizo kwenye televisheni na kutangaza kwenye redio wamesababisha kuvutia wachezaji wengi wakubwa kuja kucheza soka nchini, pia kufuatiliwa na mashabiki wengi barani Afrika, kiasi kwamba si ajabu sasa kwa mchezaji wa nje anayecheza soka nchini kuchaguliwa kwenye kikosi cha taifa, tena kwenye nchi kubwa na zenye majina, kitu ambacho huko nyuma ilikuwa kama ndoto.

"Makundi yalikuwa na ushindani mkubwa na vigogo kadhaa wameangukia pua, lakini Simba na Yanga zimevuka, ni jambo kubwa.

"Kwangu inaonyesha zaidi ni kukua kwa mpira wa Tanzania, hususan ligi yetu inaonyesha jinsi gani watu wamekuwa wakiiweka kwenye viwango vikubwa vya ligi barani Afrika na unaona kabisa matokeo haya yanaakisi kile ambacho kimekuwa kikiwekezwa kwenye ligi yetu.

Ni jambo kubwa sana limefanyika mimi kwangu nipongeze wadau wote, Yanga pamoja na Simba, lakini niende mbele zaidi kwa wadau wote waliowekeza, wameifanya kuwa moja ya ligi ambayo imevutia watu wengi na wengine wameanza kuvutika kuja kuwekeza.

"Imevutia wachezaji wengi wakubwa kuja kucheza hapa na kufuatiliwa sana Afrika, ilikuwa ni nadra sana kuona mchezaji wa nje anayecheza Ligi Kuu Tanzania Bara kuchaguliwa kwenye timu za taifa za nchi zao zenye majina makubwa. Ilikuwa ni ndoto wakati huo, lakini kwa sasa si ndoto tena ni kweli tunaona," alisema Kidao.

Simba imetinga robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuifunga Horoya ya Guinea mabao 7-0 Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na kufikisha pointi tisa, ikitinga ikiwa na mechi moja mkononi, Yanga pia ikitinga ikiwa imesalia na mchezo mmoja wa Kombe la Shirikisho Afrika, ikishinda kwenye uwanja huo huo mabao 2-0 dhidi ya US Monastir ya Tunisia na kufikisha pointi 10.



Mwanariadha Joseph John, akiruka viunzi wakati akifanya mazoezi kujiandaa na michuano ya kitaifa inayotarajiwa kufanyika Mei mwaka huu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba Queens, Yanga Princess

INATOKA UKURASA 24

kwanza, hatuhitaji kupoteza hata mechi moja, hii ni 'dabi', kama tunahitaji kuchukua ubingwa lazima tujitume kupambana kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri," alisema.

Aliongeza kuwa mechi ya awali hawakuifahamu vema Yanga Princess, lakini amewaona madhaifu na ubora wao hivyo, anajua ataingia na mbinu gani ili kutafuta ushindi katika mchezo wa leo.

Kocha Msaidizi wa Yanga Princess, Fred Mbuna, alisema wako salama na wamefanya maandalizi ya kutosha kwa ajili ya mchezo wao wa leo.

Alisema wamefanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo miwili iliyopita ambayo walipata sare dhidi ya Mkwawa Queens na sasa wanahitaji matokeo mazuri katika mchezo huo wa dabi.

"Nimetengeneza timu yangu kwa ajili ya kucheza mchezo wa dabi kwa kufanya kazi madhaifu ya kikosi chetu pamoja na kufahamu ubora wa wapinzani wetu, ninaimani tutaonyesha mpira mzuri," alisema Mbuna.

## Simba: Tunavunja mwiko CAF

INATOKA UKURASA 24

kwa umakini ule ule kwa sababu mpira wa miguu usipouheshimu mchezo uwe wa kirafiki, uwe na umuhimu au hauna, jukumu lako ni kucheza kwa heshima ile ile kwa sababu ukiuchukulia poa na ukifungwa mabao mengi, unabaki na rekodi mbaya ndani ya timu yako, kwa hiyo tutakwenda kucheza mechi yetu na Raja Casablanca Machi 31, mwaka huu, tukiwa na ubora ule ule," alisema meneja habari huyo.

# Michezo

Jumatano Machi 22, 2023

Nipashe




Stars kamili kuivaa Uganda UKURASA 20

# Simba: Sasa tunavunja mwiko CAF

## ●●● Yasema waje Mamelodi Sundowns, Wydad Casablanca, Al Hilal ama Esperance, safari hii wanaitaka...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa mara nne ndani ya miaka mitano, Klabu ya Simba imesema sasa imechoka kuishia hatua hiyo na inataka kwenda mbali zaidi, hivyo ili kutimiza azma hiyo wameanzisha kaulimbiu ambayo itatumiwa kuelekea kwenye mechi yao ya robo fainali, isemayo 'Tunavunja mwiko'.

**Jumamosi iliyopita, Simba ilifanikiwa kutinga hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuiangamiza Horoya ya Guinea mabao 7-0, na kufikisha pointi tisa kwenye Kundi C, ikiwa ni mara ya tatu kwenye Ligi ya Mabingwa na mara moja kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika.**

Hata hivyo, Simba imefuzu hatua hiyo ikiwa bado ina mechi moja mkononi dhidi ya Raja Casablaca ya Morocco, ambayo ni kinara wa Kundi hilo la F.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, amesema baada ya safari zote za timu yao kuishia hatua hiyo, safari hii hawatokubali na wanaelekea kucheza mechi ya robo fainali wakiwa na kaulimbiu ya 'Tunavunja Mwiko.'

"Safari hii kaulimbiu yetu kwenye robo fainali ni 'Tunavunja Mwiko'. Maana yake ni tunavunja mwiko wa kuishia robo fainali, tumeshafuzu sana robo fainali, tumeshacheza sana, hii ni ya nne, Ligi ya Mabingwa tatu na Shirikisho moja. Tumekuwa tukiishia hapa hapa, safari hii tunavunja mwiko wa kuishia hapa na kwenda hatua inayofuata zaidi.

"Ukitazama timu ambazo zinaonekana tunakwenda kucheza nazo ni Mamelodi Sundowns, Wydad Casablanca, JS Kabylie, Al Hilal, Esperance au CR Belouizdad, mimi niseme mpinzani yeyote yule kati yao, sisi tuko tayari kucheza nao, wakati tunakwenda kucheza ligi hii, tulijua tunakwenda kucheza na wakubwa wenzetu na wakubwa wengine waliotuzidi," alisema Ahmed.

Akizungumzia ushindi mkubwa dhidi ya Horoya, alisema Simba imeweka historia kubwa kwenye soka la nchi hii kwa sababu mara nyingi timu za Tanzania ndizo ambazo zimekuwa zikifunga mabao mengi na si kushinda.

"Tumezoea kuona mabao mengi zikifungwa timu za Tanzania, lakini safari hii ni kinyume chake, mabao mengi imefunga timu ya Tanzania kwa hiyo ni historia kubwa tumeiweka, pia ni historia kubwa barani Afrika kwenda kupata ushindi wa mabao saba na iliyofungwa si mtu wa kawaida, ni Horoya ambaye ni mbabe kwenye michuano hii ya Ligi ya Mabingwa, lakini Jumamosi iliyopita alijichanganya akala pumzi ya moto.

"Mnyama anaingia kwenye robo fainali kwa kishindo kweli kweli, na mechi zote zilizochezwa wiki hii, ni Simba pekee ndiyo iliyopata ushindi mkubwa wa mabao 7-0, hivyo unaona ni kazi kubwa na nzuri iliyofanywa kuweza kuandika ushindi huo. CAF imetikisika, Afrika imeogopa na Guinea wametetemeka," alisema.

Pamoja na kufuzu, Ahmed alisema watakwenda kucheza mechi ya mwisho ya makundi wakiwa na ari ile ile na hawatoidharau kwa kuwa wameshafuzu.

"Tutaenda Morocco kucheza

INAENDELEA UKURASA 23



Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama, ambaye ni kinara wa mabao hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika, akiwa tayari amecheka na nyavu mara nne. **PICHA: SIMBA**

## Simba Queens, Yanga Princess dabi la kibabe

**Na Saada Akida**

WATANI wa jadi kwa upande wa soka la wanawake, Simba Queens na Yanga Princess, leo wakishuka katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam kuonyeshana ubabe wa nani zaidi atakayeweza kuondoka na pointi nne msimu huu baada ya mchezo wa raundi ya kwanza kugawana pointi moja moja, makocha wa timu hizo kila mmoja ametamba "acheni waje".

Katika mchezo huo wa Ligi Kuu ya Wanawake ambao Yanga Princess ni mwenyeji, waamuzi watakaoamua mechi hiyo ni Jonesia Rukyaa atakuwa kati akisaidiwa na Janet Balama na Fatma Mambo.

Katika mchezo huo Simba Queens inahitaji ushindi ili kuendelea kung'ang'ania kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo huku Yanga Princess nao wakihitaji matokeo mazuri ili kuweza kupanda juu ya msimamo wa ligi hiyo.

Simba Queens wapo kileleni mwa msimamo wakiwa na pointi 26 sawa na Fountain Gate iliyopo nafasi ya pili kutokana na kuzidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa, wakati JKT Queens akishika nafasi ya tatu kwa alama zake 25 na Yanga Princess ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 21.

Timu hizo zinashuka dimbani zikiwa na kumbukumbu ya mechi ya mzunguko wa kwanza kutoka sare ya bao 1-1, katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kocha Mkuu wa Simba, Charles Lukula, akizungumza na Nipashe jana, amesema kikosi chake kipo tayari kwa ajili ya kutafuta pointi tatu dhidi ya Yanga Princess leo.

Alisema hana majeruhi hata mmoja na mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wao anahitaji pointi ili kufikia malengo yao.

"Mechi ya kwanza tulicheza tukiwa nafasi ya nne, kesho (leo)tunacheza tukiwa nafasi ya

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >